ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	-	SPIKA
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge

10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais
19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya

		Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Mihayo Juma N'hunga	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais wa Zanzibar/ Jimbo la Mwera
22. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ / Jimbo la Micheweni
23. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
24. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
25. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
26. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
27. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Naibu Waziri wa Uwezeshaji,Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake
28. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo,

		Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
30. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
31. Mhe. Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
32. Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil	-	Uteuzi wa Rais
33. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
34. Mhe. Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
35. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele
36. Mhe. Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi
37. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Nafasi za Wanawake
38. Mhe. Asha Abdalla Mussa	-	Jimbo la Kiwengwa
39. Mhe. Bahati Khamis Kombo	-	Jimbo la Chambani
40. Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-	Nafasi za Wanawake
41. Mhe. Hamad Abdalla Rashid	-	Jimbo la Wawi
42. Mhe. Hamida Abdalla Issa	-	Nafasi za Wanawake
43. Mhe. Hamza Hassan Juma	-	Jimbo la Shaurimoyo
44. Mhe. Hassan Khamis Hafidh	-	Jimbo la Welezo
45. Mhe. Hidaya Ali Makame	-	Nafasi za Wanawake
46. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)	-	Jimbo la Mtoni
47. Mhe. Jaku Hashim Ayoub	-	Jimbo la Paje
48. Mhe. Khadija Omar Kibano	-	Jimbo la Mtambwe
49. Mhe. Machano Othman Said	-	Jimbo la Mfenesini
50. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti	-	Jimbo la Mtopepo
51. Mhe. Makame Said Juma	-	Jimbo la Kojani
52. Mhe. Maryam Thani Juma	-	Jimbo la Gando
53. Mhe. Masoud Abrahman Masoud	-	Jimbo la Bububu
54. Mhe. Miraji Khamis Mussa	-	Jimbo la Chumbuni
55. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha	-	Jimbo la Mtambile
56. Mhe. Mohamed Said Mohamed	-	Jimbo la Mpendae
57. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali	-	Jimbo la Uzini

58. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf	-	Jimbo la Bumbwini
59. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame	-	Nafasi za Wanawake
60. Mhe. Mussa Ali Mussa	-	Jimbo la Ole
61. Mhe. Mussa Foum Mussa	-	Jimbo la Kiwani
62. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	-	Nafasi za Wanawake
63. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis	-	Nafasi za Wanawake
64. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini	-	Jimbo la Dimani
65. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy	-	Jimbo la Chaani
66. Mhe. Nassor Salim Ali	-	Jimbo la Kikwajuni
67. Mhe. Omar Seif Abeid	-	Jimbo la Konde
68. Mhe. Panya Ali Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
69. Mhe. Rashid Makame Shamsi	-	Jimbo la Magomeni
70. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa	-	Nafasi za Wanawake
71. Mhe. Said Omar Said	-	Jimbo la Wingwi
72. Mhe. Said Hassan Said	-	Mwanasheria Mkuu
73. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma	-	Nafasi za Wanawake
74. Mhe. Salma Mussa Bilal	-	Nafasi za Wanawake
75. Mhe. Shaib Said Ali	-	Jimbo la Chonga
76. Mhe. Simai Mohammed Said	-	Jimbo la Tunguu
77. Mhe. Sira Ubwa Mamboya	-	Uteuzi wa Rais
78. Mhe. Suleiman Makame Ali	-	Jimbo la Ziwani
79. Mhe. Suleiman Sarahan Said	-	Jimbo la Chakechake
80. Mhe. Tatu Mohamed Ussi	-	Nafasi za Wanawake
81. Mhe. Ussi Yahya Haji	-	Jimbo la Mkwajuni
82. Mhe. Viwe Khamis Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
83. Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Nafasi za Wanawake
84. Mhe. Yussuf Hassan Iddi	-	Jimbo la Fuoni
85. Mhe. Zaina Abdalla Salum	-	Nafasi za Wanawake
86. Mhe. Zulfa Mmaka Omar	-	Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem	-	Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Kumi na Tano - Tarehe 29 Mei, 2017

(Kikao kilianza Saa. 3.00 asubuhi)

Mhe. Spika, (Zubeir Ali Maulid) alisoma dua

TAARIFA YA SPIKA

Waheshimiwa Wajumbe, katika Kikao cha Baraza la Wawakilishi cha Tarehe 18 Mei, 2017 Mhe. Rashid Makame Shamsi aliuliza swali la nyongeza kwa Wizara ya Habari, Utalii na Michezo na kuahidiwa kujibiwa kwa maandishi, aidha katika kikao cha Tarehe 22 Mei, 2017 Mhe. Suleiman Sarahan Said aliuliza swali la nyongeza kwa Wizara hii ya Habari, Utalii na Michezo naye aliahidiwa kujibiwa kwa maandishi. Katika kutimiza masharti ya Kanuni ya 40(4) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi toleo la 2016 Wizara hiyo imeleta majibu kama Waziri wa Wizara hiyo alivyoahidi.

Waheshimiwa Wajumbe sasa namuomba Mhe. Waziri wa Habari, Utalii na Michezo asome majibu ya maswali ya nyongeza yaliyoulizwa na Waheshimiwa Wajumbe hao ahsante.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii na Michezo: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kujibu majibu ambayo yameulizwa na Waheshimiwa wajumbe wawili Mhe. Rashid Makame Shamsi wa Jimbo la Magomeni pamoja na Mhe. Suleiman Sarahan Said wa Jimbo la Chake Chake ambayo aliahidiwa kujibiwa kwa maandishi.

Mhe. Spika, wakati tunajibu suala Na. 11 niliulizwa suala la nyongeza na Mhe. Rashid Makame Shamsi alitaka kujua *tartan* imewekwa mwaka gani, jibu la suala hilo ni kama ifuatavyo:

Mpira wa kukimbilia wa uwanja wa Amaan imewekwa mwaka 1985 kwa mara ya kwanza na baadae mwaka 2010 ulifanyiwa matengenezo makubwa, vile vile nyasi bandia za kiwanja ziliwekwa mwaka 2014.

Aidha nilipokuwa najibu suala Na. 30 Mhe. Suleiman Said Sarahan katika suala la nyongeza alitaka kujua ni kiasi gani cha fedha anacholipa mtalii kutoka nje anapoingia katika makumbusho yetu na majibu ya suala hilo ni kama ifuatavyo.

Watalii wanaoingia katika makumbusho yetu wanalipa dola tatu kwa mgeni kwa siku au Shilingi za Kitanzania elfu sita na kwa watoto huwa wanalipa Dola 1, au U$ Dola 1au Shilingi za Kitanzania 2000. Ahsante Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais (Kny.Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko): Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Biashara Viwanda na Masoko kwa Mwaka 2017/2018. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Hamad Abdalla Rashid (Kny:Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo): Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kuhusu Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa Mwaka 2017/2018. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 98

Mwaka wa Kiislamu Kufanywa Siku ya Mapumziko

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:

Kwa muda mrefu Serikali imekuwa na kigugumizi kuhusu kuifanya siku ya mwaka mpya wa Kiislamu kuwa siku ya mapumziko. Suala hili licha kuwa halina matatizo kwa Waumini wa dini ya Kiislamu ambao ndiyo wengi hapa

nchini kwetu, Serikali bado imelikalia na kila linapoulizwa Serikali wamekuwa wanajibu kuwa ni jambo zuri na watalichukuwa na kulifanyiakazi.

(a) Ni muda gani huo hadi leo hii bado Serikali inalifanyiakazi

(b) Maadhimisho mengine kama vile Maulid Nabii yanakuwa na siku ya Mapumziko na hakuna tatizo lolote, kwanini Serikali inasita kuufanya mwaka mpya wa Kiislamu kuwa siku ya Mapumziko.

(c) Lini Serikali itaruhusu mwaka mpya wa Kiislamu kuwa siku ya mapumziko kitaifa.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako, naomba kumjibu Mhe..Mwakilishi swali lake Nam. 98 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, Serikali inaendelea kulifanyia kazi suala hili kwa kujadiliana na kukusanya maoni kutoka kwa makundi tafauti katika jamii juu ya haja ya kuifanya siku hiyo kuwa ni siku ya mapumziko.

(b) Mhe. Spika, Serikali haijasita kuifanya siku hii kuwa ni siku ya mapunziko, bali utendaji wa Serikali inayoheshimu Utawala Bora maamuzi yake hufikiwa baada ya kuwashirikisha wananchi wake.

(c) Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haitasita kuifanya siku ya mwaka mpya wa kiislamu kuwa ni siku ya mapumziko iwapo itaonekana ipo haja ya kufanya hivyo na iwapo mamlaka husika zitajiridhisha

Pamoja na kwamba maoni ya walio wengi yanashauri juu ya haja hiyo. Nimuombe Mhe. Mwakilishi aendelee kuwa mstahamilivu wakati Serikali inalifanyia kazi suala hili.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa masikitiko makubwa sana na Mwenyezi Mungu shahidi na wajumbe waliopita wengi walikuwa shahidi Mhe. Mohammed Aboud amekuwa shahidi wa suala hili, lakini anayehangaika hachoki. Baada ya majibu ya Serikali kutoniridhisha mimi na baadhi ya wengi waislamu naomba kuuliza masuala madogo ya nyongeza.

a) Makundi gani yaliyoitwa kutoa maoni yao ukizingatia tuko katika mwezi mtukufu wa Ramadhani kuseme ukweli ni jambo muhimu na makundi mangapi yaliyobaki ukizingatia hili ni mwaka wa saba.

b) Ni muda gani mtahakikisha makundi yaliyobaki mtayaita kama hili suali liko kwelini hasa, hili suala ni la muda mrefu Mhe. Naibu Waziri, na hii ngoma umeikuta tu wala siwezi kukulaumu miaka saba Mhe. Mohammed Aboud Waziri Makini analijua suala hili.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye kifungu (a) n (b) kama ifuatavyo.

(a) Mhe. Spika, idadi ya Makundi naomba nijibu swali hili kwa maandishi kwa sababu sina idadi hali ya hayo makundi ambayo yameshafikiwa.

(b) Ni muda gani suala hili litapatiwa ufumbuzi, napenda kumjulisha Mhe. Mwakilishi kwmba suala hili ni zito sio suala la leo na kesho, kwa sababu unapozungumzia suala la siku hii kuifanya iwe siku ya mapumziko ni suala ambalo linahitaji mambo mbali mbali kuzingatiwa. Kwa hivyo nirejee kusema kwamba tuendeleeni kuvuta subra Serikali ina nia ya jambo hili kulitelekeza kama ambavyo wananchi na Mhe. Jaku Hashim anahitaji kufanya hivyo, lakini kubwa zaidi tuendelee kufanya subra suala hili sio la kufanya masaa kwa maana ya leo na kesho hapana wacha tushirikishe wananchi wetu, wacha tushirikishe vikundi mbali mbali vya dini na taasisi zetu mbali mbali.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Ahsante sana Mhe. Spika, ramadhan kareem kwa waislam wote mimi nataka kuuliza suala la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

a) Kwa kuwa nchi nyingi duniani hasa kwenye dini nyengine ikiwemo Wakristo, Wahindu na kabila nyengine wao wameweka siku maalum za Krismas na Diwali kuwa siku za mapumziko kama vile mwaka wa Kiislam unavyokuwa, ni sababu zipi hasa za msingi kwamba wenzetu siku zao wanazithamini wameweka *holiday* sisi mwaka wa Kiisalam mpaka hivi leo na nchi iliyokuwa na waislam asilimia 99% haijawekwa siku hii *holiday*.

b) Katika makundi mliyoyaita ni watu wangapi mliowaita na wepi wamesema ndio na wepi wamekataa na ni wa aina gani mmechanganya dini zote ama dini moja.

Mhe. Spika: Mheshimiwa jibu swali la mwanzo kwa sababu swali la pili liliulizwa pia na Mhe. Jaku na ameahidi kulijibu kwa maandishi. Mhe. Waziri.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, nipende kumjulisha Mhe. Nadir kwamba siku pia na sisi tunaithamini kama ambavyo tunaithamini siku nyengine, kwa hivyo kama nilivyosema jawabu langu la awali kwamba tunaendelea kufanya utaratibu siku hii nayo pia kuitambua. Kwa sababu sasa hivi bado haijawa rasmi, lakini sio kwamba hatuithamini tunaithamini na shughuli mbali mbali tunashuhudia unapofikia mwaka huu mpya wa Kiislam sherehe mbali mbali zinafanyika, kwa hivyo tunaithamini kiufupi lakini siku kama nilivyosema jawabu langu la awali kwamba tuendelee kusubiri Serikali ina nia ya kulifanyia kazi suala hili.

Nam. 136

Programu Ndogo ya Matrekta na Maendeleo ya Huduma ya Kilimo

Mhe. Omar Seif Abeid - Aliuliza:

Kwa kuwa katika Programu ndogo ya Matrekta na Maendeleo ya huduma ya Kilimo ya 2016/2017 Serikali kupitia Wizara ilipanga kulima jumla ya ekari 33,590 kwa Unguja na Pemba, ambapo pia kilipanga kuzalisha tani 250 za mbegu ya mpunga kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji.

(a) Je, Wizara imelifikia lengo la kuzalisha tani 250 za mbegu ya mpunga na kama halikufanikiwa, Je, ni tani ngapi za mbegu hiyo zilizozalishwa.
(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuachana na mbegu ya Nerica ambayo inaonekama haina tija kubwa sana kwa Wakulima wetu wa hapa Zanzibar na badala yake kutafuta mbegu mbadala.
(c) Je, Serikali ilikamilisha mpango wake wa kununua mbolea tani 700 na lita 1500 za dawa za kuulia wadudu na kuwafikishia wakulima kwa wakati uliokusudiwa.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi – Alijibu:

Mhe. Spika, kwa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nambs 136 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuayavyo:-

Mhe. Spika, kwa kuwa program ndogo ya Matrekta na Maendeleo ya huduma ya kilimo 2016/2017 Serikali kupitia Wizara imepanga kulima jumla ya hekta 33,590 kwa Unguja na Pemba, Pia tulipanga kuzalisha tani 250 za mbegu ya mpunga kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji.

(a) Mhe. Spika, Wizara inaendelea na kutekeleza lengo la kuzalisha tani 250 za mbegu ya mpunga kupitia wakulima wa skimu za umwagiliaji katika msimu wa masika 2017. Kiwango cha mbegu hizo kitajulikana baada ya mavuno ambayo yanatarajiwa kuanza kufanyika mwezi wa Julai 2017.

(b) Mhe. Spika, Serikali inaendelea na kazi za utafiti shirikishi wa mbegu ya *NERICA* kupitia mpango wa *TANRICE* 2. Utafiti huo unahusisha uchunguzi juu ya viwango vya uzalishaji kwa eneo na kukubalika kwa wakulima kwa ajili ya matumizi ya chakula. Kuendelea au kuachana na mbegu hiyo kutategemea na matokeo ya utafiti huo.

(c) Mhe. Spika, Serikali ilinunua mbolea tani 700 (TSP tani 100 na UREA tani 600) na lita 15,000 za dawa za kuulia magugu. Pembejeo hizi zote zilinunuliwa na kugawiwa kwa wakati uliokusudiwa.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Spika, nashukuru kwa majibu yake mazuri lakini kabla ya hapo nilikuwa na swali langu dogo la kumuuliza lenye kipengele (a) na (b).

Ingawa katika jibu lake Mheshimiwa sikulisikia vizuri lakini humu ninamosoma niliona kwamba hii mbegu ya NERICA ambayo tuliizungumza niliulizia swali ni mbegu ambayo imezungumzwa kwa muda mrefu.

(a) Sasa nilitaka nijue ni lini utafiti huu wa mbegu hii ya NERICA utakamilika ili iweze kujulikana kama kweli inafaa kutumika hapa kwetu au haifai.

(b) Lakini ili tufikie lengo la uzalishaji tunahitaji utafiti na katika utafiti kunahitaji gharama kubwa Je, kwenye bajeti yako hii ya 2017/2018 kitengo cha utafiti kwa kilimo umekitengea kiasi gani ili kukipa nguvu ya kuweza kufanya utafiti na kuongeza kilimo zaidi.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, kwanza nataka nishukuru sana swali la Mhe. Omar kwa sababu hii mbegu ya *NERICA* imekuwa ikisemwa sana na ikizungumzwa sana, kwa kawaida utafiti

unapofanyika unatakiwa ufanyike na ukamilike kwa bahati mbaya ilipofanyiwa utafiti *NERICA* ilifikia pahala utafiti ukaachiwa kati kati baadae ikatangazwa *NERICA* kwamba ni mbegu nzuri, utafiti gani ambao haukukamilika.

La kwanza ambalo halikukamilika je, mpunga huu ukishalimwa namna ya kuuchakachua ukapata mchele *process* yake ikoje, ikagundulikana kumbe kwa wakulima kwamba ni mwingi unaobakia ndani kama ni chua kuliko unaosafika, kwa maana hiyo eneo hili utafiti haukukamilika.

Eneo la pili ambalo lilionekana lina matatizo ni eneo la utamu wenyewe wa mpunga wenyewe, unajua watu wetu wamezoea sana ringa na kadhalika, lenyewe nalo halikukamilika utafiti wake kwa hivyo tukarudi tena tukasema kwa kosa lililofanyika la kiutafiti utafiti haujakamilika, hebu tukamilishe *exercise* ya utafiti mpaka mwisho tuone manufaa yake.

Lakini moja ambalo tumegundua katika *NERICA* ni kwamba ni mbegu nzuri ambayo inaweza kuota vizuri kwa kiwango kikubwa, lakini ina mapungufu hayo mawili ndio maana utafiti sasa hivi unaendelea, suala la utafiti sio rahisi sana kusema ni lini utakamilika ni *process* ambayo tunategemea ikamilike na hatimae tuwatangazie wananchi. Kitu tunachotaka kukifanya sasa hivi ni kutaka kuwa na mbegu ya taifa mpaka leo sisi hatuna mbegu ya taifa, sasa huwezi ukawa na nchi halafu haina mbegu ya taifa tuna mbegu kama nne mpaka tano tumeshachagua tumefanya pale Tibirinzi majaribio, tumefanya hapa Unguja majaribio tunategemea kituo chetu cha utafiti sasa kitatwambia ni mbegu gani na gani hasa inafaa kuwa ni mbegu ya taifa ukiacha na mbegu nyengine ambazo wanatumia wananchi.

Lakini utafiti wake lazima ukamilike ndio turudi kwa wananchi kuwaeleza, bila ya utafiti kukamilika tukawa na uhakika hatutorudia kosa tulilolifanya la *NERICA* kwenda kutangaza kabla utafiti haujakamilika.

Mhe. Spika, fedha ambazo zimepangwa mara hii kwa bajeti ya utafiti ni kama Shs. 3,000,000/ ambazo tunategemea kwamba kwa sababu taasisi yetu inajitahidi sana kushirikiana na taasisi mbali mbali za kimataifa fedha nyengine zitatoka kwa wafadhili, lakini kwa upande wa Serikali tumetenga kiasi hicho.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa na mimi nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri lakini ningependa nimuulize swali dogo la nyongeza.

Kwa vile huu utafiti wa hii mbegu ya *NERICA* haujakamilika lakini pia hatujapata ile mbegu ambayo itakuwa hii ni mbegu ya taifa ili wananchi waweze kuitumia na kuweza kupata mpunga mwingi.

Je. Wizara ina mpango gani wa kuwaimarisha wananchi hawa wanaolima kilimo hichi cha mpunga ili wakaweza kuendelea na huu ukulima wanaoendelea nao na hizi hizi mbegu ambazo wako nazo sasa hivi ambazo wanaendelea nazo kuzipanda.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa swali la Mheshimiwa zuri sana, kama mnakumbuka hivi karibuni hata kwnye picha mmemuona Mhe. Makamu wa Rais akienda Cheju kwenye ukulima wa shadidi, zile ni mbegu ambazo tumezijaribu tumeshirikiana na wakulima na tuko katika *process* ya kuona kwamba je, sasa inaridhisha hii mbegu kutumika, kwa bahati nzuri Mhe. Spika, tumegundua kwamba mbegu ambazo tunazitumia kama nne kuna mbegu mmoja inatokea Pakistan tunaitumia na yenyewe kwa kweli inazalisha vizuri na watu wanaipenda tatizo lake kidogo ni suala la muda, na kuna mbegu mbili ambazo wananchi wenyewe wame wamezipenda kwa kushirikiana na kituo chetu tunaendelea nazo hivi sasa. Mimi naamini wananchi tumewashirikisha katika *exercise* nzima tunaamini kabisa tunaweza tukafanikiwa. Tatizo ambalo tumelipata mara hii tumesambaza mbegu, lakini wakulima wetu hasa sehemu ya Pemba ile mbegu tuliyoisambaza nzuri wameila ilie ya kwao ya asili wameitumia, kwa hivyo utakuta mashamba mengi, yameota mpunga mzuri lakini ni mbegu ambayo ni asili wameacha mbegu ile nyengine wamekula.

Sasa hili ni tatizo moja ambalo tunalikabili, na mimi naamini wananchi baadae wataanza kubadilika, watumie mbegu ambazo wamezifanyia utafiti na kwa bahati nzuri, mbegu hizi tunazinunua kwao nataka nimshukuru sana Rais wetu tumshukuru sana, wananchi wanalima mbegu Serikali inanunua kwa bei ya Shilingi 1,200/- , mbegu hiyo hiyo inapofika msimu tunawauzia wakulima kwa shilingi 200 hii ni Serikali ya ajabu sana inayotoa huduma kwa watu wake, mimi naomba tuwashukuru sana Serikali.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Spika na mimi kwa kunipa fursa hii ya kuuliza swali dogo sana la nyongeza. Lakini kabla nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa majibu mazuri na fasaha ya waulizaji waliotangulia.

Mhe. Spika, nimemfahamu sana Mhe. Waziri alipojibu juu ya suala la mbegu hii ya nerika, lakini katika majibu yake alisema tafiti ilisita na walitaka

kuendeleza, lakini imebainika kwamba mchele huu au mpunga huu ladha yake wananchi hawajaridhika nayo yaani si nzuri. Sasa je, kuna haja gani ya kuweza kuendelea na huo utafiti hatuoni kwamba tutakuwa tunapoteza fedha za Serikali. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Rashid Makame Shamis kama ifuatavyo:

Kwanza Mhe. Spika, si watu wote kwamba Nerika hawaipendi ni baadhi tu ya wakulima na watumiaji, lakini hapa Zanzibar sasa hivi unaona watu wote wanakula mapembe wala hawayapendi hata kidogo, lakini wanayala mapembe kwa wingi kweli kweli, na inaletwa tani thamani elfu za mapembe hapa kila mwaka. Hawayapendi watu cha kwanza kabisa ambacho tuna *fight* katika Serikali ni kuhakikisha kabisa tunaondokana na suala la njaa, na katika suala la njaa utatafuta mbegu ambayo itakupa *production* kubwa ili kwanza ukabiliane na lile tatizo ulo nalo, hizi *choice* za watu zitakuja kwa sababu tuna mbegu aina kama sita watu watachagua sisi mimi nataka ringa, nataka nini, lakini kwanza watu washibe. Nerika ina nafasi ya kuwashibisha watu wetu, kwa hio ndo maana tunaendelea na utafiti, lakini njengine ambao tunaendelea na utafiti ni nini, lakini lazima tujue sababu, kwa nini hauna *test* huo mpunga ndo lazima tuendelee na utafiti ndo maana ya utafiti, tutafute sababu ya kujua sababu yake ni ipi.

Mimi nafikiri tuendelee wala hatupotezi fedha, ni wajibu wetu kufanya utafiti na utafiti ndo kilimo ndio maendeleo ya nchi.

Nam. 167

Masharti ya Uwanachama wa Shirikisho la Vyama vya Mpira Barani Afrika (CAF)

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:

Hivi karibuni Zanzibar imefanikiwa kupata uwanachama wa Shirikisho la Vyama vya Mpira wa Miguu Afrika (CAF), kutokana juhudi kubwa zilizofanywa na aliyekuwa Waziri wa Habari, Sanaa na Michezo Mhe. Nape Moses Nnauye kwa kushirikiana na TFF, Uongozi wa Wizara na ZFA ambao kwa pamoja wanastahili pongezi.

(a) Je, Wizara inayoshughulikia Michezo Zanzibar imechukuwa hatua gani kuwaelimisha wahusika mbali mbali wa Michezo Zanzibar ambao

wanapeleka masuala ya michezo mahakamani kinyume na masharti ya uwanachama wa CAF ambao mwanachama anaweza kupoteza uanachama endapo masuala ya michezo yataamuliwa mahakamani.

(b) Hatua gani Serikali itachukuwa kuwataka wale wote waliopeleka madai yao mahakamani kuyaondowa na kupiga mstari wa kuanza kujenga upya Chama cha Mpira wa Miguu Zanzibar (ZFA) na maendeleo ya mpira Zanzibar.

(c) Je, baada ya ZFA kuwa mwanachama wa CAF mpango gani umefanyika kubadili sera ya michezo na Sheria zake ili kuenda sambamba na uwakilishi wa soka ya Zanzibar kimataifa, ikiwemo kumaliza migogoro ya michezo nje ya mahakama.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo - Alijibu:

Ahsante sana Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi Jaku Hashim Ayoub swali lake, Namba 167 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, Wizara yangu itahakikisha kuwa inawaelimisha wadau wote wa michezo kuelewa na kutambua kwamba tumekubaliwa kuwa wanachama kamili wa Shirikisho la mpira wa Miguu Barani Afrika (CAF).

Vile vile, Mhe. Spika, katika swali hilo (a) pia wakati umefika sasa kutanabahisha wadau na watu wa michezo wote, ikiwemo wahusika wa mchezo wa mpira wa miguu kwamba madai yote, yanayohusu michezo kupelekwa katika vyombo vya michezo na hasa vyombo vya usuluhisho wa michezo kama kanuni na katiba zao zinavyoelekeza.

(b) Ili kuona hatuendi kinyume na maelekezo ya CAF, Wizara itawaita wale wote waliohusika kupeleka kesi mahakamani ili kuhakikisha kwamba kama kuna kesi yoyote imeyobakia ni kuzifuta kwa mujibu wa taratibu za kimichezo zilizowekwa.

(c) Mhe. Spika, baada ya kuwa mwanachama kamili wa CAF, Serikali itaelekeza nguvu zake zote katika kukisimamia Chama cha Mpira wa Miguu Zanzibar (ZFA), ili kuhakikisha kuwa wanafuata maelekezo ya CAF na FIFA kabla hatujapata uanachama ikiwemo kusitisha masuala ya michezo kupelekwa katika mahakama za kawaida. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Waziri naomba kuuliza maswali madogo yenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

(a) Kuna kesi ngapi zilizokuwapo Mahakamani hadi sasa na wamechukuwa hatua gani kuwaita waliofungua kesi hio, ili kuwaelimisha au kuwapa mawaidha juu ya neema tuliyoipata hii tusiipige teke.

(b) Wizara ulisema itahakikisha kuwaelimisha muda mrefu kama Mjumbe wa Kamati mtachukua hatua hii ya chini ya Mwenyekiti wangu makini chini ya Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) tulikuta matatizo haya wenyewe kwa wenyewe hawaelewani viongozi kati ZFA na BMTZ ni lini kama wewe Waziri makini tuliokuamini, utaita timu zote au kuchukua ziara Unguja na Pemba kutoa elimu hiyo haraka iwezekanavyo.

Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Ahsante sana Mhe. Spika, napenda kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub, swali lake na nyongeza lenye kipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Kuhusu swali Namba za Kesi zilizokuwepo Mahamani ili nimjibu kisahihi nitakuletea kwa maandishi, lakini swali lako (b*). (Makofi)*

(b) Ni wazi kwamba Wizara yangu ina dhamira ya dhati kama ilivyofanya huko nyuma kabla kuwaita wana michezo, kuviita vilabu na kuwaita wadau wote wanaohusika, wakiwemo VETERAN ambao pia wote tushawaita ndani ya Wizara yetu jitihada hizo tutaziendeleza, na wale wote wanaohusika kupewa elimu hii kwenda kuisambaza kwengine tutawaita na kuwapa kipa umbele. Kwa hilo asiwe na wasiwasi Wizara inaendeleza hatua hizo.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante Mhe. Spika na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Spika, nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri na katika majibu yake amesema kwamba Serikali itaelekeza nguvu zake zote katika kusimamia Chama cha Mpira wa Miguu Zanzibar, lakini katika kusimamia hivyo haoni kwamba ipo haja sasa kubadilisha Katiba ya ZFA, na kuendana na miongozo na Katiba ya CAF kama ilivyosema yeye ili kuondoa migogoro na kwenda katika Vyama vya Mikoa pia badili ya Wilaya peke yake.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Ahsante sana Mhe. Spika, ni kweli yale aliyoyaeleza Mhe. Mwakilishi lakini nataka nimjibu kwamba hivi sasa ZFA imo katika hatua za mwisho za kukamilisha taratibu za

kurekebisha katiba, tuliyokuwa nayo na kuja na katiba mpya ambayo itaendana na ile inayofatana na ile inayofatana na masharti na maelezo ya uwachama wa CAF. Hivyo basi, naamini wazi masharti huwa yanabadilika kanuni huwa zinabadilika hivi sasa tutaendana kwa mujibu wa zile kanuni ziliopo. Zile zetu muda wetu zitakapokamilika tunaweza tukamjulisha Mjumbe. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Spika, kwa kuniona, Mhe. Spika, na mimi ningependa kumuuliza Waziri swali dogo tu moja la nyongeza.

Kwa kuwa Katiba yetu ya Zanzibar kwenye utangulizi wetu kifungu cha Pili kinasema kuwa "Tunatambua kwamba umoja wa Wananchi wa Zanzibar unatokana na ushirikiano wa miaka mingi tangu wakati wa mapambano ya kupigania uhuru hadi kufikia daraja hili ya mafanikio na inatokana na Siasa yetu ya Ujamaa na Kujitegemea".

1. Mhe. Spika, kwa kuwa nchi hii kuna viongozi wengi walijitokeza katika miaka ya nyuma kusaidia michezo yetu na hadi hivi sasa kuna kiongozi maarufu aliyekuwa Mwenyekiti Mstaafu wa ZFA ambae tunamtambua sisi kama Wazanzibari ndie aliyekuwa Kiongozi wetu kupigania Zanzibar, ili kufika katika eneo ambalo alofika. Je, Serikali inatambua kwamba Bwana Ali Tamim Ferej sasa hivi hali yake ya kiafya sio nzuri, na anatumia karibia dola elfu tatu kutibiwa saratani na Serikali inafikiria kufanya kitendo gani kuweza kumsaidia huyu Bwana.

2. Mara nyingi binaadamu sisi nchi yetu ina maeneo mengi, kupenda kuwaenzi watu baada ya wao wameshatangulia mbele ya haki je, Serikali haioni umuhimu kwenye Uwanja wa Gombani ulioko Pemba, tayari sasa ili kutafuta njia au kuanza mchakato kuanza ukaitwa Uwanja wa Ali Ferej Tamim Stadium. Ahsante sana.

Mhe. Spika: Mhe. maswali naona kama mapya yote, nafikiri ungeyaleta kwa utaratibu mzuri zaidi wa maandishi ni maswali mapya. Tunaendelea.

Nam. 136

Programu Ndogo ya Matrekta na Maendeleo ya Huduma ya Kilimo

(Mhe. Mjumbe aliyetaka kuuliza swali hilo ameliondoa.)

Nam. 101

Kuimarishwa Huduma za Matibabu ya Saratani Zanzibar

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohammed Shein anastahili pongezi kwa jitihada kubwa anazofanya katika maendeleo ya sekta ya afya nchini. Pamoja na hatua hizo kubwa, bado maradhi kama saratani yamekuwa yanaongezeka nchini na wananchi wanyonge hawamudu gharama za matibabu kama vile dawa na mionzi ambayo wanalazimika kufuta huduma hiyo katika Taasisi ya Saratani ya Ocean Road, jijini Dar es Salaam.

(a) Je, Serikali imejipanga vipi kuimarisha kliniki ya Saratani ya Mnazi mmoja kwa kuimarisha huduma za matibabu kwa njia ya dawa na mionzi.

(b) Serikali haoni ulazima wa kutafuta wafadhili wa kujenga miundombinu na vifaa kwa ajili ya matibabu ya saratani ili kuwapunguzia gharama wananchi za kufata matibabu hayo Dar es Salaam.

(c) Ni kiasi gani cha fedha kinahitajika ili huduma ya matibabu ya Saratani iweze kupatikana kwa ukamilifu katika Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Afya naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Paje swali lake Nam. 101 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza kabisa naomba nitoe shukrani za dhati na pongezi kwa Waheshimiwa Wawakilishi wa Baraza lako hili Tukufu kwa jinsi walivyokuwa wafuatiliaji wa huduma za Afya kwa wananchi wetu, Mheshimiwa Wawakilishi hao wanatuelekeza na kutushauri kwamba maslahi ya wananchi na hakuna kitu chengine.

(a) Mhe. Spika, kwanza kabisa nakubaliana moja kwa moja na hoja Mhe. Mwakilishi ya kuwa tunalo ongezeko kubwa la maradhi ya saratani hapa nchini, Wizara ya yangu imejipanga kuimarisha huduma hii katika Hospitali ya Mnazi Mmoja, kwa kuanzisha kliniki maalum ya magonjwa ya saratani kwa huduma zinazostahili. Kwa sasa tunao madaktari bingwa wawili *(Medical oncologist)* wanaotoa huduma za matibabu ya saratani. Aidha, Wizara yangu ina mpango wa kuanzisha huduma za mionzi kwa siku za baadae.

(b) Mhe. Spika Wizara imeshaandaa andiko la mradi *(concept note)* ya kujenga kituo husika cha matibabu ya saratani (*Oncology Centre)* nchini kwa sasa Wizara imo katika mchakato mkubwa wa kutafuta wafadhili wa kusaidiana na Serikali mradi huo.

(c) Mhe. Spika**,** jumla ya T.Sh 8,000,000,000/= zinahitajika ili huduma kamili ya matibabu ya saratani ziweze kupatikana kwa ukamilifu katika Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri wa Afya naomba kumuuliza maswali mawili madogo sana ya nyongeza yenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

(a) Kitengo cha Saratani ulipokuwa ukijibu hivi sasa karibu Mhe. Waziri wa Afya karibuni wagonjwa 600 hebu tueleze hivi karibuni Mungu akitujaalia katika siku hizi tarehe 2 au 3 tutakupitishia Bajeti yako je, Kitengo hichi kama kweli mmekijali hebu tueleze wananchi wapate kujua, mmetenga kiasi gani katika Bajeti kesho kutwa Mungu akituweka hai.

(b) Ni sababu gani hasa iliyopelekea mkaajiri Madaktari wawili tu bingwa kwa ajili ya utaalamu unaoitwa *(Medical oncologist)* ni sababu gani mkapelekea madaktari wawili kweli Wizara iko *serious* kutaka kuhudumia wananchi. Madaktari wawili na nafikiri Pemba hakuna kitengo hichi. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naomba nichukuwe nafasi hii kumjibu Mwakilishi wa Jimbo la Paje swali lake (a) na (b) kama ifuatavyo.

Mhe. Swali la mwanzo ni Kitengo kimetengewa kiasi gani naomba radhi sana hili nitamjibu kwa maandishi kwa sababu hii ni twakimu ya pesa naomba nitamjibu wa maandishi.

Lakini kuhusu wafanyakazi wawili Mheshimiwa kutokana na huduma tulizonazo sasa hivi katika Hospitali yetu ya Mnazi Mmoja, basi wanatosha kabisa na wala hawasumbuki lakini Wizara ina mpango katika wafanyakazi, ambao wanatarajiwa kuajiriwa tuna mpango wa kupeleka wafanyakazi wengine wawili kusaidiana na wale, lakini kwa sasa wale wanatoa huduma na kwa kweli hakuna malalamiko kwamba kuna wananchi, au wagonjwa wamekosa huduma kutokana na *shortage* ya *staff* katika kitengo kile.

Mhe. Zulfa Mmaka Omar: Ahsante Mhe. Spika, mimi nimuulize swali dogo la nyongeza.

Mhe. tunajua kwamba tatizo la Saratani liko sana hapa Zanzibar, na kule Pemba pia kuna watu wengi sana ambao wanasumbuliwa na tatizo hili, na tukiangalia kwamba pale Pemba hapana sehemu ambao watu wanakwenda kwa ajili ya kupata matibabu haya. Je, ni lini mtafikiria kuweka kitengo cha kuwahudumia wagonjwa hawa, ili waweze kuondokana na usumbufu wanaoupata wa kwenda Dar es Salaam na tukiangalia hali zao kifedha si nzuri ki hivyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naomba nichukuwe nafasi hii kumjibu.

Mhe. Sira Ubwa Mamboya: Ahsante Mhe. Spika, naomba kujibu swali hili la nyongeza pamoja na lile la mwanzo lililopita ili kufafanua zaidi, kuhusu huduma za *oncologist* katika wizara yetu ya Afya. Huduma za *oncologist* zina gharama kubwa sana na madaktari wawili waliokwisha tayarishwa ni mwanzo, na wizara haina tu mahitaji ya madaktari hao kensa kuna mahitaji mengi ya madaktari wengine wa fani yengine. Kwa hivyo ili wizara iweze kupata madaktari wa fani zote kuna utaratibu maalum umewekwa wa kuanzia, na kwa kuanzia kwa upande huu tumeshapata madaktari wawili, lakini ili huduma ziweze kupatikana tunahitaji kuandaa na kitengo.

Kwa hivyo tusingeweza kuandaa Kitengo kama hakuna madaktari, madaktari wameshapatikana sasa wao watakaotoa mahitaji ya kitengo yakoje, lakini tusifikirie kwamba mahitaji ya Kitengo ni rahisi mno na kama ni matibabu tu, yanafikia bilioni nane hapa lakini hivyo vifaa vyenyewe ni matrilioni sio bilioni. Kwa hiyo hivyo vitu vitakwenda hatua kwa hatua, kinachoendelea kufanyika hapa kuwasaidia wagonjwa wale walikuwapo hapa Zanzibar angalau kwanza watambuliwe hapa, halafu wanapelekwa Bara na Wapemba watakao takiwa kutambuliwa Madaktari nafikiri watatayarisha mpango maalum wa kilinki za Pemba zifanyike, na kuwafanya wagonjwa wale pia waende Dar es Salaam kwa ajili ya matibabu. Lakini hata hivyo, madaktari hao hao kadiri muda utakavyoendelea na kadri mahitaji yatakavyohitajika ndivyo itakavyofanya.

Kitengo hichi kinafanywa katika Hospitali za Rufaa, Pemba hakuna Hospitali ya Rufaa kwa hivyo wagonjwa wa Pemba wakishatambuliwa Pemba wataletwa Unguja kwa ajili ya matibabu, kama vile ambavyo Bara hospitali za Rufaa tu ndio zinazotoa ni Muhimbili, Mbeya na KMC. *(Makofi)*

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipatia nami fursa ya kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mhe. Spika kwa kuwa tunafahamu kwamba ugonjwa huu wa Saratani kwa hapa petu sana wanaoathirika na ugonjwa ni kinamama, na tunaona kwamba kinamama hawa wanakuwa wanapata tabu sana kwa sababu hii huduma ya mionzi bado hapa petu haijafanikiwa kufanya kazi. Lakini pia kuna hawa hawa kina mama ambao hawako kwenye hii huduma ya mionzi wanahitaji huduma nyengine tu za dawa na mengineyo. Je, bado lakini wanakwenda kupata matibabu katika hospitali ya Muhimbili je, wizara inatoa huduma gani katika hii Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa hawa wagonjwa wa saratani ili wananchi wajue ni huduma zipi ambazo zinatolewa na waondokane na huu usumbufu wa kwenda Hospitali ya Muhimbili kufuata huduma hii.

Mhe. Sira Ubwa Mamboya: Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum. Mhe. Spika, maradhi ya Saratani hayasumbui tu wanawake, yanasumbua wanawake na wanaume na ukitizama wanaume basi ni wengi kuliko wanawake, katika takwimu tulizonazo. Lakini haimaanishi kwamba wanawake sio wengi ambao nao wanahitaji huduma hizi. Kitengo kimeanza mipango inapangwa huduma zinazoweza kutolewa kwa kuanzia hapa itakuwa ni huduma za vidonge au huduma za kunyunyizia kwa *infusion* za *drip* hizo ndio huduma zitakazoweza kuanzia hapa. Baada ya hapo na siyo zote kwa sababu kuna dawa nyengine zinahitaji uangalizi wa daktari ambaye anayekuwepo katika wodi na sisi wodi hapa sisi hatuna. Wale itabidi kwa vyovyote vile waende Dar-es-Salaam. Baada ya hapo vyenginevyote vinavyofuata kwa ajili ya huduma hii mwaka kwa mwaka kidogo kidogo vitapanda mpaka vitakavyokamilika kwa sababu pesa zinazohitajika sio kidogo.

Nam. 65

Ujenzi wa Bandari Ndogo Huko Makangale, Pemba

Mhe. Omar Seif Abeid - Aliuliza:

Mhe. Spika, kwa kuwa eneo la Makangale ni eneo la Uwekezaji ambalo lipo karibu sana na Tanga kwa Tanzania Bara na Mombasa kwa nchi ya Kenya kiasi ya kilomita 22 tu baharini.

(a) Je, serikali baada ya kujenga kituo kidogo cha polisi, ina mpango gani wa kujenga Bandari ndogo katika eneo hilo au eneo lililokaribu na Makangale kwa ajili ya kutoa huduma kwa wageni ambao wanaweza kuingia na kutoka nchi jirani.

(b) Je, serikali ina mpango gani wa kujenga Uwanja mdogo wa ndege japo wa kutua helikopta kwa ajili ya kurahisisha usafiri wa wageni.

(c) Ni lini serikali itaweka Ofisi za Uhamiaji, ZRB pamoja na TRA katika eneo hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji – Alijibu:

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 65 lenye kifungu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza nitajibu swali (a) na (b) kwa sababu lina muingiliano kidogo.

a) Mhe. Spika, kwanza naomba kumjuilisha Mhe. Mwakilishi kwamba kwa sasa serikali haina mpango wa kujenga Bandari katika eneo la Makangale, badala yake serikali inaendelea na mipango ya kuziimarisha baadhi ya Bandari bubu zilizopendekezwa kwa Unguja na Pemba. Kati ya Bandari zilizopendekezwa ni bandari ya Shumba Mjini ambayo ipo katika Wilaya ya Micheweni, kama ilivyo kule kwake. Kwa hivyo Wizara yangu inatarajia kuwa Bandari hiyo itakaporasimishwa itatumika kwa maeneo yote ya Wilaya ya Micheweni baada ya kujengwa miundombinu ya msingi ya kibandari zikiwemo Afisi ya Uhamiaji, ZRB, TRA, na kadhalika.

b) Mhe. Spika, muongozo wa taarifa za Anga Tanzania *(Aeronautical Information Publication)* kifungu namba GEN.1.2.4 kinaeleza kwamba huduma ya kutua na kuruka kwa vyombo vya angani yaani ndege au helikopta kwa Zanzibar zitatolewa katika sura tatu kama ifuatavyo:"

i. Ruhusa ya kuruka na kutua katika viwanja viwili pekee yaani kiwanja cha ndege cha Abeid Amani Karume (AAKIA) na kiwanja cha ndege cha Pemba, *(Pemba Airport).* Ruhusa hii inaamaanisha kuwa maeneo

yanayoruhusiwa kuruka na kutua kwa vyombo vya anga ni viwili tu vya ndege kwa vyombo vya aina zote ikiwemo ndege na helkopta binafsi.

ii. Ruhusa ya kuruka na kutua kwa sehemu yoyote ya Zanzibar zaidi ya hizo ni za vyombo vya ulinzi na usalama tu vinavyomilikiwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Serikali ya Muungano.

iii. Ruhusa ya kuruka na kutua sehemu yoyote kwa ajili ya kutoa huduma za dharura pamoja na shughuli za uwokozi zitasimamiwa na serikali. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza na mimi sitaki nisimame na kanuni kwa sababu swali langu mimi lilihusu eneo la Makangale.

Mhe. Spika, nashukuru kwamba amejibu kwamba haina mpango wa kujenga bandari lakini itaimarisha bandari bubu. Mimi swali langu lilihusiana na eneo la Makangale ambalo ni eneo lenye wawekezaji. Pemba inajulikana kwamba Makangale ndiyo eneo lenye wawekezaji. Kwa sababu pale karibu na Makangale ipo bandari bubu ya Mkia wa ng'ombe ambayo ipo karibu na Tanga na Mombasa na eneo lenyewe la Makangale ambalo ndilo eneo lengwa.

Je, serikali ina mpango gani wa kuiweka hiyo bandari kuihuisha hiyo bandari bubu au kuisimamia hiyo bandari bubu ya Mkia wa ng'ombe ili ikaweza kupatikana mapato ya serikali ambapo pale wale ni rahisi kuingia na hata leo ukienda pale utakuta bidhaa ni rahisi kuliko Chake Chake na Wete kwa sababu ya ukaribu wao pale watu wa Mkia wa ng'ombe. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa idhini yako napenda kumjibu Mheshimiwa swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Kama nilivyosema mwanzo bandari bubu hazitambuliki na sisi tunazipiga vita kwa nguvu zetu zote ndio maana tukasema tulikaa na wakuu wa Mikoa na wao ndio waliyoleta mapendekezo kutokana na hali halisi ya mambo wakasema bandari ambayo tuirasimishe kwa Kaskazini Pemba ni Bandari ile ya Shumba.

Mimi namuomba sana Mhe. Mwakilishi kwa kushirikiana na Wawakilishi wengine hizi bandari bubu zipo nyingi Zanzibar zaidi ya 350, kwa hivyo tujipange kwa pamoja kupiga vita na kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama kutoa taarifa pale ambapo watu wanazitumia hizi bandari bubu kwani

zinatukosesha mapato yetu na hivyo kuikosesha nchi kuendelea zaidi kutokana na yale mapato tungeyapata wangetumia bandari hizi zilizokuwa rasmi. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nimuulize Mhe. Waziri swali la nyongeza kama ifuatavyo:

Eneo la Makangale limepakana na msitu wa Uhifadhi wa Ngezi na kuna hilo suala la uwekezaji, kuna habari za uhakika kwamba ule msitu sasa kwa sababu nime-*inclose* na eneo la uwekezaji sasa unakatwa viwanja kwa *element* ya uwekezaji. Je, yeye kama ni Waziri wa dhamana ya ujenzi atalifuatilia vipi na kulisimamia suala hili kwamba lile suala la uhifadhi wa msitu wa Ngezi haliwi *eroded*. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuchukua nafasi hii kumjibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwakilishi kama ifuatavyo:

Sisi kama wizara na kama serikali tutaendelea kuhakikisha kwamba:

1) Tunahifadhi mazingira
2) Tunailinda ile misitu yote ya asili na
3) Tutahakikisha kwamba iwapo tutaruhusika kuweka miundombinu basi tutaweka lakini iwapo mazingira yatatukataza hatutoweza kufanya hivyo.

Mimi namuhakikishia kabisa kwamba serikali ina nia ya dhati ya kutaka kuhakikisha kwamba hifadhi zile za mazingira na misitu yetu inaendelea kuzitunza na kuziendeleza.

Mhe. Spika: Swali linalofuata ni la wizara hiyo hiyo linaulizwa na Mhe. Suleiman Sarahani Said Mwakilishi wa wananchi jimbo la Chake Chake.

Nam.156

Ukarabati wa Jengo la Uwanja wa Ndege unguja

Mhe. Suleiman Sarahan Said – Aliuliza:

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imejitahidi katika kuitangaza Zanzibar Kiutalii na kwa kiasi kikubwa imefanikiwa. Katika sehemu moja inayogusa Utalii ni Uwanja wa Ndege kwa kuja na kusafiri kwa wageni wetu,

lakini serikali imejipanga kujenga Uwanja wa Ndege mpya isipokuwa kwa hali inayojionesha Uwanja huo mpya bado kutumika nikimaanisha bado Uwanja wetu mkongwe unahitajika kwa hivi sasa ili kukidhi haja ya wageni.

(a) Je, serikali ina mpango gani wa haraka kulifanyia matengenezo jengo la Uwanja wa Ndege huo.

(b) Je, serikali haioni kuwa kuna haja ya haraka kuufanyia matengenezo Uwanja huo hasa eneo la kusafiria na kuondokea abiria.

(c) Je, serikali haioni kuwa kulifumbia macho suala hili ni kupoteza wageni na mapato yetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 156 lenye kifungu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, serikali kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, tayari imeshaanza kulifanyia matengenezo jengo la abiria kwa lengo la kuimarisha huduma zake. Kazi zilizonza kufanyika ni pamoja na utanuzi wa kumbi za abiria wa ndani *(Domestic)* na abiria wa kimtaifa *(International),* ujenzi wa kipaa kuelekea kumbi ya abiria wa ndani, ujenzi wa sehemu za kupokea na kusubiria abiria pamoja na ujenzi wa ofisi mbali mbali za kibiashara na kiofisi tayari zimeendelezwa. Aidha, kazi ya uimarishaji wa miundombinu ya uwanja huo, Mamlaka inaendelea kuhakikisha kwamba inaimarisha huduma na vifaa katika uwanja huo wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Spika, na mimi nashukuru kwa majibu yake mazuri, mimi nataka nimuulize Mhe. Waziri swali la nyongeza kama hivi ifuatavyo:

a) Kwa sababu uwanja wetu ule ambao tuliutegemea kwamba uwe tayari ni kwamba bado haujakuwa tayari na pengine utachukua muda mrefu. Matengenezo haya anayoyatengeneza anachukua kiwango kile kile cha kimataifa au kwa ajili ya kufanyia matengenezo madogo.

b) Matengenezo ambayo anayafanya ni ya kutanua majengo pamoja na kuweka vifaa vya kisasa au matengenezo ya kufanyia *repair* tu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumjibu Mheshimiwa swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Katika ujenzi ule tunaangalia viwango vya kimataifa kwa sababu sote tunajua kwamba uwanja wetu ule ni uwanja wa kimataifa na hivi sasa upo katika class, kwa hivyo unapofanya kazi zile ni lazima kutakuwa na waangalizi baadaye wanakuja na wakaguzi kuangalia namna gani ile kazi ilofanyika.

Napenda kumuarifu kwamba kazi tulizozifanya kule ni za vifaa, huduma pamoja na majengo ambayo mpaka hivi sasa imetuharimu zaidi ya bilioni moja katika majengo pamoja na vifaa vile vilivyokuwepo katika uwanja wa ndege wa kimataifa wa Abeid Amani Karume. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Zulfa Mmaka Omar: Ahsate Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Waziri tunaona kwamba jengo la *Airport* ya Pemba limeshakuwa bovu na chakavu, na tunashuhudia kwamba mara kwa mara jengo lile linakatwa baadhi ya kuta na kuwekwa sawa ili abiria waweze kupata nafasi ya kukaa katika maeneo yale. Pia hivi juzi mimi na wewe nilikwenda kukuonyesha jengo lile la *Airport* ya Pemba ambalo lina sehemu moja ya VIP ambayo wanatumia Waheshimiwa kwa ajili ya kukaa pale na kusubiri usafiri ulishuhudia kwamba sehemu ile iliroa na wewe mwenyewe ulikaa pale pale kwa kuona tabu kuondoka kutuacha sisi wenzako tunaroa.

Swali langu lina (a) na (b)

a) Ni lini Wizara yako itafikiria kulijengo jengo lile.
b) Je, kulikata makuta jengo lile huoni kwamba unahatarisha hali ya binaadamu ambao inaweza kuja kusababisha vifo vya binaadamu katika eneo lile.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Spika kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mheshimiwa swali lake lenye (a) na (b) kama ifuatavyo:

a) Kwanza nakiri ni wazi tulikuwa pamoja siku ambayo alisema pamoja na Wawakilishi wengine kuangalia hali halisi ya uwanja wetu wa Ndege hasa ile sehemu ya VIP ya juu kule kipaa imejengwa na Kampuni ya SKAZ kwa gharama za milioni 37. Lakini licha ya hivyo bado tupo ndani ya mkataba wa

mwaka mmoja tumewaelezea yale mapungufu yaliyokuwepo na wao wamesema wapo tayari kuyarejea yale mapungufu ili kuonekana kwamba ile hali inarudi katika hali ya kawaida. Sote tunajua kwamba safari hii mvua zilikuwa ni kubwa na imetusaidia kuona yale mapungufu ambayo yametokezea. Bado tupo ndani ya makataba wetu.

b) Mhe. Spika, sisi kama Wizara tutahakikisha kwamba tunalinda kama ilivyo viwanja vyetu vya ndege, usalama wa abiria na mali katika viwanja vyetu vyote vya Ndege na tutatumia utaratibu maalum kuhakikisha kwamba yale majengo tunayoyafanyia ukarabati yanakwenda kwa mujibu wa viwango vinavyotakiwa. Ahsante.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Maswali yamekwisha na hatuna matangazo ya wageni. Katibu kwa shughuli inayofuata.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Maliasili Mifugo na Uvuvu, kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

(Majadiliano Yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe leo tutakuwa tunahitimisha hoja hii ya Wizara ya Kilimo, maombi bado tunayo kutoka kwa upande wa Mawaziri lakini pia kutoka kwa baadhi yetu ambao tumeomba kuchangia hii hoja. Lakini tukumbuke kwanza ni mwezi wa Ramadhani kwa hivyo tunaendelea moja kwa moja mpaka saa 9:00 kama tutatoa fursa kwa watu wote hawa kuchangia tutakosa kumpa nafasi Mhe. Waziri wa Biashara kuanza kuwasilisha hoja yake.

Napenda nikujulisheni kwa upande wa Mawaziri ambao mmeomba nitampa Waziri mmoja tu ili aweze kuchangia na atakuwa anamsaidia Waziri mwenziwe katika majibu ya hizo hoja za Waheshimiwa Wajumbe ambao walichangia. Baada ya hapo nitamwita mtoa hoja moja kwa moja ili aweze kuhitimisha hii hoja yake. Baada ya maelezo mafupi hayo naomba sasa nimwite Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais ili sasa awasilishe hoja. Karibu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na pia naomba nimpongeze Waziri wa Kilimo kwa kuwasilisha hoja yake hii ambayo ameieleza hotuba yake kwa ufasaha

mkubwa. Kabla ya kuendelea na mazungumzo yangu naomba niunge mkono hoja hii kwa asilimia 100.

Mhe. Spika, baadhi ya Wajumbe walipokuwa wakichangia hoja hii wapo waliochangia kwa sauti ya juu kidogo kwa kutaka maelezo ya kina, walikuwa wanafanya wajibu wao kwa mujibu wa taratibu zetu za Kibaraza. Naamini walifanya hivyo kwa kutaka kuelewa zaidi ili kujua nini hasa dhamira ya serikali ya kusimamia zaidi suala la mchanga kutokana na umuhimu wa rasilimali hii kutokana na umuhimu wa sekta nzima ya mchanga katika suala zima la sekta ya ujenzi. Walisema kwa ukali kidogo, lakini naamini baada ya maelezo ya serikali na maelezo ya mtoa hoja nina hakika kwa kiasi kikubwa tutaelewa nini dhamira ya serikali ya kufikia uamuzi huu wa kusimamia suala la uchimbaji mchanga kwa ukaribu zaidi.

Mhe. Spika, wako Wajumbe waliosema uamuzi huu wa serikali ni wa kuwanyima au kuwanyang'anya wananchi mashamba yao. Wapo waliosema kwamba serikali imejiingiza katika biashara ya mchanga.

Nataka niwahakikishie Waheshimiwa wa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwamba serikali haina dhamira ya kuwanyang'anya wananchi mashamba yao na vile vile serikali haina dhamira ya kujiingiza katika biashara ya mchanga. Bali serikali imechukua hatua hizo kwa makusudi kwa nia ya kusimamia maliasili hii muhimu yenye uhai wa taifa letu kwa ukaribu zaidi kutokana na athari zilizojitokeza hususan za kimazingira, kijamii na kiuchumi, ilibidi ifanye maamuzi magumu kwa ajili ya kuhakikisha usalama wa wananchi wetu.

Mhe. Spika, serikali kwa kufanya hivyo ina wajibu wa Kikatiba na Kisheria. Kwanza nataka niseme wazi kwamba suala hili la uamuzi wa serikali sio uamuzi wa Wizara ya Kilimo ni uwamuzi wa serikali kutokana na hali halisi ilivyojitokeza ya athari baada ya sekta binafsi kuchimba mchanga na iliposhindwa kusimamia vizuri matokeo baada ya uchimbaji.

Waheshimiwa Wajumbe kuna athari nyingi zimejitokeza baada ya sekta binafsi kuchimba mchanga ikiwemo athari za kimazingira, ikiwemo kuwacha mashimo makubwa ambayo yamekuwa yakituwama maji na katika maeneo mengi yaliyosababisha kupanda kwa maji chumvi. Kwa msingi huo husababisha maji chumvi kuingia katika maeneo ya kilimo na kusababisha baadhi ya maeneo ya kilimo kutokutumika kwa shughuli za kilimo ambapo wananchi wetu wengi wanategemea. Hata ukiangalia *survey* iliyofanywa imeonekana wazi kwamba Wilaya ya Kaskazini (B) umasikini umeongezeka katika nchi yetu ukilinganisha na Wilaya nyengine kutokana wananchi kutokosa fursa zile za

asili za shughuli zao za kilimo kutokana na maeneo hayo kuchimbwa mchanga na matokeo yake kuachiwa yasichukuliwe hatua vinazofaa za kimazingira ili kurudisha hali katika ukawaida wake.

Mhe. Spika, matokeo ya athari hizo za kupanda kwa maji chumbi, mmong'onyoko wa ardhi, kupungukiwa kwa nafasi ya kilimo katika maeneo hayo pamoja na upungufu mkubwa uliojitokeza wa mchanga kutokana kutokusimamiwa vizuri na kama serikali ingewaachia hali hiyo ikiendelea tungekuwa tunalo tatizo kubwa zaidi la ukosefu wa mchanga wenyewe katika shughuli za ujenzi. Kwa hivyo inapotokeza hali kama hiyo ambayo imeleta athari kubwa ya kimazingira na athari kubwa katika shughuli za kilimo Serikali inawajibu wa kuingilia kati na kufanya mambo ambayo yatawaondolea usumbufu wananchi wake.

Waheshimiwa Wajumbe, chukulia mfano wa eneo moja tu ambalo lilichimbwa mchanga maarufu katika eneo la Mwanakwerekwe tunaona athari yake maji yale yakijaa pale sio tu yanasababisha uharibifu wa miundombinu ya barabara katika eneo la Mwanakwerekwe bali pia maji yale yanasabisha magonjwa ya mripuko yakiwemo kipindupindu, magonjwa ya malaria na kwa kiasi kikubwa sana yameshasababisha kupoteza kwa maisha ya watu.

Kwa hivyo kwa umuhimu wa kipekee linapotumika suala la uchimbaji wa mchanga kuchukuliwa hatua madhubuti ya kurudisha hali katika ukawaida wake na ndio maana Serikali inatoza tozo fulani kwa ajili ya kusaidia kuirudisha hali ya mazingira katika ukawaida wake si kwa sababu ya kufanya biashara ni gharama kubwa sana katika kurudisha hali katika ukawaida wake ambapo sekta binafsi wakati wakifanya hivyo hawachukuwa hatua madhubuti za uhifadhi wa mazingira. Hivi sasa nikiwapa mfano mdogo tu wa hatua ya Serikali katika kuhakikisha kurudisha hali vizuri katika bwawa lile la Mwanakwerekwe zinahitajika fedha nyingi sana kuyaondoa maji pale kuyapeleka ima Ziwa maboga ama kuyapeleka katika bahari kwa kupitia bwawa la sebleni kuelekea saateni na kupeleka baharini.

Ni fedha nyingi sana mamilioni ya fedha katika kuchukuwa hatua hizo kama mnavyojua ile awamu ya kwanza ya mradi wa *ZUSP*, ule mradi wa michirizi umegharimu zaidi ya dola milioni 10.5 hii maana nini? Hii maana yake kurudisha hali katika ukawaida wake si wa gharama ndogo ni wa gharama kubwa sana. Kwa hiyo tunapotona tozo zile si kwa msingi wa kufanya bishara tunapotoza toza zile ni kwa msingi wa kuhakikisha kwamba tutalinda mazingira yale kuruduisha hali katika kawaida wake na kuchukuliwa hatua zote

muhimu zitakazoweza kuzuwiya athari kubwa kwa wananchi wanaoishi katika maeneo hayo.

Kwa hiyo Serikali ilikuwa inafanya vile kwa kuelewa athari ya upungufu mkubwa wa mchanga uliojitokeza na athari ambayo tungeweza kuukosa kabisa na kuhatarisha pia usalama wa watu wetu na Serikali imepewa jukumu hili kikatiba na kisheria ndio maana ikafanya maamuzi ya makusudi kabisa kuchukulia hatua za kusimamia kwa ukaribu zaidi suala la uchimbaji wa mchanga.

Mhe. Spika na Waheshimiwa Wajumbe katiba yetu ya Zanzibar kifungu cha 23(1) kinasema hivi na ninaomba ninukuu.

> "Kila mtu ana wajibu wa kufuata na kutii katiba hii na sheria za Zanzibar na kuchukua hatua za kisheria kama zilivyowekwa na kuhakikisha hifadhi ya katiba na sheria ya nchi".

Katika kifungu hicho hicho cha 23(3) naomba tena ninukuu Mhe. Spika kinachosema:

> "Watu wote watatakiwa na sheria kulinda vizuri mali ya Zanzibar na kwa pamoja kupiga vita aina zote za ubadhirifu, uharibifu na kuendesha uchumi wa Zanzibar kwa makini kama watu ambao ndio waamuzi wa hali ya baadaye ya Taifa lao".

Tunachokifanya hapa Mheshimiwa ni kulinda rasilimali hii ili itufae sisi na vizazi vinavyokuja. Kwa hiyo uamuzi huu uliofanywa na Serikali umefanywa kwa makusudi kulinda usalama wa wananchi wetu na nchi yetu.

Vile vile Mhe. Spika na Waheshimiwa Wajumbe sheria ya umiliki wa ardhi sheria namba 12 ya 1992 kifungu cha 8(2)(g) kinaelezea wazi kwamba Serikali itahakikisha inamilikisha ardhi kwa wananchi au kwa umma kwa ajili ya matumizi yao lakini imeweka ukomo isipokuwa katika maeneo ya fukwe, maeneo ya maji na maeneo ya madini. Maeneo ya madini ni pamoja na mchanga, mawe, mafuta, gesi na madini mengine, kwa hivyo katika maeneo hayo Serikali ina kila wajibu kusimamia vizuri na kulinda hali hiyo ili iwe kwa matumizi ya umma na matumizi endelevu, ndiyo maana Serikali ikafanya uamuzi wa makusudi katika kuhakikisha inalinda hali hiyo.

Mhe. Spika, yapo maneno mengi yaliyozungumzwa na Waheshimiwa Wajumbe kwamba kwa nini Serikali ikachukua uamuzi huo. Serikali Mhe.

Spika imechukua uamuzi huo kama tulivyosema kuhakikisha inalinda usalama wa watu wake, inalinda mazingira na inaweka utaratibu mzuri wa matumizi ya mchanga ili itufaye sisi na vizazi vinavyokuja.

Mhe. Spika, tatizo hapa kubwa lililojitokeza ni kutokana na baadhi ya watu waliokuwa wakifanya biashara hii ya mchanga kuwa na mapato makubwa sana na matokeo yake kadiri hatua zinavyochukuliwa na kuweka hali vizuri ndio hawa ambao wanasabisha kuchochea sana kwa wananchi ili kuonekane yapo malumbano kati ya wananchi na Serikali yao na wamefanya hivyo kupotesha kwa makusudi pia kugombanisha viongozi na Serikali yao na kugombanisha wananchi na Serikali yao.

Mhe. Spika, mapato waliokuwa wakipata kutokana na uchimbaji wa mchanga na ambayo mapato hayo yalikuwa hayawapati wale wenyewe walipewa heka hizo na Serikali, wale wenyewe walikuwa wanapewa fedha kidogo kwa kutokujua kwa mfano mtu mwenye shamba yake eka tatu alikuwa analipwa milioni 10,000,000 mpaka 20,000,000.

Mhe. Spika, katika eneo la eka tatu maana yake ni zaidi ya hekta moja na hekta moja mchanga unaochimbwa pale unatoa zaidi ya tani elfu 35,000 na kwa wakati huo wafanyabishara hawa walikuwa wanauza tani moja Shs. 7000 maana yake katika hekta moja ni milioni zaidi ya 230,000,000 na huyu mwenye shamba yake hapa aliyekuwa amemilikishwa kama ni eka au kwa utaratibu mwengine wowote aliyokuwa akimiliki hapa, amelipwa na hawa watu haizidi milioni 20,000,000 wakati yeye katika kieneo cha hekta moja anapata mapato ya zaidi milioni 230,000,000 na katika hekta moja kwa kawaida kwa muda wa siku nne tayari imekuwa imemalizika, maana yake nini maana yake kwa siku wafanya biashara hawa walikuwa wanatengeneza zaidi ya milioni 50,000,000 kwa siku moja kwamba kwa siku kumi ni milioni 500,000,000 kwa mwezi zaidi ya bilioni 1,000,000,0000 karibu milioni 1.5.

Kwa hiyo yanapokosekana mapato hayo ndio kunakuwa na upotoshaji mkubwa na kugombanisha wananchi na Serikali yao lakini wananchi wahusika walioko katika maeneo hayo wametulia na hawana tatizo lolote, wanachotaka ni kuhakikishiwa namna gani utaratibu huu utaendelea kuhifadhi maeneo yao, namna gani, wataendelea kufanya shughuli zao za kilimo na namna gani wanapata fidia yao kutokana na vipando vyao na Serikali iliunda kamati maalum ya Baraza la Mapinduzi kwenda kukutana na wananchi kusikiliza maoni yao na kusikiliza mahitaji yao na wananchi wakatoa malalamiko yao na pale ambapo pana uhitaji wa mazunguzo zaidi Serikali milango yake iko wazi.

Lakini maeneo yote ambayo yametumika kwa ajili ya shughuli za mchanga Serikali kwanza hufanya tathmini ya vipando na miti iliyopo hapo na baada ya kufanya tathmini hiyo huandikiwa wahusika na thamani ya vipando hivyo na wale ambao walikuwa tayari kupokea fedha hizo Serikali haikuwa na tatizo lolote kuwalipa wananchi vipando vyao katika maeneo hayo, na bado Serikali milango yake iko wazi kusikiliza maoni yoyote ya wananchi pale wanapoona kuna haja ya mazungumzo na Serikali na Viongozi mbali mbali watembelea katika maeneo hayo akiwemo Makamu wa Pili wa Rais, timu ya mawaziri kwenda kujua undani wa jambo hili.

Kwa ufupi Mhe. Spika na Waheshimiwa Wajumbe tatizo si wananchi katika maeneo yale tatizo ni watu ambao walikuwa wanafanya biashara hii ya mchanga na wakipata mapato makubwa bila hata kulipa kodi za Serikali, hawakulipa kodi za Serikali kwa maana Serikali kuu kwa maana ZRB, TRA na hata kwenye Halmshauri hayakufanyika vizuri malipo haya ndio maana hivi sasa Serikali inasimamia zoezi zima hili kuweka utaratibu mzuri kwa ajili ya matumizi bora ya mchanga ili tuweze kuutumia sisi tuliopo leo na vizazi vinavyokuja, tukiendelea kutumia kinyume na utaratibu huu matokeo yake ni kwamba hata hii rasilimali muhimu kwa wananchi wetu itamalizika katika muda mfupi na matokeo yale itabidi sasa Zanzibar iagize mchanga kutoka nje.

Kwa vyovyote vile Serikali inaangalia namna gani ya matumizi mengine ya mchanga itakayopunguza kutumia matumizi yote mchanga kama inavyotumika sasa, ili tusiweze kutumia mchanga mwingi katika shughuli zetu za ujenzi tuweze kutumia mchanga kwa kiasi ili mchanga hii uwepo kwa muda mrefu zaidi na kila namna ambayo itawezekana kutafuta utaratibu wa matumzi bora ya mchanga tutafanya hivyo ili kunusuru rasilimali yetu hii muhimu. Tatizo letu la msingi kuna upungufu mkubwa wa mchanga kwa ajili ya shughuli za ujenzi na tukiendelea hivi ambavyo tunavyo tunaendelea bila ya kuchukuliwa hatua madhubuti itakuwepo tatizo kubwa la maeneo ya kilimo, litakuwepo tatizo kubwa la kimazingira na maji chumvi kupanda juu na matokeo yake kuhatarisha usalama wa wananchi wetu. Kwa hivyo ni wajibu wa Serikali kuchukua kila hatua kuhakikisha nchi yetu inakuwa katika salama na Serikali inafanya hivyo kwa umakini mkubwa wa kuheshimu sheria za nchi na kuheshimu katiba ya nchi.

Kwa hivyo niwaombe sana Waheshimiwa Wajumbe tusikubali kupotoshwa kwa maneno ambayo yasio sahihi wakati mwengine kwa wananchi ambao wanapenda kujenga hoja kwa ajili ya kuendelea kuhodhi biashara hii ili waweze kupata mapato makubwa yanayotokana na rasilimali hii ya umma ambayo ni kwa ajili ya watu wote na msimamizi mkuu wa rasilimali hiyo ni

Serikali. Kwa hivyo kufanya hivi Serikali imefanya wajibu wake naamini waheshimiwa viongozi wenzangu mtashirikiana kulinda rasilimali yetu hii lakini kulinda sheria zetu ambazo tumezipitisha hapa Barazani na kulinda heshima ya katiba yetu kama ambavyo imejieleza pale ambapo linapotokea jambo ambalo linaharibu maslahi ya nchi na watu wake naamini sana waheshimiwa wajumbe watakubaliana nami kwamba hatua hizi ambazo Serikali zimechukuwa na kwa ajili ya maslahi mapana ya watu wetu, ni kwa ajili ya maslahi mapana kulinda mazingira yetu na ni kwa ajili ya maslahi mapana kuhakikisha usalama wa wananchi wetu.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu naamini sasa tutashirikiana kwa pamoja ili kuendeleza uhifadhi wa mazingira ambao dunia nzima wanafanya shughuli hiyo ya kulinda mazingira yao. Naamini na sisi kwa pamoja tutashirikiana tulinde mazingira yetu vizuri pale ambapo pana kasoro ya aina yoyote Serikali siku zote itakuwa tayari kukaa chini na Waheshimiwa Wajumbe tuzungumze tuondoe kasoro hiyo na wananchi wetu ili wananchi wetu wandelee kuishi kwa furaha na wawe na maisha bora na mazuri.

Baada ya maelezo hayo narudia tena kusema naunga mkono hoja hii kwa asilima mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na umetumia dakika ishirini juu ya alama sasa naomba nimwite mtoa hoja Mhe. Waziri wa Kilimo ili aje kuhitimisha hoja yake. Mhe. Waziri karibu.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika awali ya yote naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehma na utukufu kwa kutujalia leo Jumatatu hii tukiwa kwenye saumu tukakutana tena hapa kufanya kazi ambayo wananchi wametutuma.

Lakini pili niwaombe tena ndugu zetu waislamu sote tujitahidi mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani hii zawadi aliotugawia Mwenyezi Mungu tuitumie vizuri ili tufike kwenye safari salama usalimini.

Tatu Mhe. Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii kujibu baadhi ya hoja ambazo waheshimiwa wawakilishi wamezitoa kwa kupitia bajeti yetu hii ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

Awali ya yote naomba Mhe. Spika niwapongeza wote waliochangia hotuba hii ama kwa kusema au kwa maandishi lakini hata kukutana pembeni hata

kukutana pembeni ambao hawakupata kuchangia kwa maandishi au kusema wakipongeza kwamba tumefanya kazi vizuri kwa muda mfupi na matokeo yanaonekana nataka niwashukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa dhati kabisa naomba niishukuru sana Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa bahati nzuri mimi nina uzoefu mdogo toka nilipokuwa kwenye bunge mwaka 1977 nikiwa kama Mwenyekiti wa kamati ya *PAC* ya ndani ya nchi, Makamo Mwenyekiti wa Kamati za *PAC* za *SADC*, Katibu Mkuu wa Kamati za *East African Public Accounts Committee*, Mwenyekiti wake akiwa waziri wa Kenya sasa hivi Uhuru mimi nilikuwa katibu Mkuu wake na uzoefu kidogo nimeuona.

Moja ambalo nilijifunza kwenye kamati yetu hii ukizungumza nao unaweza ukafikiri hawana jambo kubwa watakwambia na watakwambia waziri tuna mambo kidogo sana wanakwambia ukiondoka wana mambo kumi na tatu wamekuandikia, wanafanya kazi kwa ufanisi na kwa umakini mkubwa sana.

Nasema nimejifunza kwamba ni kamati makini inajua kufanya wajibu wake vizuri na wana wizara nzito wanazozishauri Wizara Fedha, Wizara ya Biashara na Wizara ya Kilimo nataka niwapongeze sana kabisa kabisa na wamefanya kazi kubwa sana ya kuweza kuikosoa, kutuelekeza na hata pale ambapo hakuna vikao vya kamati wajumbe walikuwa wanafika kutuelekeza yale ya kufanya nataka niwashukuru sana Mheshimiwa kamati yako uliyoichagua ni kamati makini sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba niwataje wale ambao wamechangia kwa kusema:

1. Mhe. Hamida Abdalla Issa - Makamo Mwenyekiti wa Kamati kwa niaba ya Kamati ambaye ndiye aliyekuja kusoma hutoba hapa ya kamati namshukuru sana na kamati kwa pamoja wameunga mkono hoja.

2. Mhe. Hidaya Ali Makame
3. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)
4. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf
5. Mhe. Rashid Makame Shamsi
6. Mhe. Machano Othman Said

7. Mhe. Shehe Hamad Mattar
8. Mhe. Omar Seif Abeid
9. Mhe. Makame Said Juma
10. Mhe. Abdalla Maulid Diwani
11. Mhe. Ahmada Yahya Abdul-wakil
12. Mhe. Suleiman Sarahan Said
13. Mhe. Asha Abdalla Mussa
14. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi
15. Mhe. Mussa Foum Mussa
16. Mhe. Masoud Abrahman Masoud
17. Mhe. Said Omar Said

Waliochangia kwa maandishi ni:

1. Maryam Thani Juma
2. Mhe. Mussa Ali Mussa
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar
4. Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo
5. Mhe. Tatu Mohammed Ussi
6. Mhe. Naibu Waziri wa Afya
7. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa
8. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
9. Mhe. Bahati Khamis Kombo
10. Mhe. Hassan Khamis Hafidh
11. Mhe. Miraji Khamis Mussa
12. Mhe. Shaib Said Ali.

Hao ndio niliopata Mhe. Spika, lakini nisipomsahau Mhe. Mohammed Aboud Mohammed sikumtangaza kama amechangia. Pia Mhe. Suleiman Makame Ali nae amechangia kwa maandishi namshukuru sana.

Mhe. Spika, baada ya hayo naomba niseme maneno ya jumla. La kwanza nataka niwashukuru sana wajumbe hakuna mjumbe yeyote aliyenyanyuka akawa hakuiunga mkono hoja. Wako waliounga mia kwa mia, lakini aliyekuwa hakuunga kabisa kabisa anasema asilimia 85 anaunga mkono anangoja asilimia 15 ya maelezo. Sasa ukishapita asilimia 50 maana yake umeunga mkono, ila unataka ufafanuzi wa mambo. Kwangu mimi nasema wameunga mkono na nawashukuru sana.

La pili niseme sifa zote ambazo na pongezi mmetupa kwetu sisi ni changamoto, kwamba tuna kazi kubwa mbele yetu ya kufanya ili kuuridhisha umma wa Wazanzibari waondokane na shida ambazo wanazo.

Mhe. Spika, wizara yetu asilimia 42 ndio imeajiri na asilimia 74 wanaitegemea Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi. Hiyo ni idadi kubwa sana tunahitaji kwa makini kusaidiana kufika tunapofika. Sasa kuna jambo moja la jumla ambalo huwa nalisema sana wananchi na wajumbe wana wasi wasi, kwamba tunaposema katika kipindi cha miaka miwili ijayo tutajitosheleza kwa chakula kuna miujiza gani tutafanya wakati *production* zinaanguka kiasi hivi, wamesema hapa baadhi ya wajumbe.

Mhe. Spika, tunahitaji hekta 4000 za *irrigation* ili angalau tupate tani 40,000 za mchele. Sasa hivi tuna hekta 850 tunazofanya *irrigation*, katika bajeti mnayoipitisha sasa hivi kuna fedha za kumwangilia maji hekta 1,600. Mradi huu tukiutekeleza na naamini utatekelezwa tutakuwa na angalau hekta 2000 za kumwagilia maji, ukichukua na *production* ambayo tunaipata sasa hivi ya tani 29 tukiisimamia vizuri, tunaamini kabisa upungufu wa mchele kwa kiwango kikubwa sana utakuwa umeondokana na suala la kuagizia mapembe litakuwa limepungua kwa kiwango kikubwa sana. Sasa hizi si *wishes* ni mipango iliyopangwa vizuri, yenye kamanda mzuri Rais wetu anayesimamia siku kwa siku kuhakikisha kabisa tunalitekeleza hili kwa vitendo.

Mnakumbuka waheshimiwa tulikuwa na Mradi wa *Exim Bank* kwa bahati mbaya *tender system* haikwenda vizuri, baadae Rais akasema turudie tuangalie *tender* hii itakuwaje? Nataka kukuhakikishieni *tender system* imekuwa vizuri sasa *Exim Bank* wameendelea kutoa pesa na katika bajeti hii kuna 27 bilioni utazikuta zimo ikiwa ni sehemu ya mradi huo wa kutekelezwa. Naamini *irrigation program* hii ikitekelezwa ule wasiwasi wenu kwamba kweli hatuwezi kujitosheleza kwa chakula itaondoka, kwa sababu tatizo la kilimo sasa hivi tuachane na suala la kutegemea mvua lazima tuingie kwenye *irrigation* ndio tunaweza kutatua tatizo la kilimo, kwa kutegemea mvua tutakuwa tunajidanganya. Sasa nilikuwa nataka niliseme hili la jumla la kwanza kabla sijaingia kwenye maeneo.

Mhe. Spika, nataka niwakumbushe wajumbe vile vile Ibara ya 20(c) ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi, mimi ni ADC lakini *Atullahi Waatu Rasulu Wal amri minkum* namtii Mwenyezi Mungu na Mtume wake lakini vile vile na anaeniongoza, na anayeniongoza hapa ni Dkt. Ali Mohamed Shein aliyechaguliwa na Chama cha Mapinduzi. Kwa hivyo, Rais wangu anasimamia ilani ya uchaguzi ya CCM, na mimi nimekamata msahafu kula kiapo kwamba

nitafata Katiba na sheria na akanikabidhi na ilani yenyewe. Nasema hili nataka niwatoe wasiwasi wale wanaofikiria kwamba labda nafanya jambo lina ujanja ujanja ndani yake. Mimi ni muumini wa kweli kweli tena na ndio maana nasimamia nguzo muhimu sana ya *Atullahi Waatu Rasulu Wal amri minkum*. Kwa hivyo, sifanyi hila ya aina yoyote ya kwamba wananchi wa Zanzibar hii wapate shida au dhiki kwa sababu tu natoka kwenye chama chengine. Mimi ni Mzanzibari maslahi ya Taifa naweka mbele kuliko maslahi yoyote mengine. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kamati imekuja na hoja nyingi lakini nyingi ni za mafunzo, maelekezo. Nataka niwahakikishie kabisa kamati tumezichukua hoja zenu zote ziko kama 12 sitaki nizijibu zote moja kwa moja, lakini nakuhakikishieni kabisa tutakwenda kuzifanyia kazi na mtakapokuja kufanya ziara katika kamati mtakuta majibu yapo na kazi tumeshaifanya. Lakini katika haya ya kamati vile vile kuna wajumbe wamesema, kwa mfano Mhe. Rashid Makame Shamsi amezungumzia sana suala la namna gani tutakuwa *focused* katika kilimo, katika ufugaji. Yeye akasema kila kitu angalau tuende kwa eneo ambalo tunataka kuona tunafikia vipi.

Mhe. Spika, katika wizara tunazungumzia hizi kama *base lines*, nichukue mfano Zanzibar inaagizia mafuta tani 35,000 kwa mwaka, hiyo ndio *base line* yetu ya kwanza. Je, tunapoanzisha viwanda vya kusindika mafuta, mashamba tutakayolima halizeti kuzalisha mafuta yako wapi, ni akina nani, na kwa ukubwa gani, na vipi tutayasaidia kuondokana na kuagizia mafuta? Maana serikali iliyo makini unafanya vitu viwili, inaongeza *exports* lakini vile vile inapunguza *import*. Lengo hapa ni kupunguza *imports* ya mafuta ndio maana nasema nakubaliana nae kabisa tuwe *focused* tuangalie je Wilaya fulani ina mkulima gani anaweza kutupa tani ngapi ili tumsaidie aweze kuzalisha tufikie kiwango tunachotaka ili kupunguza *importation* bila ya kuhangaika kwa wakulima wengi.

Mhe. Spika, na kwa sababu hiyo basi ndio Mhe. Rais katika kipindi cha miaka minne tulikuwa tukigawa mbolea ovyo ovyo, akasema hapana tuwe *focused* tuchague mashamba maalum, watu maalum tuwape *input* za kutosha tutizame uzalishaji utakuwa kiasi gani. Ndio mara hii katika programu niliona ya 2016/2017 na hii inayoendelea tuna mashamba maalum tumeyachagua kwa ajili ya *irrigation* tumewapa mbolea kamili ili waweze kuzalisha kwa ufanisi zaidi na kwa kiwango kikubwa kinachohitajika. Kwa hivyo, ushauri wenu mheshimiwa tumeuchukua tumeanza kuufanyia kazi na tutaendelea kuufanyia kazi.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf alizungumzia sana suala la kumpongeza Rais katika suala la kuongeza mshahara. Hili sote tunampongeza Rais kwa kweli ni jambo kubwa sana, kuna watu walikejeli kwamba haiwezekani lakini *Alhamdulillah Rabil alamiin* imewezekana hata wale waliokuwa wakisema haiwezekani imewezekana. Lakini nataka nikwambieni jambo moja ambalo ni kubwa sana, CCM yenyewe hamjui kitu kizuri mlichonacho. Kama kuna Rais ambaye mimi nimekaa na ma-Rais wengi yuko makini sana, *cautious* ni Rais Ali Mohamed Shein. Wajumbe wenzangu wa Baraza ni mashahidi namna gani anatushirikisha katika kufikia maamuzi. Rais kwa mujibu wa Katiba anaweza kuamua bila ya kutushirikisha sisi, hata Baraza la Mapinduzi lenyewe linasema linamshauri Rais.

Kwa hivyo, ana hiari kukubali ushauri au kuukataa, sio Rais Shein. Anamuuliza mjumbe mmoja baada ya mmoja mpaka anamaliza, akimaliza anasema jamani tumekubaliana, tumekubaliana. Huu ni uongozi tofauti kabisa na ndio matokeo yote unayoyaona haya ni umakini wake ndio tukafika nchi hii ikabaki amani na usalama tulionaao leo. Aminini Mungu tulikuwa tunamwambia Mhe. Rais mbona unakuwa mpole mno huchukui hatua anasema aah subirini. Siku moja alikuwa ananambia kwani maiti kwenenda anapigwa? Nakuulizeni waheshimiwa maiti kwenenda anapigwa si anatembea ni maiti tayari si muache tu afe, tuna Rais makini sana. Kwa hivyo, maamuzi yote yaliyochukuliwa na serikali yamechukuliwa kwa ufanisi mkubwa sana na kwa uadilifu mkubwa sana. Nataka niwahakikishie kwanza hilo wale ambao wana *doubt* najua Rais hapana. Ni Rais mwenye mfano wa pekee, msomi, anafanya kazi hachoki mnaweza mkakaa kwenye kikao saa tisa za usiku anaendelea na kazi. Naomba hilo kwanza vile vile wale ambao wana mashaka na *cabinet* yake, wana mashaka na Rais, kwa kweli ni Rais makini na uteuzi wake ni makini lakini anafatilia kazi zote anazozifanya.

Mhe. Spika, limezungumzwa sana suala la matrekta, najaribu kuyajibu kwa jumla kwa sababu kila mjumbe baadae tutampelekea majibu yake. Ni kweli kabisa tuna matrekta machache mahitaji kabisa ya idadi kubwa ya matrekta ni 100 sasa hivi tunayo 50, katika 50 mazima hasa ni 26 mengine tunayafanyia ukarabati. Ndio Rais akasema sasa hebu tuanzishe mamlaka ambayo itakuwa na jukumu la kusimamia uendeshaji wa vifaa wa matrekta na kadhalika. Nataka mkipata waheshimiwa baada ya maamuzi hayo ya Rais mupite kwenye Karakana yetu ya matrekta sasa hivi muangalie mabadiliko yaliyopo, hivi sasa ninavyokwambieni kutokana ni muda mfupi sana wa maagizo yake. Wameweza kuyachukua matrekta yote wakayakusanya, wameweza kupata vipuri vya kutengeneza matrekta ambayo yalikuwa yameshatupwa

mashambani. Hali inaanza kubadilika kutokana na uongozi imara na usahihi wa Rais.

Mhe. Spika, Rais alipofanya ziara pale alituchukua mawaziri sote tukashuhudie hali ilivyo. Sote tukaenda kushuhudia akasema nataka hili na hili lirekebishwe. Imefanyika hiyo kazi kwa ufanisi mkubwa na kwa sababu ya usimamizi wake, nawaomba waheshimiwa mkipata nafasi hapa sio mbali piteni mkaangalie hali ilivyo. Kuna hali nzuri sana nategemea katika msimu ujao na matrekta 20 yale ambayo tutapata kutoka Mahindra hali yetu yakuwa na matrekta itakuwa nzuri sana. Sasa nimepiga kelele sana katika hotuba hii kwamba je wananchi wanasaidiwa vipi?

Mhe. Spika, sijapata kuona nchi hii ni ya ajabu sana, asilimia 75 ya mahitaji ya mkulima hasa wa mpunga yanafidiwa na serikali, wakulima wanachangia asilimia 25. Lakini hata hii 25 mheshimiwa wanachelewa watu kutoa fedha zao matokeo yake ni kwamba wanakosa huduma kwa sababu hakuchangia asilimia 25. Nimekwenda kuonana na wakulima tumezungumza nao tukiwaomba kwamba waharakishe kuchangia asilimia yao 25 ili waweze kupatiwa huduma. Nawashukuru baadhi ya wakulima wameitikia mara hii katika kazi tuliyoifanya nzuri ni asilimia 90 ya kuwalimia wakulima hapa na asilimia 75 Pemba kuwalimia, kwa sababu Pemba kidogo kulikuwa na upungufu wa matrekta. Huo ndio uongozi wa Dkt. Ali Mohamed Shein, Makamu Mwenyekiti wa CCM. (*Makofi*)

Mhe. Spika, jambo jengine jengine ambalo limezungumzwa ni suala la shamba la Razaba. Mhe. Spika, nataka tena nimshukuru Rais awali serikali ilikuwa iagize tutengeze *tender* ili tupate mtu atakayeweza kuliratibu shamba letu la Razaba. Tukapata watu wawili katika *tender* hizo, kwa bahati mbaya tukagundua kwamba mapendekezo yao na maombi yao sio mazuri. Rais akasema hapana, hebu ongozaneni mawaziri watatu mwende Bara mukaangalie kwanza shamba lenyewe, halafu mkutane na viongozi, nakuelezeni umakini wa Rais tu. Tukaenda na Mhe. Mohammed Aboud Mohammed yupo hapa tukakutana na Waziri wa Ardhi akatuhakikishia kwamba ardhi yetu ipo ambayo ilikuwa ni moja katika wasi wasi Wajumbe wa Baraza lako. Lakini pili tukakutana na *National Housing Cooperation* na waziri akatupa na *list* ya mashirika ambayo tunaweza ku-*deal* nayo, tukaenda kwenye *National Housing Cooperation* kwa bahati nzuri wakatuelekeza wakasema hiyo kazi mnayotaka kuifanya sisi tuko tayari kuifanya.

Tukatoka tena tukaenda kwenye shamba pamoja na *National Housing Cooperation* wakatwambia katika eneo peke yake Tanzania nzima ambalo ni zuri kwa maendeleo ya kila aina ni eneo hili hakuna jengine, lina sifa zifuatazo.

Kwanza, ardhi kubwa na nzuri, ardhi ina mto mkubwa na karibu yake kuna bahari, pembeni kwake kuna mbuga ya wanyama, huwezi kukuta mazingira haya pahala popote pengine. Wakasema hii tunaifanya na kwa taarifa yenu tumesha-*sign MOU* tumeshawaachia kazi wanafanya zile gharama za kwanza ambazo tulipata sasa wanazibeba wao wakiona kwamba mradi huu una maana. Huo ndio uongozi wa Dkt. Ali Mohamed Shein. Kwa hivyo, msiwe na wasi wasi Razaba ipo na Mwenyezi Mungu akipenda tutafanikiwa vizuri sana. (*Makofi*)

Mhe. Spika, tumepata vile vile suala la mashamba ya mpira kwamba wangependa wajumbe wapate taarifa juu ya maendeleo ya mashamba ya mpira. Mashamba ya mpira sasa hivi yapo chini ya Wizara ya Fedha kama utaratibu wetu wa rasilimali zetu zinakuwa chini ya Wizara ya Fedha, serikali imeshaagiza tufanye utafiti kuona kwamba je mashamba yaliyopo yanazalisha kwa kiwango gani na hatimae tuamue kwamba je tunaendelea na mashamba ya mpira au tunapanda minazi au tunapanda *vanilla* au chochote kingine. Maamuzi hayo yatapatikana serikali hivi karibuni na kazi hiyo imeshaanza kufanyika na tutapelekea taarifa serikalini na serikali itatoa maamuzi namna gani mashamba haya yaweze kutumika. Ama yabaki kama ya mpira tuendeleze mpira au tuyabadilishe kwa kupanda jambo lolote jengine uamuzi huo utatoka serikalini. Nakuhakikishieni kabisa serikali iko makini inafatilia rasilimali hizi kwa makini sana.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo lilizungumzwa sana na wajumbe wengi ni namna gani tunaweza tukapata mbegu hasa za uhakika. Na hili nasema nilikubaliana nao kabisa na katika hotuba yetu nimesema mwaka huu sisi tumepata tabu sana suala la mbegu tumekwenda mpaka Bara kutafuta. Ndio maana katika programu mtakazozikuta mara hii kuna programu ya kuzalisha mbegu zetu sisi wenyewe. Kizimbani tumewaelekeza sasa hivi watakuwa na hekta 50 kwa ajili ya kupanda mbegu nzuri ya muhogo, Pemba kutakuwa na hekta 10 kwa ajili ya kupanda mbegu nzuri ya muhogo, tutakuwa na hekta 26 kwa ajili ya mbegu ya mpunga Unguja na hekta 15 kwa ajili ya mbegu ya mpunga Pemba. Hapa tutafanya mambo mawili eneo tutakalowashirikisha wananchi na eneo tutakalolisimamia sisi wizara kuhakikisha kwamba mbegu nzuri inapatikana kupitia Chuo chetu cha Utafiti.

Kwa hiyo, tunategemea mwakani suala la kuhangaika na mbegu ya mpunga tena itakuwa limemaliza habari yake, tunangoja tuvune kazi hii tulishaimaliza kama suala lilivyokuja hivi asubuhi tunategemea Julai tutajua uhakika mbegu tumepata kiasi gani ya mpunga lakini mashamba ya muhogo tumeanza kuyaandaa ili tuondokane na tatizo la kupata muhogo. Kwa sababu mazao makubwa hapa yanayotumika zaidi ni mchele, muhogo na kidogo ndizi. Kwa hivyo, hayo mazao matatu tunataka kuyashughulikia kwa ukamilifu ili tuondokane na balaa hili la njaa linalotukabili kila wakati.

Mhe. Spika, suala la kuwapatia elimu wafugaji tunakubali kabisa bado tuna upungufu huo hatujawafikia wafugaji wote, lakini programu iko nzuri mimi naamini kabisa tutaweza kuwafikia watu wote na kupata taaluma inayostahiki.

Limetoka suala la ubora wa maziwa ya ng'ombe. Ni kweli kabisa Mhe. Spika, lipo tatizo la ubora wa maziwa ya ng'ombe kwa sababu zifuatazo: Wafugaji wetu wengi hawamuogopi Mwenyezi Mungu wanakamua maziwa wanaingiza maji, wakishaingiza maji yakishakuwa meng iwanaongeza na unga kidogo ili yawe mazito. Kwa hiyo, Mhe. Said Salum Bakhresa ameshindwa kuyanunua kwa sababu maziwa sio safi. Hilo moja lipo.

La pili, yako maradhi ambayo yanapatikana kama maziwa hayakukamuliwa wakati mwengine kiwele kile, kuna aina fulani ya maradhi huwa yanapatikana pale na hilo linasababisha ubora wa maziwa. Sasa kazi ambayo tunataka kuifanya la kwanza ni kufufua yale mashamba yetu makubwa tuliyonayo na ndio maana Rais katika taasisi moja aliyoifufua sasa hivi ni utafiti wa kilimo na katika bajeti hii mtakuta wamepata pesa ya ruzuku kutoka Hazina kama shilingi 500 milioni kuweza kufanya kazi hiyo ya utafiti. Lakini vile vile tumetafuta watu ambao tunaweza kuingia nao ubia namna gani ya kuendeleza mashamba haya makubwa, tutakuwa na *stock* ya mashamba makubwa ambayo tunayaamini. Vile vile tunamuona Mhe. Said Salum Bakhresa tuzungume naye kama katika mashamba haya makubwa tuwekeze kwa pamoja ili awe na uhakika wa kupatikana kwa maziwa ili maziwa sasa yazalishwe hapa nchini. Mimi nafikirikwa hatua hizi tutakuwa tuna maziwa ya uhakika na kiwanda chetu hiki kitakuwa kimefanya kazi nzuri sana.

Kwa hivyo, nasema hilo ni kweli kabisa tunalo tatizo hilo, lakini nataka nirudi kwa wafugaji vile vile ni vizuri wafugaji wakaheshimu sheria na taratibu ili sasa ng'ombe wetu tunaowapata kuna msaada tunawapa huu kopa ng'ombe lipa ng'ombe; kopa mbuzi lipa mbuzi; basi angalau wafanye kazi vizuri. Mara hii tuliwapa ng'ombe 360 wasifanye udanganyifu ndani yake na washirikiane bado utaalamu tunawapa ili waendelee kupata taaluma hiyo.

Mhe. Spika, maradhi ya mwani tunakubali kwamba tumepata tatizo la maradhi ya mwani na tulipolipata tatizo hili binafsi kabisa nilikutana na Mkurugenzi Mkuu wa *FAO* Mauritius nikamueleza, tukamuandikia na *Alhamdulillah* amesaidia US$ 85,000, wameshakuja wataalamu wanafanya utafiti namna gani ya kupambana na maradhi haya ya mwani. Kwa hivyo, hilo linafanyika na Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar imetoa fedha tunaendelea na kazi hiyo na wataalamu wanaendelea na kazi hiyo hivi sasa. Kwa hivyo, ni kweli maradhi hayo yametokea na yametokea kutokana na tabianchi mengine. Kwa mfano, ule mwani mkubwa ukipata joto kule chini zaidi hauwezi kukubali, kwa hivyo kuna matatizo mengine ni ya nje ya uwezo wa kawaida kwamba ni matokeo ya tabianchi ndio ambapo kuna matatizo kama hayo. Lakini niseme yote mawili tutayakabili tutaona ni kiasi gani tunaweza kuendeleza, lakini shida kubwa ya hii sio haya maradhi peke yake, shida kubwa ni soko la mwani wenyewe.

Mhe. Spika, nataka nimshukuru sana Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko tumekaa pamoja tukaangalia ni namna gani tunaweza kuondokana na rasilimali hii kubwa tunayovuna si chini ya tani 16,000 tupate viwanda ambavyo vitaweza ku-*process* mwani kwa sababu unatoa bidhaa zaidi ya 17. Sasa hivi viko viwanda vidogo vidogo tunafanya lakini tunahitaji kiwanda kikubwa na juzi tulipozungumza na Benki ya Kilimo wamekubali akipatikana mwekezaji kukopesha fedha kwa ajili ya kujenga kiwanda hivyo. Nawaambia kabisa Waheshimiwa wiki ijayo tutakaa mimi na Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko wako wawekezaji yeye mwenyewe ameniandikia ki-*note* tutakaa nao ili tuone kama kweli wanaweza kuwekeza katika biashara hiyo hasa kwa sababu mtaji wa fedha umeshapatikana. Tukipata hili naamini kabisa wakulima watalima kwa wingi mwani na watapata bei nzuri na tabu hii ambayo wanaipata sasa hivi itakuwa imeondoka.

Kuhusu madagaa wizara imepokea ushauri na naahidi kabisa katika kipindi cha mwezi mmoja tutakuwa tumelishughulikia na hasa kuna hizi mashine ambazo ndogo ndogo tumepeleka pale za kukaushia dagaa. Kwa hivyo, tutalisimamia lakini ni ndogo sana hatujaridhika nazo sana lakini angalau mvua kama hizi zinazonyesha wawe na pahala pa kuweza kukaushia dagaa lao. Hilo tumeanza nalo na tutaendelea nalo, naamini kabisa itakuwa tumeweza kuwasaidia watu wetu wavuvi wa dagaa.

Tumeambiwa kuna tatizo la Mwanasheria Pemba nawahakikishia katika kipindi cha wili moja mwanasheria katika kipindi cha mwezi mmoja samahani, atakuwa amefika Pemba kwenye Wizara ya Kilimo na atafanya kazi zake na jana tumemu-*identify* nani tutampeleka huko.

Suala la Bwanashamba na Bibishamba kwa bahati nzuri tuna ugatuzi sasa, wizara itasimamia juu lakini utumiaji hasa utakuwa kwenye ugatuzi kule chini. Kama kutakuwa na upungufu wizara waziri wetu wa Tawala za Mikoa atatueleza namna gani tunaweza kusaidia pale ambapo pana upungufu tuweze kusaidia. Sasa ni jukumu letu sisi wawakilishi kwa sababu ugatuzi uko kwetu kule chini ndio tutaona kabisa watu hawa wanafanya kazi na kwa misingi gani. Mimi nafikiri hilo litatusaidia kuweza kufanya kazi nzuri ya bwanashamba, lakini taaluma tutaendelea kutoa kama walivyotuagiza nawahakikishia kabisa tutalifanya kwa ufanisi mkubwa sana.

Kuna suala zima la kutumia visima vidogo vidogo kwa ajili ya *irrigation*, tunakubaliana kabisa na ushauri tulioupata kwa waheshimiwa. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) alisema sana hili namhakikishia kabisa tutalisimamia ili tuone visima hivi vinapata *pump* na kadhalika. Tuna mpango wa *NETAFIM* wale Wa-Israel tuna mipango nao, tunaamini kabisa tunataka twende kwa wakulima wadogo wadogo tuwasaidie zana za kumwagilia maji kwa kutumia matone ili tuweze kupunguza matumizi makubwa ya maji, lakini vile vile kuhakikisha kabisa wanazalisha vizuri.

Mhe. Spika, limezungumzwa sana suala la kuvuna maji ya mvua. Ni jambo jema sana, ni jambo zuri sana na katika programu zetu tumeona kwamba mara hii angalau tutafanya maeneo mawili, lakini nataka niseme tutakaa na Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira ambayo suala la maji liko kwao, tukae pamoja na utaalamu wanao ni namna gani sasa tutumie utaalamu wetu kwa pamoja kuweza kuvuna maji haya ya mvua. Ni kweli maji ni mengi yanapotea bure na mazingira yetu haya tunaweza tukayahifadhi lakini najua gharama ni kubwa. Lakini vile vile kuna ile *study* tuliyosema katika hotuba yetu ya KOICA kwamba wameshafanya *study* maeneo gani na gani tunaweza tukavuna maji ili tuweze kuyafanyia kazi. Kwa hivyo nasema ushauri tumeuchukua tutaufanyia kazi na nawahakikishieni kabisa waheshimiwa watapata majibu ya haraka sana.

Mchango wa Vikundi vya Wakulima. Mhe. Spika, awali ya yote nataka niishukuru sana nimshukuru Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko amepitia mabenki mengi hapa nchini, lakini vile vile niwashukuru Benki ya Kilimo ambao wamekuja kuonana nasi Wizara ya Kilimo na wizara nyengine pale mpaka *ZSTC* wamekwenda kutaka kufanya mambo yafuatayo.

Benki ya Kilimo iliiandikia mikoa yote 26 kwamba sisi tunazo *funds* tunaweza kuwasaidia wakulima kwa masharti nafuu. Sisi bahati nzuri Zanzibar tukawa watu wa kwanza kuwaandikia kupokea mpango wao, wa pili walikuwa ndugu

zetu wa Mali. Kwa hiyo, wakaja hapa tukavipitia vikundi 68 Unguja na vikundi 56 Pemba tarehe 5 watakwenda kuvipitia. Hapa kuna firsa kweli Waheshimiwa Wawakilishi na fursa hii tunataka tuitangaze hapa mbele yenu hadharani. Benki hii imekubali kutoa mkopo kwa nafuu sana na kwa masharti nafuu kwa kutumia benki zetu hizi wao sio *conventional bank*, wao si kwamba wana ule utaratibu wa kuweka na kukopa aa, kazi yao ni kutoa mitaji. Kwa hiyo, watatoa mitaji hiyo kwa benki yetu ya *Peoples Bank* kama wana *account NBC,* kama wana *account* popote pale, lakini wao watatoa *funds* kwa masharti yao wao wenyewe.

Sasa nawaomba wawakilishi kwa lile alilosema Mhe. Rashid Makame Shamsi tuwe *focused*, nenda katika jimbo lako kaangalie ni mradi gani katika jimbo lako ukifanyika utaweza kuleta manufaa makubwa. Sisi kwa kushirikiana na Wizara ya Biashara tutafanya uchambuzi, tutawakabidhi watu wa benki na wao wameahidi watafungua hata ofisi yao hapa ili kusaidia vikundi hivyo na tarehe 5 kwa taarifa watakuwepo hapa, watakwenda Pemba kwa wiki nzima ili miradi ambayo iko tayari iweze kufanya. Hii ni *opportunity* kwenu 2020 sio mbali waheshimiwa. Hii ni nafasi na fursa pekee itumiwe tumshukuru sana Waziri wa Biashara na Waziri wa Kilimo kwa kushirikiana kwa hili. Lakini nataka nimshukuru sana Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto wanazo *fund* kupitia ushirika pale na sisi watatu huwa tunakaa pamoja wakati wowote kuona ni namna gani tutatumia fursa zilizopo ndani ya wizara zetu lakini nje ya wizara zeti ili kuwawezesha wananchi.

Hii timu ya Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein sio timu ya mchezo hata kidogo, waitumie fursa hiyo wakiwa tayari Naibu Katibu Mkuu wangu wa Kilimo pale Maryam ndiye anayepokea mapendekezo hayo na yeye atayafanyia kazi watu wale wakija ndiye *coordinator* wetu atafanya ihyo kazi vizuri kwa ufanisi mkubwa sana. Kwa hivyo, nasema huo ni utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa uzuri sana kuwasaidia watu.

Mhe. Hidaya Ali Makame aliulizia suala la vikundi alisema Pemba wako vikundi 59 na unguja viko 68 na kuanzia tarehe 5 wataanza kupitia na kama kuna vikundi vingine vitaonekana vinafaa fedha ipo ya kutosha wana *two hundred ninety-eight billion* walizozipata kwa kutokea *ADB.*

Suala la soko la Kinyasini hasa Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf alilizungumza sana. Mhe. Spika, soko hili gharama yake ni shilingi 2.5 bilioni, michoro ya kwanza iliyochorwa na *ADB* na hatimaye wakenda kukaa na viongozi wa Halmashauri tukakubaliana yafuatayo:

Kwanza, soko lile litakuwa la chini lakini kutakuwa na jengo la ghorofa moja, lakini soko limejengwa kwenye *foundation* ya kuweza kulipandisha juu baadae. Kwa hivyo, ni kweli kwenye hiyo ghorofa moja hakuna *lift*, maana jamani kweli ghorofa moja mnataka *lift* kweli? Lakini hilo jengo jengine litakalojengwa baada ya *foundation* hii ishakamilika na soko liko chini mkienda juu lina uwezo wa kwenda ghorofa tano hao ndio patahitajika *lift*. Sasa kwa sababu vile vile katika mchoro wa kwanza kuna aneo mbalo halikuzingatiwa la senyenge na kadhalika tukasema hizi pesa za *lift* basi kwa wakati huu tuzitumie kwa maeneo haya ambayo hayakuingizwa katika michoro ya kwanza. Kwa mfano, senyenge na vitu vyengine *compensation* na kadhalika. Kwa hivyo, hizo ndio takwimu na habari za mradi huu wa Kinyasini. Sasa kuna watu wanaema hakuna *value for money* na kadhalika hii benki iko makini sana nawahakikishia kabisa Halmashauri imeshirikishwa kikamilifu katika *process* nzima ya ujenzi wa soko hili. Kwa hiyo kama kuna mapungufu yatakuwa ni ya pamoja sote kwa sababu tushiriki sote kwa pamoja, lakini naamini kabisa liko vizuri na mimi nawahakikishieni kabisa mambo yatakuwa mazuri hapo baadae tusubiri.

Mhe. Spika, limezungumzwa sana suala la ufugaji wa sungura nataka niwaambie kwa nini hawamjamuonja sungura ni mtamu sana. Lakini ni biashara moja ambayo kubwa sana. wenzetu wa Kenya wamekuja na utaalamu wa kufuga sungura kiasi ya kwamba kama unafuga sungura katika kipindi cha miezi mitatu maisha yako yanabadilika sana na wao bahati nzuri wanakuwezesha unafuga halafu wananunua wao, kwa hivyo huna tatizo la soko ni kuchangamkia tu fursa mkitaka taarifa zaidi mkifika wizarani tutakupatieni ili wake wanaotaka kujiunga na ufugaji wa sungura basi waweze kufanya kazi hiyo kwa ufanisi mkubwa kuna fedha kubwa sana inapatikana hapa Mhe. Spika.

Mhe. Ali Suleiman Ali na Mhe. Suleiman Sarahan walizungumzia sana suala la ukataji wa minazi. Mhe. Spika, hii ni *sad story*, miaka mitano iliyopita tulikuwa na minazi si chini ya milioni nne, leo tuna minazi haizidi milioni mbili na laki tatu na katika hiyo asilimia sitini ni mikongwe angalau kwenye miembe tunashukuru sana miembe mikongwe ni kidogo kuliko miembe mipya, lakini kwenye minazi hali ni mbaya sana. Lakini kinachotisha zaidi ni hii *speed* ya ukataji wa minazi. Kwanza nataka nikubaliane na waheshimiwa walipouliza juzi hapa inakuwaje hamuwakamati watu na magogo ya minazi yanaonekana barabarani? Hili waheshimiwa tumelichukua na mwenzangu Waziri wa Tawala za Mikoa tumekubaliana tutakwenda kulifanyia kazi tuone ni kwa nini sheria haisimamiwi sawasawa watu wanaokata minazi na kununua magogo ya minazi halafu hawakamatwi. Nakubaliana nao kabisa mia juu ya mia, tutakwenda kulifanyia kazi ni jambo ambalo usimamizi wa sheria sio mzuri na hili ni tatizo

la msingi. *Law enforcement* bado ni tatizo katika nchi yetu na inapotokea kuchukua hatua mnaonekana kama watu wabaya sana. Lakini ni sheria tumezipitisha ndani ya Baraza hili tunahitaji kuzisimamia kwa pamoja. Hili tunakubaliana na waheshimiwa tutalifanyia kazi kwa pamoja.

Mhe. Omar alizungumzia sana suala la kukodishwa mikarafuu kwamba utaratibu wa kukodishwa mikarafuu na kwa sababu mashamba hayatizamwi basi sawa waachiwe watu na kadhalika.

Mhe. Spika, nakubaliana kabisa tunahitaji kukaa kitako kuangalia lakini kwa sasa tunayo sheria yetu ya *procurement* ndiyo inayotuongoza utaratibu mzima wa kurudisha mikarafuu, tukimaliza kuiangalia sheria hii vizuri tukaangalia kama kuna haja ya kubadilisha mfumo nawahakikishia kabisa tutarudi kwenye Baraza hili ili tuombe ridhaa yao na mfumo huo uweze kubadilika. Amezungumzia sana suala la karafuu botea, hata sisi tunapopata ile miche tunapata mabotia madogo ndio tunayapeleka kwenye vitalu vyetu na lazima mkarafu ukae mwaka mmoja na mienzi minane ndio unapata mkarafuu uliokomaa na nilipokwenda kwenye shamba lake nimekuta mikarafuu hiyo imekaa vizuri mimi nashukuru ushauri aliyoutoa ni mzuri. Lakini nataka niwashukuru sana wananchi ambao sasa wenyewe wanaweka vitalu vya mikafuu maomba tuendelee na *speed* hiyo, tufanye kazi hiyo kwa sana na ile mikarafuu iweze kuwa mingi kama ambayo tulikuwa nayo hapo nyuma.

Suala la *Green House* pale chuoni lipo tunatolea mafunzo, Mhe. Rashid Makame aliuliza suala hili. *Green House* ipo pale chuoni wakienda wataikuta tunatolea mafunzo. Kitu kimoja ambacho tumewaambia chuo kwa sababu wao wana ardhi kubwa badala ya kuwafundisha watu katika kilimo cha eka ndogo ndogo wachukue eka kubwa wampe mtaaluma ili akitka pale mwenyewe akaanze kujiendeleza. Kwa hivyo, nasema hilo linashughulikiwa vizuri sana.

Sasa waheshimiwa nataka nizungumzie suala la mchanga. Kabla sijaingia nataka nizungumzie

Mhe. Spika: Mhe. Waziri samahani kidogo, Mheshimiwa kwa mujibu wa kanuni ya 96(5) muda wako wa kufanya majumuisho ni saa moja umeshatumia dakika 40 kwa hiyo utakuwa una dakika 20. Kwa hiyo, jipange vizuri ili uweze kumaliza kwa wakati. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Zinanitosha. Mhe. Spika, kwanza nataka nirudi tena kumshukuru sana Rais Dkt. Ali Mohamed Shein. Dkt. Ali Mohamed Shein alipoingia madarakani mwaka 2010 jambo la

kwanza alilolifanya baada ya kuangalia mazingira yetu yalivyo aliunda Idara ya Misitu, Idara ya Mali zinazohamishaka hatua ya kwanza kabisa alichukua, Rais aliye makini. Halafu aka-*comission* kazi ya kufanya utafiti juu ya rasilimali hizi, 2010 wale wanaofikiri kama kuna kitu kimekurupuka hakuna kukurupuka huyu siye Rais wa kukurupuka.

Kwa hiyo, tarehe hiyo alifanya kazi ya kwanza...

Mhe. Spika: Samahani kidogo kuhusu utaratibu Mheshimiwa.

Utaratibu

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Spika, nimesimama kwa kanuni 13(1) lakini lengo langu ni kanuni ya 59(6).

Mhe. Spika: Endelea.

Mhe. Machano Othman Said: Niendelee ee. Kwa mujibu wa Kanuni ya 59(6) ukurasa wa 46 inasema ni "Marufuku kwa mjumbe yoyote kutumia jina la Rais au Makamu wa Kwanza wa Rais au Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar kwa dhihaka katika mjadala au kwa madhumuni ya kutaka kulishawishi Baraza kuamua jambo lolote kwa namna fulani". *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante imesikika na imefahamika kanuni tuendelee Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, narudia kusema sijapata kumdhihaki Rais yoyote katika maisha yangu. Sijapata kumdhihaki kiongozi yeyote katika maisha yangu. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Naomba uendelee kwenye hoja yako hiyo iache tu.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante, lakini nitafanya zambi kama sitotaja sifa aliyonayo kiongozi ambayo tunahitaji kuiiga. Kwa hiyo nataka nirudie kwamba Rais Ali Mohamed Shein hakukurupuka wala serikali haikukurupuka na ndio maana Oktoba, 2010 aliunda Idara ya kusimamia suala zima la Urasilimali zinazohamishika, hiyo ni hatua ya kwanza. Hatua ya pili aliweka utaratibu wa kufanya utafiti akatafuta timu ya wataalamu wakafanya utafiti, timu ya wataalamu ikafanya utafiti ikaelezea kiwango cha rasilimali iliyopo ikiwemo mchanga, kokoto, mawe na kadhalika. Taarifa hizo zikafanya kazi mpaka mwaka 2015 wakati Waziri wa

Kilimo alikuwa Mhe. Dkt. Sira Ubwa Mamboya akaangiza mambo matatu. La kwanza utafiti uendelee kwa kina suala la mchanga suala la mawe na suala la kifusi, maagizao matatu 2015 wakati wa *Government of National Unit*. Utafiti huo umeendelea mpaka sisi tumeingia kwenye serikali ndio taarifa ikaja wa talaamau wakisema kiwango cha mchango kilichopo na kiwango hicho kiasi gani kitatuchukuwa kwa muda gani.

Nataka nimshukuru sana Mhe. Mohammed Aboud Mohammed kwanza ame-*quote* katiba. Jukumu la Rais alie makini anavyotakiwa kusimamia rasimali za nchi na Baraza hili kwa umakini wake likapitisha sheria namna gani ya kuzisimamia rasilimali hizi. Kwa hivyo, taasisi mbili muhimu sana, Taasisi ya Kwanza ni Rais katimiza wajibu wake kwa mujibu wa katiba na Baraza hili likatimiza wajibu wake kwa kupitisha sheria. Na namshukuru sana Mohammed Aboud Mohammed amezi-*court* hizi sheria sitaki nizirude zimepitishwa na Baraza hili.

Lakini moja katika sheria hizi ni kwamba rasilimali hizi, taka, maji, madini ni rasilimali hizi haziwezi kutumiwa na mtu yoyote ni mali ya serikali ndio sheria inavyosema. Sasa kuna watu wanahoji kwa nini serikali siku zote ilikuwa wapi. Serikali makini inafanya wajibu wake kwa utaratibu ....

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, kuhusu utaratibu.

Mhe. Spika: Mheshimiwa naomba tuendelee tumalize naomba ukae.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Kwa hiyo, hatukukurupuka tu baada ya utafiti ndio serikali ikaweza kuamua kwamba jamaa rasilimali iliyopo haitoshi ni vizuri tuchukuwe hatua.

Mhe. Spika, Baraza lako tukufu limepitisha sheria nyingi ikiwemo moja ya mapato. Mohammed Aboud Mohammed hapa ameelezea mapato ya kiasi gani serikali ilikuwa inakosa katika kipindi chote hichi na sasa yanapatikana. Naomba Mhe. Spika, niwaelezee Waheshimiwa Wajumbe waelewe.

Katika kipindi ambacho serikali imeamua kusimamia uvunaji wa rasilimali hii sio kufanya biashara kama kuna watu wanafahamu tendo la biashara maana yake ni mpaka unapofika kwa mlaji, serikali haijafika kwa mlaji haifanyi biashara inasimamia na inaposimamia pale hununui unapata mchanga si chini ya laki moja na sitini na saba elfu bei imekupangia serikali ukaze kwa shilingi laki mbili na ishirini elfu kwa tani kumi ndio bei ya serikali iliyoweka. Sasa

kama kuna watu hivi sasa na wanaosamehewa kodi lakini bado wanasamehewa kodi ya chakula lakini wanauza kwa bei kubwa ya juu.

Mhe. Spika, katika mwezi wa Machi peke yake kutoka tarehe 6-31 fedha iliyokusanywa ni milioni mia tano thalathini na sita elfu mia nane na hamsini sita mia nane na ishirini na tatu. Katika Ilani ya Uchaguzi katika katiba inazungumzia serikali kusimamia mapato na kukusanya mapato, kwa mara ya kwanza *ZRB* ilikuwa haijapata kukusanya hata kitu kimoja mara hii imekushanya milioni hamsini na moja mia moja na arubaini na mbili shilingi mia sita na ishirinia na sita kwa mara ya kwanza chukuwa kama miaka ishirini waliochimba ni kiasi gani cha fedha kilikosekama.

Ni wajibu wa serikali na ni wajibu wa Baraza hili kusimamia mapato ya serikali someni ile katika inasema vizuri sana. Kwa mara ya kwanza fedha ambayo imekwenda kwenye Halmashauri ni milioni sabini na nne mia saba na ishirini na tano. Sasa ukizungumzia kiongozi ambaye anasimamia maendeleo ya eneo lake hawezi kutetea mtu mmoja akaacha milioni sabini na nne zitakazohudumia skuli, madarasa, afya katika jimbo lake hawezi kuziacha hizo. (*Makofi*)

Mtu yoyote anaeweka maslahi ya taifa mbele huwezi kumtetea mtu mmoja pesa hizi zote azichukuwe zisiende kwenye Halmashauri, Halmashauri ilikuwa inakusanya milioni kumi na kumi na tano lakini kwa mwezi mmoja imekusanya milioni sabini na nne *any serious leader* atahakikisha kabisa wananchi ndio wafaidike kwanza, huu ni mwezi mmoja na mwaka mmoja inakuwa kiasi gani. Kwa mara ya kwanza Halmashauri imelipa mishahara yake mwaka huu. Tunazungumzia ugatuzi, unapozungumzia ugatuzi ni kuzewezesha Halmashauri kufanya kama kuna rasilimali ndani ya nchi wazitumie rasilimali hizi kwa manufaa yao.

Kwa mara ya kwanza Mheshimiwa katika sheria ambazo Mohammed Aboud Mohammed amezisoma hapa. Wajibu tunaemwachia nafasi ile kuchimba ni ku-*habilitate* ile *area*. Serikali haikuongeza kodi hata senti tano imeweka shilingi mia tano for *rehabilitation*. Kwa pesa hizo serikali imepata milioni mia koja na kumi na mbili na thamanini na saba na mia nane na tisini na mbili inakwenda hekta mia tano na sitini ambazo zimeharibika na kusababisha umasikini katika Wilaya ya Kaskazini "B" twende tukazi- *habilitate* hizi *area* angalau ziweze kulima hilo baya Waheshimiwa. (*Makofi*)

Manasema serikali haiko makini iko makini, umasikini umeongezeka katika mkoa huu kwa sababu hekta mia tano na sitini zimechimbwa mashimo

hazipandiki chochote. Tumekwenda sisi na Makatibu Wakuu ingekuwa tumekusudia kutoa *audio* hapa Mhe. Spika, mwananchi wanalia, wanasema shamba langu limechukuliwa nilikuwa nikikodi nikipata kulima, sasa silimi kwa sababu mwenyewe anakuja kuchimba mchanga amekata minazi, amengoa mihogo anasubiri umasikini umeongezeka kiongozi gani anetetea mtu mmoja kuacha jamii yote hii asiweze kuitetea. (*Makofi*)

Someni jamani Ilani ya Uchaguzi mimi ninao na naisoma, kiongzi yoyote lazima kwanza aangalie maslahi ya watu hilo. Lakini Mhe. Spika, Rais hakuridhika na hayo ameunda kamati imeongozwa na Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria na Utumishi wa Umma kuna mawaziri saba kuna na Mwanasheria Mkuu ndani ya kamati kaeni mkazungumze na viongozi, mkaangalie hali halisi, tumekwenda tumekutana na viongozi wote si Mkuu wa Mkoa si Mkuu wa Wilaya wote tumekutana nao tumezungumza nao, tumekutana na viongozi wa kamati ya Siasa ya Chama. Na mimi nataka niwashukuru sana wale viongozi wa siasa na walisemaje walisema huyu nafikiri ni pandikizi la *CUF* linataka kutuvurugia, kikawachekesha nikawaambia nani alikuwa *ASP* hapa hebu anyanyuke mmoja aliekuwa *ASP* hamna.

Hamuwezi kutetea mtu binafsi katika masuala ya kitaifa na ndio tafauti imepatikana tu hapa. Serikali inangalia taifa watu wanaangalia *individual* watu wawili watatu. Baya zaidi Mhe. Spika, *Captain* huyu amekuja na *document* na mimi nasema tutakwenda kuzipeleka kunako husika. Ameleta *documents* za ununuzi wa shamba. Kwanza sheria ya kununua shamba hakuna maana ardhi ni mali ya serikali, ukitaka kufanya hilo lazima urudi kwenye utaratibu wa kiserikali hawakurudi. Pili amefanya biashara hakuna *stamp duty*. Tatu kuna *forgery* aliyoifanya pahala ameweka saini kwa kidole pahala pengine amaweka saini anaenunua mali kuna saini yake aneuza hakuna saini yake hivi kuna biashara hiyo duniani.

Tumemwita kwenye kamati tuelezeeni gharama zenu mlizifanya tupeni risiti zenu hazipo Mheshimiwa tunazipeleka Polisi hizi na nampelekea Mkuu wa Jeshi *forgery* tupu iliyopo hapa anasema anadai *1.3 billion fine*. Tukamwambia *fine* si unadai *1.3 billion* tupe uthibitisho analeta *document* Mheshimiwa ni aibu kama inatoka kwa mtu ambaye ni mwanajeshi, msomi hii hapa mnanyanyuka kumtetea Waheshimiwa mnafanya makosa kwanza fanyeni utafiti. (*Makofi*)

Hatukurupuki hatutaki kumuonea mtu *we call them* njooni mueleze shida zenu mahitaji yenu nini, madai yenu nini pamoja na Mheshimiwa Mbunge Sadifa akasema yeye ametoa milioni mia moja na thalathini kumpa huyu ndugu yake Mwanajeshi, unaushahidi gani juu ya hilo akasema sina hata katika orodha ya

mwanajeshi alieandikwa humu ndani haoneshi jina la Sadifa kama kampa milioni mia moja na thalathini maneno ya uongo, nyinyi mtakuja kutubana nyie kwenye *Public Accounts Committee* pesa hizi zimezitolea kwa misingi gani *document* ziko wapi.

Mimi nimeshakaa Mwenyekiti wa *PAC* Mhe. Spika, atalaumiwa nani serikali makini inafanya kwa utaratibu wake hatutaki kumdhulumu mtu. Aje mtu na vithibitisho tumewaita kwenye kamati, tumewaambia waandike wameandika walioleta hapa ni utumbo mtupu ni aibu. Kwa sababu wanan'gangania sisi tunalipeleka kwenye vyombo vya sheria hatuwachi athibitishe mtu madai yake serikali haitaki kumdhulumu mtu, haitaki kumuonea mtu. Lakini haitochukuwa rasilimali za watu kumlipa mtu kwa sababu ya madai ya maneno, wanaowasingizia wale wazee wamewalipa *hundred and twenty millions.*

Nataka muende mkawaangalie hayo majina tutakupeni, hali yake ya maisha yule mtu hata kanzu ya kuvaa hana amelipwa *hundred and twenty millions* kweli unashindwa kuwa na nguo nzuri, kweli unashindwa na kuwa na nyumba nzuri ya kuishi, maneno ya kupachika saini za ku- *forge* na kadhalika *you can't do that* hatuwezi. Sio Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar labda serikali nyengine. (*Makofi*)

Sasa Mhe. Spika, kuna dai ya kuunda kamati, Rais ameunda kamati kuendelea kufatilia tu *process* nzima hii. Lakini mimi nimeshakaa Bungeni Mhe. Spika, na sijakaa Bunge hili tu nimekaa kwenye Bunge la Mataifa lina Wajumbe elfu moja na ishirini nne nikiwa *external auditor* kwa miaka minne, nikiwa *vice President* nikiwakilisha Afrika kwenye Kamati ya *Finance and Trade.* Kwa hivyo, sizungumzi vitu vya ovyo ovyo nafahamu hakuna Bunge lolote limekwenda kufanya kamati ya kwenda kuvunja sheria waliyoitunga wenyewe, mmetunga sheria, serikali inatekeleza sheria halafu unakwenda kuunda kamati kupingana na sheria yenu.

Maana kamati mnakwenda kwenda kuwatetea watu waliovunja sheria ya nchi *not only that* huwezi kuunda kamati ambapo Rais wako kaunda kamati na yeye mwenyewe ndie mwenyekiti wa kamati hiyo na kamati bado inaendelea kutoa taarifa hata juzi wamepeleka taarifa ya awali *you can't do that* nimeshakaa kwenye Mabunge yote Mheshimiwa Wabunge wanakuwa kila wakati kuibana serikali katika mambo ambayo kama kuna uvunjaji wa sheria na utaratibu na simamizi wa fedha huo ndio utaratibu na Kamati ya Fedha ipo hapa na Mwenyekiti wake ni makini kweli kweli Mhe. Spika, na Wajumbe wake ni makini wote wanaendelea na hiyo kazi ya kufanya utafiti wataendelea kuja kuwasiliana, watakuja kutoa taarifa hapa ndani ya Baraza.

Mhe. Spika, Baada ya kusema hayo naomba kutoja hoja. (*Makofi*)

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, naafikiri.

Mhe. Spika: Ahsante sana Waheshimiwa hoja imetolewa na iemunga mkono. Ahsante sana kwa muda pia Mhe. Waziri maana umetumia dakika 54 katika kujumuisha.

Baada ya hapo sasa, Waheshimiwa Wajumbe naomba sasa niwahoji. Wale wote wanaounga mkono hoja ya Mhe. Waziri wa Kilimo wanyanyue mikono, wanaokaa, waliokubali wameshinda. Mhe. Waziri. (*Makofi*)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja ialiamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, kwa kuwa Baraza lako limejadili kuikubali Hotuba ya Bajeti ya Wizara. Sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama kamati ya Matumizi ili kuvipitisha vifungu vya Matumizi wa Wizara yangu. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

KAMATI YA MATUMIZI

Fungu L01 Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi

Jumla Kuu

4,930,197,000

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu PL0101

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, mimi nilitaka kuuliza itasomwa PL0102 au nipige hapa hapa?

Mhe. Mwenyekiti: Nafikiri bado.

Mhe. Jaku Hashi Ayoub: Nauliza itasomwa hii au hapa hapa maana yake nisije kusahau

Mhe. Mwenyekiti: Itasomwa

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ah basi mimi mtu wa mwanzo unione.

Kifungu PL0101 Programu Kuu ya Maendeleo ya Kilimo
35,849,583

Mhe. Mwenyekiti: Hukuwahi Mheshimiwa tunaendelea.

Kifungu PL0102

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sasa nitataja orodha ambayo nitawapa hiyo nafasi nitaanza na wewe Mhe. Jaku Hashim Ayoub atafuatiwa na Mhe. Machano Othman Said atafuatia Mhe. Hassan Khamis Hafidh, Mhe. Suleiman na halafu Mhe. Nadiri Abdul-latif Yussuf.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana ....

Mhe. Mwenyekiti: Naomba Mheshimiwa uende kwenye hicho kifungu husika unachokitaka na jielekeze zaidi kwenye matumizi au sera, tusingependa tuanze kumtaka Mhe. Waziri atuhutubie upya tena.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu ni kifungu hichi kusimamia na kudhibiti maeneo ya wachimbaji maliasili zisizorejesheka.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante endelea.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante**,** Mhe. Mwenyekiti, tupo hapa kuna milango mitatu ya kuingilia ndani ya chombo hichi, moja kutoka Jimbo la Ikulu, moja Viti Maalum na moja Wananchi na mwezi huu Mtukufu wa Ramadhan tumechukua dhima kwa wananchi ndio maana chombo hichi kikaitwa Baraza la Wawakilishi kuja kuwakilisha Wananchi. Hii hoja ni ya muda mrefu na nilitaka kauli ya serikali katika kipindi kilichipita kuhusu kadhia ya mchanga. Elimu iliyotolewa ni ndogo na akajipapatua sana Mhe. Waziri kipindi kile ilikuwa suala la maji akasema hoja imeshatolewa nikawaambia kuwa suala la majibu mbali na hoja mbali..

Mhe. Mwenyekiti: Nenda kwenye hoja yako moja Mheshimiwa moja kwa moja usirudae.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mheshimiwa cha kusikitisha hii biashara iliyofanywa, serikali imeenda kuichukua wao, sasa baada ya wananchi kuwanyang'anya na cha kushangaza mchanga huu walipokuwa wanauza wananchi ulikuwa bei ya chini kuliko wanavyouza serikali na mashamba watu wameshamiliki miaka 12/13 na Mhe. Waziri kama nitakosea Ramadhan Mwenyezi Mungu anisamehe. Aliita watu wa Donge Ofisini kwake, akawaambia hata kama wapiga kura wanaweza kumchagua hata yeye. Aliwachukua wapiga kura wakaenda Ofisini kwake akasema wakati ukifika wa kupiga kura haya maneno yanatoka Donge hata kumchagua watamchangua yeye, kama nimekosea Ramadhani Mwenyezi Mungu anisamehe, lakini maneno hayo yanatoka Donge.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa ili isiwe hotuba refu sana hebu nenda *specifically* hicho unachokihitaji moja kwa moja.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Nataka itolewe elimu wananchi wale niiombe serikali tunapokwenda 2020 Mwenyezi Mungu akitujaalia na tunachokipanda ndicho tunachokivuna na Ilani ya Chama cha Mapinduzi alisema mwenzetu alipewa katika kula kiapo. Kwa hivyo nimuombe tu yale mashamba awarejeshee kuna watu wameshahodhi zaidi ya miaka 12, na kwa nini sheria hii ipo Unguja tu Pemba haipo ya kutumika mchanga huu, sheria hii Pemba haipo watu wanachukua mchanga kama kawaida kwa nini itumike Unguja tu. Mhe. Mwenyekiti, naomba muongozo wako.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Waziri mwenyewe.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka nimshukuru sana Mhe. Jaku Hashim amezungumza jambo la msingi sana, suala la taaluma na ndio maana tumefanya kazi kubwa sana ya taaluma ndani ya Baraza hili hapa kwanza. Lakini ile kamati aliyoiteuwa Rais alipanga programu ya kwenda kukutana na wananchi wote tena katika ngazi zote na programu imeshatolewa tutakwenda kutoa taaluma juu ya rasilimali za nchi, umuhimu wake wa kutunza na namna gani nchi itapata hasara kama rasilimali hizi hazikuwa. Nakubaliana na wewe kabisa kwamba suala la taaluma ni la muhimu sana na tutaendelea nalo, na semina tutafanya kwa Baraza la Wawakilishi tutawaletea wataalamu hapa watawaonesha hasa athari ambazo zimepatikana na ambazo serikali mipango imefanya ili tupate kwa taaluma kwa sote pamoja. Nakubaliana na yeye kabisa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, namshukuru Mhe. Waziri kwa kukiri kuwa taaluma ni ndogo na ndio ukweli ulivyo taaluma

ni ndogo. Lakini uzoefu wa serikali humu ndani ya Baraza kwenye chombo hiki ni kwamba serikali iko mbioni, matunda yake yataonekana, huku watu wanazidi kuteketea.

Hoja yangu mimi kwa hivi sasa ili tumpitishie bajeti yake, kwa muda huu akubaliane kugawana nusu na wale wananchi, mashamba amechukua zaidi ya bilioni na sheria ya nchi inasema kwamba kuna katiba kuna sheria, mtu akishakaa miaka 12 lile eneo keshajiendeleza, alipwe *compensate* ya *value ya market* iliokuwepo. Kwa hivyo, kwa muda huu ili tumpitishie, vyenginevyo wajumbe ningekuombeni, kama hatutokuwa wanafiki tupigeni kura twendeni na hoja kama tutakuwa wa kweli, nisiwe mimi mbuzi wa kafara tu humu ndani.

Mhe. Mwenyekiti: Hapana Mheshimiwa, suala la kura. Tunaendelea Mhe. Machano.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana. Waheshimiwa Mawaziri wawili wamejibu hoja zetu, wamejitahidi sana kujibu na mmoja akazungumzia mpaka ilani ya CCM.

Mhe. Mwenyekiti, mwaka 2010 mpaka 2015 tulikuwa na mawaziri wanasoma ilani ya CCM, hawakupitisha wanasoma ilani ya CCM.

Mhe. Mwenyekiti: Najalia Mhe. Machano Othman, hoja yako iko kwenye kipengele hiki.

Mhe. Machano Othman Said: Hicho hicho.

Mhe. Mwenyekiti: Haya.

Mhe. Machano Othman Said: Lakini tukaachana mwaka 2015, tukabakia sisi wenye ilani wale walioisoma waliondoka. Nahofia sana isije na mwaka 2020 tukawa hivyo hivyo, wenye kusoma wakaondoka na wale waliyokuwa yao wakaendelea nayo.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye hoja, maelezo ya Mhe. Waziri ni mazuri lakini yana masuala mengi kuhusu mchanga. Masuala mengi ya Mhe. Waziri ndio ambayo yanatufanya sisi wawakilishi tulete hoja ya kuunda Kamati Teule, yale masuala mengi aliyosema Mhe. Waziri kama wananchi waongo wamedanganya Baraza hili watajua au ukweli wa serikali wataujua.

Lakini lengo kubwa zaidi Mhe. Mwenyekiti, ni kulinda maslahi ya serikali na maslahi ya wananchi na Chama cha Mapinduzi, kwamba kweli mchanga umepungua Zanzibar hata mimi nakubali, lakini kuwe na utaratibu mzuri utakaowanufaisha wenye mashamba, serikali na watumiaji wa mchanga. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, ilivyokua mchanga kwenye mashimo unauzwa na wenye mashamba, basi gari kubwa ya mchanga ilikuwa shilingi 35,000/-, leo gari shilingi 100,000/- wanauziwa wenye magari shimoni, maana yake bei ya mchanga ipande. Sasa kama tusiunde Kamati Teule mimi nina pendekezo jengine, kwanza serikali ikubali hapa kwamba itaangalia kushusha bei ya mchanga shimoni, ili wananchi wa Zanzibar wanufaike ambao ni maskini.

Pili serikali ikubaliane na wenye mashamba kwamba kama gari ya mchanga itakuwa shilingi 70,000/- basi serikali ichukuwe shilingi 35,000/- na wenye mashamba wachukuwe shilingi 35,000/- baada ya kutoa zile gharama Mhe. Waziri alizozisema za kuyaendeleza maeneo baada ya uchimbwaji wa mchanga, zile zitolewe mapema kama mechi ya mpira unatoa mambo yote kabla ya kutoa ile *get collection* yenyewe, zitolewe halafu wagawane serikali na wenye mashamba.

Lakini jambo la tatu, wakati wa uchukuaji wa mchanga wenye mashamba washuhudie idadi ya gari au *trip* zinazochukuliwa katika maeneo yao, hapo tutakubaliana na serikali.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mheshimiwa, lakini naona hoja zako zimekuwa nyingi, yaani umelihodhi wewe suala hili peke yako, maana yake wengine wakinyanyuka hapa sasa wasilizungumzie tena suala la mchanga.

Nimpe Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Ikulu.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi katika kutoa mchango wangu katika kutoa ufafanuzi kwa lile ambalo Mhe. Machano Othman Said Komredi ambaye ni Mwakilishi wa Wananchi wa Jimbo la Mfenesini, ambaye aliuliza hoja tatu. Hoja ya kwanza alikuwa anauliza kwamba serikali kama iko tayari kushusha bei ya mchanga kule bondeni.

Msingi kwamba serikali haijapandisha bei na serikali tutasimamia bei hiyo hiyo ndogo ili wananchi wetu waweze kufaidika.

Pili ametaka serikali ikubali utaratibu wa kugawana nusu kwa nusu baada ya kutoa gharama za uchimbaji, serikali hatuna tatizo na hilo tunakubali tugawane nusu kwa nusu, lakini msingi upo pamoja. Huyu tunayetaka tugawane na yeye awe ni yule *owner* wa lile shamba, kwa maana kwamba awe ni mtu analimiliki shamba kihalali. Mgogoro mkubwa uliopo hapa kuna tatizo baina ya serikali na baadhi ya watu ambao hawana vielelezo vya kumiliki hayo mashamba. Kwa hivyo, kama kutakuwa kuna mwananchi yeyote anamiliki shamba kihalali, ana vielelezo vyake serikali tunakubali kwa asilimia 100 tutagawana naye kwa kadiri utaratibu wa kisheria unavyoelekeza na yeye atapata kile ambacho anastahiki.

Hoja ya tatu ya wenye mashamba kuweza kushiriki zoezi. Hatuna tatizo nalo, wenye mashamba watakuwepo watahesabu na watajiridhisha, msingi unabaki pale pale mwenye shamba lazima ithibitike kwamba huyu ndiye mwenye shamba kweli, asije akawa mtu ambaye yeye anajipachika jukumu la kumiliki shamba na jukumu la kumiliki ardhi minhali yeye siye mmiliki halali. Kwa hivyo, wamiliki halali watashiriki zoezi la ku- *count* hayo magari na watapata huo mgao nusu kwa kujiridhisha kwamba *how there real the owner of that peace of land* hilo halina tatizo na serikali. Msingi ni kwamba ahakikishe kama mtu huyo atakuwa hana vielelezo basi serikali hatutokubali ku- *interven* na utaratibu wa serikali utaendelea kama ulivyo.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Mwenyekiti, mimi humu Barazani tutakuwa ma-*senator* wengine umri ni mrefu. Mhe. Gavu na yeye anaingia kipindi cha pili na ni mtu wangu wa karibu sana. Nakubaliana na mapendekezo matatu ya serikali.

1. Waangalie bei ya mchanga shimoni waishushe.
2. Walipane nusu kwa nusu na wenye mashamba hao halali watakaokubaliana nao. 3. Wenye mashamba washuhudie uchukuaji wa mchanga katika mashamba yao.

Kwa hivyo, mimi hoja yangu ya kuunda Kamati Teule naiondoa na tunaomba tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa nafikiri hakuna haja ya kutoa maelezo zaidi. Dayaspora. Samahani, subiri Dayaspora. Mhe. Waziri kuna maelezo.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kwanza Baraza hili linakwenda

kwa *record Hansard* zinabakia. Naomba tuweke *Hansard* sawa Mhe. Mwenyekiti.

Kwanza serikali haijapandisha bei ya mchanga, serikali imeweka kodi ambayo ilikuwa hailipwi ya *stamp duty*. Kodi hiyo ni asilimia 3 kwa kila tani, yaani shilingi 3,000 kwa tani ambayo kwa gari ya tani 10 ni shilingi 30,000 na shilingi 1000 ni ada ya halmashauri *local government* husika, shilingi 25 wanalipwa wale wanaopakia wachimbaji kwa maana ya ajira kwa vijana, wale wachimbaji binafsi yule mwenye gari anawalipa wale wala haziji serikalini. Shilingi 500 ndio ada inayokwenda kwenye Idara ya Maliasili zisizorejesheka. Kwa hivyo, mwenye gari ya tani 10 shimoni analipa 61,000/- kwa hiyo serikali bado haijapandisha bei. Nilisema niseme hili Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Samahani Mhe. Waziri, mimi nadhani ungekuwa unatoa msaada mkubwa ungetoa rai nini kifanyike, kwa sababu sasa hivi bei za mchanga ziko juu huku kwenye soko. Sasa nadhani ungetueleza ni kitu gani tunahitaji, kwa sababu sote tunajua serikali haijapandisha bei, lakini kuna kitu kimefanyika ndio kimesababisha bei ipande. Sasa serikali itafanya nini ili yule mtu wa mwisho anayenunua kule kwenye gari apate bei kama hapo mwanzo, nafikiri ndio maelezo yangekuwa mazuri zaidi.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Hilo halina matatizo Mhe. Mwenyekiti. Lakini ilikuwa kwanza ndio niweke sawa ya ile bei ambayo ilitajwa kwamba serikali imeongeza bei. Mhe. Mwenyekiti, hapa lazima utukubalie tuweke sawa ili wananchi waelewe.

Lakini kilichopo inaonekana wafanyabiashara wa mchanga wale wenye magari ndio wanaopandisha bei. Cha msingi hapa kauli ambayo serikali inachukua tutachukua hatua ya kufuatilia ili tuweze kudhibiti hii hali. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Machano Othman nakupa nafasi ya mwisho. Mhe. Jaku Hashim hata usi-*attempt* hata kusimama, kwa sababu nilishakupa nafasi na ulikwisha kumaliza hili suala. Hapana Mheshimiwa usinyanyuke *please*. Tuendelee Mhe. Machano Othman.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Mwenyekiti, napata bahati mbaya sana leo napambana na watu wangu wa karibu sana tena, nisingestahili kusimama, lakini ukweli lazima uwe ukweli na tukiendelea kubishana inakuja ile hoja kwamba Baraza lijuwe, lakini hatutaki kufika huko bei wenye magari wanadai wanauziwa kwa shilingi 100,000 ndio maana na wao bei yao imekuwa kubwa.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, kwa ukweli kabisa sisi tumekubaliana, kama hiyo bei ni kubwa hivyo, basi ishushwe na kama iko ndogo haikufika hivyo maana yake hakuna haja ya kuishusha, lakini kama iko bei kubwa basi ishushwe kama iko ndogo haikufika hivyo maana yake hakuna haja ya kuishusha lakini kama iko kubwa ishushwe. Hilo la kwanza.

La pili wenye mali nao wagawane nusu na serikali na tatu washuhudie mali yao ikiondolewa. Hayo ndio ya msingi. Sasa Mhe. Mwenyekiti, mimi Mwenyekiti pia wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum. Sisi huwa tunatembelea mashimo ukiwacha hayo ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo na sisi tuna uwezo huo kwa sababu Halmashauri ya Kaskazini 'B', kabla yale aliyosema waziri kwamba wamepata pesa mara hii shilingi 74 milioni, walishavuka lengo kwa asilimia 105 kwamba walikuwa wakipata zamani.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, tusitake kutoa mengi tukubaliane hayo matatu, Baraza likubali na serikali itekeleze.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, nataka niendelee tena kumshukuru sana mheshimiwa. Nataka nirudie kwamba serikali haitomdhulumu mtu yeyote haki yake hata siku moja. Tunachoomba serikali ni mtu athibitishe uhalali wa madai yake hicho ndio kitu cha msingi, njoo uthibitishe madai yako. Wanaosema kwamba wana maeneo hayo, tuliwaomba watuletee hati zinazowaonesha kwamba kweli wanayamiliki maeneo hayo, hakuna hata mmoja aliyeleta hati. Wanasema tumenunua. Utaratibu wa kununua mali ya serikali upo, tuletee utaratibu wa kununua mali hiyo, haupo.

Kwa hivyo, nataka niwaambie Waheshimiwa Wajumbe, kwamba serikali iko tayari kufidia na kuna fungu la fidia hatujalisoma tu. Kuna fungu la fidia tumeliweka makusudi, kwamba yeyote mwenye madai yake fungu la fidia lipo alipwe haki yake, ilimradi athibitishe madai yake.

Mhe. Mwenyekiti, suala la bei. Bei ya serikali mpaka mchanga ukafika Mwanakwerekwe ni shilingi 220,000 kwa tani 10. Ni kweli watu wanaongeza bei wenyewe huko ndani. Tulikutana na wafanyabiashara hawa madereva tukawauliza ni sababu zipi ambazo mmeongeza bei. Mhe. Haroun Ali Suleiman yupo hapa shahidi ndio mwenyekiti wangu wa kamati. Wakasema ooh! mafuta yamepanda bei, kitu gani sijui kimepanda bei wala hakihusiani na mchanga. Tukawauliza kinahusianaje na mchango hicho na hata mkapandisha bei. Kwa hivyo, unachokisema kwamba tukafuatilie. Mimi nakubali kabisa tutakwenda

kufuatilia. Lakini madai yote halali tuko tayari kuyalipa kwa asilimia mia juu ya mia. Narudia tena, madai yote halali tukishapitisha hapa mtakuja *PAC* mtatuuliza, mmelipaje malipo haya na hayana vithibitisho na sisi tumefuata sheria. Lakini Mhe. Mwenyekiti, hakuna anaye *own* ardhi, ardhi ni mali ya serikali na ardhi maana yake ni nini?

Mhe. Mwenyekiti, ardhi maana yake ni madini, maji na cha tatu ni ufukwe. Hizo aina tatu, sheria tumepitisha ndani ya Baraza hili, kilichoko juu ya ardhi ndio haki yako na ndio maana tunawaita wahusika twende tukaangalie kilicho juu tufanye hesabu tukulipeni. Mhe. Mwenyekiti, hawakuja na barua zipo. Mwisho wameandika barua za hasira tu kusema kwamba serikali iendelee kufanya inavyotaka, huwezi kuiambia serikali hivyo. Barua zipo waheshimiwa tumezikabishi Kamati yetu ya Fedha, Biashara na Kilimo iangalie itakuja kutoa taarifa mkipenda hapa ndani. Lakini nasema serikali iko tayari kabisa kulipa fidia ya gharama yoyote halali. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hassan Khamis Dayaspora labda nikutanabahishe tu, jibu limeshakuwa *covered* unakuja kwa *issue* nyengine.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, bora nisikilize na mimi kidogo hoja yangu halafu. Mhe. Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kwa kunipa fursa hii. Mhe. Mwenyekiti, naomba kusema pamezungumzwa bei na mambo mengi. Lakini kuna kitu kimoja kimeshindwa kuzungumzwa ambacho kinafanya mchanga upande, kuwa na zamu kule shimoni

Mhe. Mwenyekiti: Hapana Mhe. Mjumbe, kwa sababu tumesha-*cover*, twende na hizi kanuni na taratibu Mhe. Mjumbe. Kama una hoja nyengine nakuruhusu uzungumze hapo hapo kama linahusiana na hili *please*.

**Mhe. Hassan Khamis Hafidh (Dayaspora*): When do respect Mr Speaker I have to sit down*.

Mhe. Mwenyekiti: *Thank you very much*. Mhe. Suleiman na wewe hivyo hivyo.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Mwenyekiti, mimi siko kwenye mchanga kabisa, nadhani hilo limeshafahamika. Mhe. Mwenyekiti, mimi niko kwenye HN01020101 Kuhifadhi na kusimamia misitu ya hifadhi mashamba ya serikali na mikoko.

Mhe. Mwenyekiti, kuna msemo unasema kwamba "Tumbili akisha miti huja mwilini". Mhe. Mwenyekiti, katika kuwasilisha mchango wangu nilipeleka hoja kwa maandishi kumwambia Mhe Waziri kwamba kuna misumeno ya moto ambayo kwamba tayari inakwenda kule kwenye mikoko inakatwa kwa kasi sasa. Ndio hilo lengo la kusema kwamba Tumbili akimaliza miti huja mwilini.

Mhe. Mwenyekiti, juzi nilipokuwa nilipokuwa nikichangia hapa nilimuuliza Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi Mhe. Hamad Rashid, akaniambia kwamba tunasubiri ilani ya kutekeleza kwa kipindi cha miaka mitano.

Mhe. Mwenyekiti, bahari haisubiri ilani ya Chama cha Mapinduzi wala ilani yoyote ile, kila kukicha inakuja juu. Sasa nataka kumuuliza Mhe. Waziri je, ana mpango gani wa kuhakikisha kwamba misumeno ile ya moto kila Shehia ndio inakohusika, kwa sababu kila Shehia misumeno hiyo nadhani iko na kwa kila Shehia kuna kiongozi wake wa kusimamia ni Sheha na kwa kila Sheha nina imani kwenye Shehia yake anajua kwamba nani na nani msumeno wa moto anao na kibali hana.

Je, nataka kujua hapa Mhe. Waziri kuna mpango gani wa kuhakikisha kukaa na masheha na kuwadhibiti hawa waliokuwa na misumeno ya moto ili kuhifadhi haya mazingira yetu yasipotee kila siku, nilitaka kujua hilo.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, kwanza napenda nikubaliane sana na Mhe. Mjumbe kwamba ni kweli kuna mmong'onyoko mkubwa sana wa ardhi, ukataji wa mikoko umekuwa mkubwa na mazingira yanaharibiwa kwa nguvu sana. Kimoja katika kilio chetu ni kwamba ni vipi tunaweza kushirikiana na ndugu zetu masheha na kamati zao za ulinzi na usalama kudhibiti hali hii. Tumejitahidi sana kukamata misumeno tumeichoma moto na kadhalika. Lakini bado *traffic* kubwa ipo.

Mhe. Mwenyekiti, jambo moja ambalo tumeligundua ni hii mizigo ambayo inaingia bandarini, watu wanaleta *used* kontena lakini ndani yake wanachomeka misumeno. Pengine pale ndio pahala pa kuanzia kabisa kuona kama *entry point* ya misumeno inazuiwa. Hiyo ni hatu ya kwanza.

Hatua ya pili tutaendelea kukutana na Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya ili tuone ni utaratibu gani sasa tuuchukuwe kwa yale maeneo ambayo misumeno ya moto inatumika. Kwa hivyo, nakubaliana na hoja yake na tuko tayari kuifanyia kazi.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Kwa vile Mhe. Waziri amelikubali hilo, mimi nasema tuendelee wala sina tatizo lolote.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy:

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Ahsante sana Mhe. Spika, mimi nimebahatika mtu wa mwisho, lakini pia hatuko kwenye mgogoro wala kusumbuana mimi ningeomba Serikali…

Mhe. Mwenyekiti: Kifungu kipi?

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mimi nataka atwambie bei ya mchanga…

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa suala la mchanga *please.*

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Bei tu watwambie kwa sababu zamani 220,000 sasa hivi 670,000.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa lishazungumzwa hilo Mhe. Nadir *please* naomba ukae kama unalo jengine tuko tayari kukusikiliza labda hukuridhika na majibu ya soko lake lile la wapi lile unataka kuzuia kifungu sawa.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: La soko hapa halihusiani .

Mhe. Mwenyekiti: Haya basi naomba ukae tunaendelea Waheshimiwa, Mhe. Omar Seif Abeid wewe ulichelewa kusimama watu wamenyanyuka watu watano nikawaita kwa majina watu wote, sasa hivi wewe hapa unataka kudandia au kuchupia hapana tunaendelea.

Kifungu PL 0102 Maendeleo ya Rasilimali za Misitu na Maliasili zisizorejesheka

2,770,947,000

Kifungu PL 0103

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mwenyekiti, nimesimama kwa kifungu HL0010203 Juu ya suala zima la kadhia kwa upande wa chakula cha mifugo, nilimuomba sana Waziri atakapokuja humu anambie mbinu gani mbadala zitakazofanyika ili kuweza kuwasaidia wafugaji wetu kwa suala zima la chakula cha kuku, bei zimekuwa zinatisha sana wafugaji wanashindwa

kufuga hata lile lengo la kuondoa umasikini linashindikana, hilo jibu sijalipata naomba nielekeze mpaka nifike kwenye safari yangu.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Uvuvi na Mifugo: Mhe. Mwenyekiti, nikubaliane kabisa na Mhe. Mwakilishi kwamba lipo tatizo kubwa sana la chakula cha mifugo na moja katika Serikali kuja kufanya ni kuanza kwa upande wa kuku, nakumbuka tulikuwa na shamba letu la kuzalisha chakula cha kuku akapewa muwekezaji kwa bahati mbaya hakuwekeza. Kwa hivyo Wizara ya Fedha sasa imetakiwa kuchukua ile mali kurudisha ili tutafute njia nyengine ya kuwekeza bahati nzuri *process* hiyo inaendelea na nakuhakikishieni kabisa kuwa kutapatikana wawekezaji wa kuwekeza katika shamba lile ili angalau tuweze kupata chakula cha kuku. Katika kitu ambacho kinawagharimu sana wafugaji ni bei ya chakula cha kuku tunachokiagizia hii tuko kwenye *process* tunalishughulikia.

Kwa upande wa chakula cha mifugo cha wanyama ni kufuga majani tutawapatia mbegu za majani ili waweze kupata majani ya kula ng'ombe mimi naamini hilo tunaweza kufanya, lakini hasa kubwa ni hili la chakula cha kuku nakubaliana nae kabisa na hatua tumekuwa tukifanya kulishughulikia hili suala.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante pamoja na majibu ya kisiasa zaidi kuliko utekelezaji kwa sababu hii kesi hata katika Baraza lililopita tulizungumza kadhia hiyo, sasa atanithibitishia mwaka gani au bajeti gani angalau Zanzibar tuweze kurudisha kile kiwanda chetu cha chakula cha kuku ili watu wetu waboreke zaidi wapambane na kuondoa umasikini. *Unless otherwise* kama hana jibu natuendelee lakini nataka mwaka gani kile kiwanda kitaanza kazi pale kama alivyozungumza.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Uvuvi na Mifugo: Mhe. Mwenyekiti, mategemeo katika kipindi cha miaka miwili hii Kiwanda kitakuwa tayari.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Mwenyekiti, mimi kwenye Wizara hii wala usiwe na wasiwasi kwa sababu Waziri nimemkubali na kaingia na dua nzito leo, sasa uzuri wa Wizara nyengine zinazokuja ndio vizuri zaidi Ramadhani.

Mhe. Mwenyekiti: Kifungu tafadhali.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Mwenyekiti mimi nilizungumzia suala la mifugo na sisi nchi yetu ni ya Utalii nilizungumzia suala la mbwa na paka, ambao wanazurura nje wanatishia watu wanakichaa na

wengine hata watu wakila wanakuwa wanapata usumbufu kweli hasa maeneo ya Forodhani na nyenginezo, nikazungumza na nikamuomba Mhe. Waziri watafanya utaratibu gani wa kuwachukua hawa Mbwa na paka wanaosumbua watu kwenye sehemu wanazokula na katika jamii inayozunguka Zanzibar nzima.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Uvuvi na Mifugo: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka nikubaliane na Mhe. Nadir kwamba wanyama wengi wanatusumbua juzi tulikuwa na tatizo la ndugu zetu wa Tumbatu kuna kima karibu 5000 ukipanda wanatoa tukajitahidi kushirikiana na Mhe. Waziri hapa tukenda tukapiga kima 553, kwa hivyo nakubaliana kabisa lipo hilo tatizo tunahitaji kukaa kitako pamoja sisi na Serikali Wizara ya Tawala za Mikoa ili tuone kwa upande wa Halmashauri tunafanyaje kudhibiti kwa sababu haya yako kwenye mazingira ya Halmashauri sisi Wizara tuko tayari kutoa msaada wa hali na mali na kitaalam ili tukabiliane na tatizo hilo, nakubaliana tatizo lipo tutalikabilia kwa pamoja.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa vile mimi sikupata majibu kwa sababu muda nadhani ulikuwa hautoshi nilipeleka mchango wangu wa maandishi, kwanza nipo kwenye kifungu cha HL 01040105 kuimarisha fursa za uwekezaji katika ufugaji wa samaki na mazao ya baharini.

Mhe. Mwenyekiti, ukiwa mvuvi ukitajiwa samaki hata ukiwa usingizini unamjua bila ya kuamka katika jimbo langu Ndagoni asilimia kubwa ni wavuvi.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa huko hatujafika.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Hivyo.

Mhe. Mwenyekiti: Wee uko chini huko sisi tuko juu bado.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante Mwenyekiti.

Kifungu PL 0103 Maendeleo ya Mifugo

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa tunaendelea maana yake tumeshamaliza hili tuendelee.

Kifungu PL 0103 Maendeleo ya Mifugo
2,613,701,000
Kifungu PL 0104

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa nitaanza na Mhe. Suleiman halafu Mhe. Abdalla Maulid Diwani, Mhe. Hassan Khamis Hafidh, nakuona nyuma huko Mhe. Omar Seif Abeid halafu nitamalizia na Mhe. Jaku ikisha nitakuja na wewe Mhe. Nadir.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mwenyekiti, tuko kwenye Ramadhani na pengine Ramadhani husababisha pia nisione baadhi ya wakati mwengine, Mhe. Menyekiti nipo kwenye kile kifungi cha HL010405 Kuimarisha fursa za uwekezaji katika ufugaji wa Samaki na mazao mengine ya baharini.

Mhe. Mwenyekiti, wananchi wangu wa Ndagoni katika jimbo langu hususan Ndagoni ni wavuvi wanajitahidi katika masuala haya ya majongoo na uvunaji wa samaki …….

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. halafu kwanza futa kwamba huoni vizuri kwa sababu umefunga?

Mhe. Suleiman Makame Ali: Nilikwambia kwamba Ramadhani huenda ikasababisha.

Mhe. Mwenyekiti: Hapana Ramadhani inakupa siha nzuri zaidi tuendelee.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kunielewesha hilo Mhe. Mwenyekiti, wananchi wangu wa Ndagoni wanafuga samaki kuna mabwawa yasiyopungua kumi kule ya ufugaji wa samaki, lakini wafugaji wale hawana taaluma yoyote mpaka leo hii karibu ni mwaka wa nne tangu waanzishe ufugaji wa samaki ule.

Lakini pia na majongoo kule Ndagoni yanapatikana kwa wingi lakini vile vile taaluma hiyo ya ufugaji wa majongoo hawana na wala hawajawahi kupata, kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri kwamba kuhakikisha kwamba kule Ndagoni katika ule masuala ya ufugaji wa majongoo atanihakikishiaje kwamba wafugaji wale watapata taaluma ya ufugaji wa samaki na ufugaji wa majongoo ili waachane na kwenda kuvua uvuvi haramu unaokataziwa.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Uvuvi na Mifugo: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka nimshukuru Mheshimiwa na mimi nimetembelea kwa wafugaji wake wa samaki pamoja na majongoo, kwanza Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu moja ya kuanzisha hichi kituo cha uzalishaji majongoo kwa wingi mbegu ya majongoo kwa sababu tumeona ni biashara ambayo ina faida kubwa na inaweza kuondoa umasikini kwa kiwango kikubwa sana, hesabu tulizopiga ni kwamba Pemba wanahitaji vifaranga vya majongoo na samaki kama milioni mbili na Unguja kama laki saba. Kwa bahati nzuri sisi tunazalisha kama milioni kumi tutapata vile vile kuuza kwenye masoko ya nje, kwa hivyo nataka nimhakikishie kabisa hatuwezi kuzalisha bidhaa hiyo halafu tusitoe taaluma kwa hivyo taaluma tutaendelea kuitoa na kwa bahati nzuri tumepata jumuiya nyingi ambazo zinatuunga mkono katika kuendeleza biashara hii.

Kuna mfanya biashara mmoja ameshaanzisha vituo 13 sasa hivi na kila kituo katoa milioni kumi kuweza kufuga majongoo, tuna mpango sasa hivi atakwenda Pemba atafanya kazi hiyo lakini vile vile Benki ya kilimo wamekutana nae huyu mfugaji ili tuone kwamba si tu kama tunazalisha majongoo na kusafirisha lakini tuya-*process* wenyewe na tuweze kuyasafirisha nje. Kwa hivyo namhakikishia kabisa hii *project* hii itasaidia sana kwa sababu ni ya muda mfupi inaengeza mapato kwa haraka sana na mimi naamini kabisa wafugaji wake tutawatembelea ili tuone namna gani tunaweza kuwasaidia zaidi.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa vile Mhe. Waziri amekubali na ni vizuri katika kuwatembelea wafugaji wangu hao au wavuvi wangu wale wa Ndagoni na mimi anishirikishe Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, mimi wakati nachangia nilizungumza suala zima juu ya ufugaji wa vifaranga aliosema Mhe. Waziri, seuze vifaranga vya kuku lakini vifaranga vya samaki anataka atuletee Mhe. Waziri na vipo, lakini nikazungumza kwamba ni kweli Zanzibar imefika wakati sasa hivi kutokana *Geography* yetu asilimia kubwa sana tumezungurukwa na bahari kuna masamaki chungu nzima kule bahari kuu, hata hapa karibu karibu wengi washamaliza lakini kule ukisogea mbele kidogo tu wapo. Umefika wakati je atawaezesha vipi wale wavuvi wadogo wadogo *at least* wapate nguvu za kwenda kuwavua wale samaki kuliko sasa hivi kufuga samaki mpaka tumvue.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Uvuvi na Mifugo: Kwanza Mhe. Mwenyekiti, niseme tu kwamba katika sekta ya uvuvi si tu peke yake watu kwenda kuvua na ukenda sasa hivi Duniani sehemu kubwa watu wanajitahidi sana kufuga samaki, kwa sababu ya tabia ya nchi samaki wakati mwengine wanakosekana kwa sababu ya uharibifu wa mazingira kwenye bahari samaki wanakosekana na nyinyi mnashuhudia hapa ulikuja upepo mkali hakuna mvuvi anayekwenda baharini. Lakini kama una mabwawa ambayo yanafugwa samaki kwa hivyo huwezi kupata upungufu wa samaki, ndio sababu kubwa sio sisi tu nchi nyingi wanafanya hivyo. Wenzetu wamefika mbali zaidi ukenda Omani wametenga hekta 100 ya kufugia samaki tu wamefanya heavy investment kwa sababu ni biashara moja ya uhakika ukenda Asia ni hivyo hivyo.

Lakini biashara pekee inayoweza kutusaidia kusafirisha samaki kwa uhakika mbali ile ya kwenda kuvua baharini siku unapata siku hupati unafanya hivyo, lakini kuna ufugaji mwengine Mhe. Mwenyekiti, vile vile tunaita *hatching* unakwenda katika bahari unaweka chombo pale samaki wanakuja wanataga wanavuliwa kwa urahisi sana, tunanunua mia mbili wenzetu Bara wameshanunua kama 120 sasa hivi wameweka pale nasi tunategemea kununua 200 kwa kampuni yetu itakapoanza kazi ili tuwe na uhakika wa kupata samaki. Kwa hivyo umuhimu wa wa kuanzisha *hatchery* ni muhimu sana tutapata order kwa mfano wenzetu wa Maldive wanataka chambo cha samaki tutawazalishia tutawasafirishia. Kwa hivyo sio tu kuwasaidia wafugaji wetu lakini kuna mpango vile vile tunataka tuwaondoe wavuvi wetu katika kutumia vyombo hivi vidogo vidogo wanavyotumia.

Kuna mpango kwenye Serikali kutengeneza kiwanda chetu cha kutengeneza boti ili kuhakikisha watu wetu wanaweza kupata boti, nashukuru nasema wawekezaji wametokea *financing* ipo tupe muda Mheshimiwa tutakuja kukagua utaona hali ya mabadiliko ya wavuvi wetu. Tunachoomba kwa vavuvi ni wazito sana kubadilika kama walivyo wakulima na wavuvi nao wana tatizo la kubadilika wabadilike, wenzetu tumejifunza wa Mauritius wamesema kuwabadilisha wavuvi ilikuwa kazi imebidi wakachukue vijana 1500 chuoni wawa-*train* ndio hao waingie kwenye *Industry* ya uvuvi. Tunaomba na wavuvi wetu nao wabadilike wamepewa vyombo hapa na *MASAP* wameviuza wamepewa nyavu wameziuza, wamepewa boti wameziuza tunahitaji watu waadilifu kile wanachosaidia na Serikali wakitumie vizuri.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na nimshukuru Waziri kwa ufafanuzi mzuri lakini yeye anasema kubadilika wavuvi, wavuvi hawawezi kubadiliki kama akili zetu hazijabadilika. Je, yeye ana mpango gani kasema Mauritius walichukuliwa vijana wakenda

kusomeshwa baadae ndio ikawa chanzo cha kubadilika. Je, kwa hili Zanzibar analichukulia hatua gani kuona kwamba wale wavuvi wetu wanabadilika.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Uvuvi na Mifugo: Mhe. Mwenyekiti, sisi tulichojipanga kwanza kutumia chuo chetu tulichonacho, lakini vile vile kutumia Chuo cha Mbegani na vile vile kuwashajihisha sasa watu waweze kufanya hivyo na Rais alituagiza sisi na Wizara ya Elimu tukae tutengeneze mtaala ambao tutawasaidia watu wetu kupata taaluma ya uvuvi, tunaifanya hiyo kazi ili tupate vijana wengi ambao tunaweza kuwa-*train* kuingia katika sekta ya uvuvi.

Mhe. Mwenyekiti: Nimekuona Mhe. Hassan Khamis Hafidh lakini Mhe. Waziri Katiba na Mhe. Waziri wa Elimu hivi viswahili vya watoto samaki kuitwa vifaranga, maji ya mvua kuvunwa hebu viangalieni kidogo maana yake haviko *palatable*. Mhe. Hassan Khamis Hafidh.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii, kwanza nataka kujua kwa nini ukiangalia mapato ya bahati kuu yalikuwa *over one billion* ……

Mhe. Mwenyekiti: Kifungu gani hicho.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Hapa hapa.

Mhe. Mwenyekiti: Vipo vingi unakusudia hichi cha mwisho sio chini kuimarisha uvuvi wa bahari kuu haya twende.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Kwa nini Mheshimiwa mapato ya bahari kuu yameshuka Why? Lakini Mheshimiwa kuna kampuni moja ilikuja kutaka kuwekeza kuhusu uvuvi wa bahari kuu hapa Zanzibar nilishiriki na tulifanya utafiti tukenda katika madiko mbali mbali na tuliyagundua mambo matatu makuu yanawakwaza wavuvi wetu Zanzibar.

Kwanza ulikuwa ni utaalam, pili ilikuwa dhana na tatu ilikuwa uwezo ndio maana mvuvi wetu Mhe. Mwenyekiti, anakwenda kuvua lakini hajui kama tapata au hapati tofauti na nchi nyengine. Mvuvi anakwenda kuvua akijua hasa sijui nitawatia wapi hawa samaki, kwa sababu anajua, atawapata nchi nyingi tu mfano Norway nchi nyingi zilizoendelea hata ukiangalia …….

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa nenda kwenye hoja.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Hoja yangu Mheshimiwa namjua Mheshimiwa ni mtaalam wa kusema lini ataweza kuwawezesha wavuvi wetu waweze kwenda kuvua au wana mpango gani na ana *program* gani ya kuwawezesha wavuvi wetu hapa Zanzibar, hasa ukizingatia nchi yetu imezungukwa na bahari, utajiri wetu uko kwenye bahari waweze kwenda kuvua wakiwa na uhakika wa kupata ili umasikini Zanzibar uweze kupungua.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Uvuvi na Mifugo: Mhe. Mwenyekiti, kwanza suala la mapato ya bahari kuu kama nafahamu sheria inasimamiwa pamoja na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na katika kubadilisha sheria mara hii kanuni hasa imesema meli zote ambazo zinavua bahari kuu lazima ama walete samaki kwenye bandari zetu, Dar es Salaam, Tanga, Mtwara au Zanzibar waweze kusafirisha samaki wao. Kwa hivyo wengi wenye meli wakaona hili sharti hawawezi kulitekeleza kwa hivyo idadi ya meli ambazo tumezirejesha mara hii ilikua kama 26 kulinganisha na mia zaidi tulizirudisha wakati ule, na mapato yetu makubwa yalitokana na leseni na maamuzi haya ya Serikali yana sababu mbili.

Kwanza tunataka hii sekta ya uvuvi wa bahari kuu sasa ianze kumilikiwa na raia, kwa hivyo anayetaka kuvua aje aingie ubia na Serikali kupitia kampuni yetu au akubali anachokivua kule anakipitishia bandarini kwetu kwa kile anachosafirisha nje na ile *bycatch* inayopatikana basi inauzwa ndani ya nchi yetu hayo ndio mambo yaliyotokea. Kwa hivyo wengine wamekubali wengine wamekataa wameondoka lakini kikubwa tulichokifanya ni kuanzisha kampuni yetu sisi wenyewe ili sasa tuende tukavue sisi wenyewe, wavuvi wetu wote wanaovua hawajafika hata *nautical mile* 4 kwenda kuvua wakati tuna eneo la *nautical miles* 12 kwenda kuvua, tunataka tuwapatie zana na *Training* ya kutosha ili waweze kwenda kuvua katika maeneo hayo.

Alichokisema kwamba kweli nchi nyengine wanapata samaki ni kile nilichokieleza mwanzo kwamba siku hizi wanatumia hizi *hatching* wanaziweka kule watu ni rahisi kwenda kukuta samaki wakavua kuliko ule utaratibu wa zamani. Kwa hivyo hilo tunalifanya Mheshimiwa tutakukaribisha wawekezaji wamekuja kuingia nataka niwashukuru baadhi ya Waheshimiwa Wawakilishi hapa wameleta watu makampuni ambayo yataweza kufanikisha.

Lakini nataka nichukue nafasi hii nimshukuru sana Makamu wa Rais katika ziara zake zote alizofanya amejitahidi kutuletea wawekezaji ambao wanaweza kuwekeza katika sekta ya uvuvi na naamini hilo litasaidia sana.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri lakini mimi nimezungumzia wananchi wetu wa Zanzibar ambao ndio kazi yao uvuvi sijazungumzia muwekezaji najua muwekezaji tajiri atafaidika yeye tu, wananchi wetu wa Zanzibar atawawezesha lini waweze kuvua na kuwa na uhakika wanachokipata.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Uvuvi na Mifugo: Mhe. Mwenyekiti, nimeeleza sana hata akisoma kwenye kitabu chetu wavuvi wangapi tumewapa *training* mara hii na nimeeleza *program* zetu za *MASAP* na kadhalika ni boti ngapi na nyavu ngapi tumewapa watu wetu, cha msingi ninachokuomba watu wetu wengi tunawapa zana tunawapa na *training* lakini hawafuati yale masharti, wanapewa dhana na kila kitu halafu wanakwenda kufanya uvuvi haramu kwa zana zile ambazo tumewapa. Tumewapa boti wengine wameziuza ndio maana nikasema ni pande mbili, juhudi za Serikali zinazochukuliwa lakini na yule anayesaidiwa nae lazima ajisaidie na hiyo kazi tunaifanya. Ndio maana tukasema vile vile ni vizuri sasa na Rais ametuagiza kabisa hizi boti wanazozitumia hizi pengine haziwasaidii. Tuwatafutie utaratibu wa kuwapatia boti za kisasa ambazo watafika huko kwenye bahari kuu.

Suala la wawekezaji Mheshimiwa Mwenyekiti, sharti tuliloweka la wawekezaji lazima washirikiane na raia wetu zamani walikuwa wanakwenda tu wanavua wanaondoka sasa nasema ni njia ya kuwawezesha na kuwaendeleza watu wetu kwa hivyo tujawaacha mkono watu wetu kabisa, tunataka waendelezwe lakini tukubali wenzetu wana sayansi na teknolojia tunataka sayansi na teknolojia ije hapa ili iweze kuwasaidia watu wetu.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti nashkuru nimefahamu Mhe. Waziri lakini nataka tuendelee lakini nataka akumbuke kwamba wavuvi wa Zanzibar ni maskini na jukumu hili kapewa yeye, kwamba wavuvi wa Zanzibar waweze kuvua na uhakika na waweze kupata na kama unavyojua nchi yetu ni Kisiwa na tumezungukwa na bahari sasa hii ya wawekezaji nina wasi wasi nayo, anaweza kuja kupata tajiri sisi akatubakisha masikini natumeona katika mambo mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa nadhani kajibu vizuri. Mhe. Omar Seif Abeid.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi mimi niko kwenye kifungu:

HL01040101 Kuimarisha huduma za ugani kwa Wafugaji wa samaki na wakulima wa mwani.

Mhe. Mwenyekiti: Naam tuendelee.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mheshimiwa mimi nikitaka nijuwe kidogo pamoja na kwamba Mhe. Suleiman kanifilisi kwenye ufugaji wa samaki lakini niko kote kuwili pamoja na mwani. Serikali ilikuwa na mpango mzuri na wananchi kwa ajili ya kilimo cha mwani lakini soko la mwani ambalo wananchi wetu wengi wa Zanzibar, hasa wavuvi walikuwa wanategemea kupata kipato lakini bei ya mwani sasa hivi inaendelea kuwa chini, sasa nilitaka nijue tu Serikali imefanya mpango gani wa kuwasaidia kutafuta soko la mwani ili hawa wakulima wa mwani waweze kunufaika na kile kilimo cha mwani. Kwa sababu ukiangalia kazi ya kulima mwani ni kubwa na nzito na kipato kidogo, lakini pia tukirudi kwenye ufugaji wa samaki nitaka nijue,

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa wewe ume-quote cha kwanza ambacho kinahusiana.,

Mhe. Omar Seif Abeid: Kinagusa na ufugaji wa samaki.

Mhe. Mwenyekiti: Ehee endelea.

Mhe. Omar Seif Abeid: Lakini pia nilitaka kujua huu ufugaji wa samaki kwa sababu Serikali ina lengo ya kuzalisha vifaranga wengi, jambo la faraja kwamba kuna wakulima wafugaji wa samaki watanufaika. Lakini nilitaka nijue Serikali ina mpango gani wa kuwashajiisha hawa wafugaji wa samaki kuunda vikundi vya ushirika ambavyo vitakuwa ni wepesi kwao Serikali kuvisaidia kulikoni kusaidia mkulima mmoja mmoja ambao kama wataweka ushirika itakuwa ni manufaa zaidi na itatoa ajira zaidi, kwa wakulima wetu wafugaji wetu. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Kilimo Malia asili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza nianze lile la mwani na bei ya mwani Mhe. Mwenyekiti, kama umefuatilia maelezo niliyoyatoa nilisema kwamba soko la mwani kwa maana ya kuuza mwani sio zuri hatai juhudi tulioichukua na Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko kuhakikisha kabisa tumezungumza na UNIDO na kadhalika tuanzishe viwanda vyetu sisi wenyewe vya ku-*process* mwani, hiyo ndio itakuwa *solution* ya soko la mwani. Kwa hivyo nategemea masoko ya nje haya ambapo wenzako wanazalisha tani 1,000,000 wewe unazalisha tani 16,000 mara nyingi ushindani wake sio rahisi sana. Kwa hivyo nasema kubwa ni kuwasaidia kufanya hiyo kazi nataka niwashukuru sana wazalishaji wa mwani wameanza na viwanda vidogo vidogo sasa hivi wanatengeneza sabuni

wanatengeneza vitu mbali mbali lakini nasema nakubaliana na wewe kabisa kuna haja ya kushughulikia soko la mwani kwa maana ya ku-*process* mwani ili tupate bidhaa zenye thamani zaidi kuliko hizi wanaozalisha.

Kuhusu suala la ugani Mhe. Mwenyekiti, sisi tumejipanga tunatoa taaluma na wataalamu wako tuna programu zetu kama ulisoma katika bajeti yetu, tumeweka kabisa fedha za kutosha za kutoa taalamu kwa ajili ya ugani, wa uvuvi wa ufugaji na kadhalika.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. nashukuru kwa majibu yake mazuri lakini nilitoa wazo la kuwashajiisha kuunda vikundi vya ushirika ili itakapofika ule muda wa kutoa vile vifaranga wale tayari wameshakuwa kwenye vikundi vya ushirika ndo nilizungumza hilo miye, lakini sina pingamizi naomba tuendelee.

Mhe. Waziri wa Kilimo Mali asili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti nilisema tuna vikundi vya ushirika 127 ambavyo tumevitembea, lakini vile vile Idara yetu ya Ushirika chini ya Wizara ya Uwezeshaji kuna vikundi zaidi ya 3,000 ambavyo vile vile, navyo ni wazalishaji ndo maana nikatoa wito kwa waheshimiwa wawakilishi katika majimbo yenu muangalie namna gani mnaweza mkaimarisha vikundi vya ushirika, mkaviingiza katika programu hii ya kusaidia inapatikana kutokana Benki ya Kilimo ili iweze kusaidia hawa watu wetu. Kwa hivyo Serikali kweli haisaidii mtu mmoja mmoja tunasaidia vikundi vya ushirika lakini ndio maana tunahimiza watu waweze kujiandikisha katika Ushirika na Vikundi vya Ushirika hivyo.

Cha kufurahisha Mhe. Mwenyekiti, vikundi vya ushirika vilivyokuwepo Zanzibar sasa hivi vina mtaji wa shilingi bilioni 11 tunafikiria utaratibu gani wa kuweza kuanzisha Benki yao sasa, kwa hivyo ni watu ambao wamejipanga vizuri hivyo wanataka kusaidiwa ili na sisi wenyewe tuwasaidie. Tumieni hiyo fursa wananchi nyinyi waheshimiwa wajumbe kuweza kuanzisha vikundi vyenu ambavyo mtaweza kusaidia katika majimbo yetu. *(Makofi)*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nipo hapo hapo kwenye kifungu hicho kama alivyosema Mhe. Hassan Khamis Hafidh chini yake

HL01040101 Kuimarisha huduma za ugani kwa Wafugaji wa samaki na wakulima wa mwani.

Kwanza kabla ya kusahau nimpongeze sana ndugu yangu,

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. kifungu kipi kwanza ngojea. Kuimarisha uvuvi wa bahari kuu au unaongelea nini.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ndo hicho hicho Kuimarisha ufugaji wa mazao baharini

HL01040101 Kuimarisha huduma za ugani kwa Wafugaji wa samaki na wakulima wa mwani

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Bahati miye nafikiri umeshakiona Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Endelea endelea

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante nakushukuru Mhe. Mwenyekiti kwanza nichukuwe fursa hii kumpongeza sana Ndugu Mussa Aboud Jumbe kwa umakini wake katika sekta hii kwa kipindi kirefu, Mheshimiwa, hili suala si la juzi wala jana, ni la muda mrefu na bahati mbaya au bahati nzuri Mwenyenzi Mungu kanijaalia jimboni kwangu nimezungukwa na bahari na ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi ukaiona utaona watu wanavyohaghaika na mwani. Wakulima wa zao la mwani wakivuna zao hilo katika kijiji cha Kojani Wilaya ya Wete Mkoani Kaskazini Pemba.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. nenda kwenye hoja yako.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Waziri alipokuwa akijibu hapa anasema ananunua mpunga 1,200 anauzia wananchi 200 wajua mdomo kusema rahisi vitendo ni kazi, mwaka wa saba yeye mwenyewe keshafanya kuwaita wakulimawa mwani Pwani Mchangani na akawapa matumaini ya kutosha ikiwemo sijui kuna vihori vya mwani, kuna nini.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa yaani kifungu ulichotaja wewe sio cha mwani, mwani uko juu tushamaliza.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kuimarisha huduma za ugani kwa Wafugaji wa samaki na wakulima wa mwani, mwani unalimwa Mhe. Spika, kiangalieni vizuri

Mhe. Mwenyekiti: HL01040101

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Naam angalia vizuri chini yake hapo.

Mhe. Mwenyekiti: HL01040102 kwa hiyo au vipi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Apo apo 01. Ukataka chini utapata matatu hapo hapo vifungu vyote vinakubalika hoja inaingia.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. tumeshamaliza hapa watu watatu tayari.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Uliniahidi Mhe. Mwenyekiti, na Ramadhani hii na ukanambia niinuke.

Mhe. Mwenyekiti: Ndio ahadi inakwenda na niliwaita watu watano Mheshimiwa si matarajio yangu kwamba watu wote watakichangia jambo hili.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Nilochangia ni mimi peke yangu suala mwani *specific* peke yangu hakuna aliyegusa mwani.

Mhe. Mwenyekiti: Omar Seif kagusia mwani.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kagusa watoto wa baharini

Mhe. Mwenyekiti: Haya malizia basi njoo endelea.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Inaonekana kama Mhe. Mwenyekiti hapa sikupata haki kwa hivyo huko tunakokwenda utaniweka chini Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Endelea basi kuongea hilo suala lako la mwani.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti waziri keshafanya vikao vingi tu ikawa Pwani Mchangani kuwaita watu na akawapa matumaini leo mchanga wameweza kuudhibiti, kwa nini wasiweze kudhibiti na haya ya muda mrefu au ndio msemo uliosema “Shamba likiwa la bangi la mkulima likawala dhahabu la Serikali” kwa nini hasa muda wa miaka 7, 8, bajeti ile tulipiga kelele hapa hapa suala hili, wakulima wanateseka sana mwani wazee wetu. Na sisi bahati kubwa tuliyoipata tumezungukwa na bahari, ikawa ananunua mpunga shilingi 1,200 kilo anauza 200 kuna sababu gani asinunue na huu mwani, hili suala ni muda mrefu Serikali huwa inatoa kauli nzuri lakini utendaji unakuwa haupo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nishakusikia Mheshimiwa. Mhe. Waziri majibu mwani.

Mhe. Waziri wa Kilimo Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, kwanza niseme tu suala la ugani si *process* si kitu ambacho kinamalizika siku moja, mpaka dunia itakwisha ugani utaendelea jamii na jamii kwa *level* mbali mbali. Kwa hivyo ugani ni taaluma na taaluma haina mwisho inaendelea tu leo huyu unamfundisha atumie kihori kidogo, kesho utamfundisha kutumia meli kubwa na kesho unamfundisha kwenda bahari kuu na kadhalika. Na mwani ni hivyo hivyo *procces* zake ni hizi hizi za kufundishana kwa hivyo suala la taaluma litaendelea kuwepo kila wakati kwa hivyo sifikirii kama litaisha. Kama sisi wawakilishi hapa tunapata semina kila wakati hazishi tukiingia leo kesho kesho kutwa na semina ni taaluma tu. Kwa hivyo taaluma itaendelea lakini Mhe. Mwenyekiti, lazima tukubali kwamba tumejitahidi sana katika hili jambo.

Nakumbuka kama Rais aliahidi kutoa vihori na akatoa vihori akawapa wakulima, sasa hivi tumewapa tai tai zile kamba za kufungia, kesho kutwa tunakwenda Pemba kuwasaidia vifaa vya kufungia mwani, kwa hivyo tunafanya kazi hii na tunaendelea nao sana watu wa mwani. Lakini nasema ufumbuzi wa tatizo la bei ya mwani ni kuwa na kiwanda chetu sisi wenyewe cha ku-*process* mwani sio soko la nje, soko la nje hatuwezi kushindana nalo. Philippines wanazalisha mwani tani milioni 1,000,000, Indonesia milioni 1,200,000, sisi tunazalisha tani 16,000 elfu wakitaka kuangusha soko wanaliangusha tu. Kwa hilo huwezi kutegemea kama wewe utaingia kwenye soko njia peke yake ni kuzalisha *by product* za mwani.

Ndio maana vikundi tulivyonavyo sasa hivi tumevipatia machine ndogo ndogo, angalau wanatoa sabuni, wanatoa keki wanatengeneza vitu vingi na tunakuombeni tarehe 28 Agosti, tuna siku ya mwani tutawaalika mkaangalie, tulifanya mwaka jana, tunafanya siku ya mwani mkaangalie *development* zilizotokea katika kipindi hichi juu ya mwani. Nakuhakikishia Mhe. Mwenyekiti, suala la msingi ni kupatikana kiwanda tunalifanyia kazi mimi na Mhe. Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko mimi naamini kiwanda kitapatikana tatizo la bei ya soko ya mwani litakuwa limeondoka.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti nashukuru pamoja na majibu ya Mhe. Waziri hili ni agizo la Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alitoa wizara nne zikae, ikiwemo Wizara ya Biashara, Fedha, Kilimo lakini mwaka wa ngapi na wananchi huku wanazidi kuteseka na mwani huu leo mchanga umetafutiwa *fomular* maalum sababu gani hii.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. baki kwenye mwani tafadhali baki huko kwenye mchanga usende.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Serikali inanunua mbegu ya mpunga shilingi 1,200 na inawauzia wananchi shilingi 200 Serikali haiogopi kula hasara kwa wananchi wake ndio majibu ya Serikali humu na *hansard* tunazo, sasa atueleze tu ajalize japo shilingi 300 wananchi waneemeke sikukuu hii maisha magumu, najua uongozi kazi dhamana kwa wananchi.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, naomba ni kidogo na mimi nichangie kuhusu suala la mwani kama alivyoeleza Mhe. Waziri wa Kilimo kwamba suala la mwani Serikali imechukua juhudi ya hali ya juu kuona kwamba hili zao la mwani linaendelea na wakulima na wananchi wanafaidika. Pia iliundwa kamati ya Mawaziri ambayo kamati hiyo ilikuwa inaongozwa na Mhe. Makamu wa Rais, Kamati ya Mawaziri na Kamati ya Watendaji, kubwa ambalo linalisumbua hili zao la mwani ni kwamba huko nje kuna wanunuzi kidogo sana na hawa ndio wameli-*control* hili soko kwa hivyo jambo ambalo tumeliona, kwamba baada ya kutegemea soko la nje ni vizuri kutafuta njia kuweza kutumia mwani na kusarifu mwani hapa hapa nchini na kuuza mazao au matunda au bidhaa inayotokana na mwani.

Na hiyo Mhe. Mwenyekiti, inatokana na sera yetu sasa hivi ya kujenga mnyororo wa thamani, kwa hivyo ndani ya Bajeti ambayo nakuja kuizungumza mimi nitakuja kuisoma sasa hivi, tumepatiwa fedha kuanzisha kiwanda cha kutengeneza, kusarifu mwani kwa hiyo ningemuona Mhe. Mwakilishi akasubiri wakati nitakapokuja kuisoma hotuba yangu tutaeleza nini tunataka kukufanya kuhusu hili zao la mwani. Ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mheshimiwa bado hujaridhika Mhe. Jaku haya.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Nimshukuru Mhe. Waziri kwa jibu lake lakini ningelimuomba akaangalia mahali gani pa kujenga hicho kiwanda cha mwani *center* ilipo tuendelee.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sana mimi nilizungumza suala *deep sea* nilimuuliza Mhe. Waziri aje anijibu ni meli ngapi, ambazo zipo *off shore* kwenye *deep sea* zinavua na na bei ya leseni ya meli zile wanalipa vipi kwenye kila meli leseni ya kuvua *deep sea* na nikasema vile vile, kwenye uvuvi wao katika kodi wanakusanya kwa samaki mmoja mmoja kila samaki wana-*charge* kodi au kwa tani wana-*charge* kodi naomba jibu.

Mhe. Waziri wa Kilimo Mali asili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti kwa bahati mbaya sana katika Sheria zetu *deep sea* hatukushanyi kodi tunachokushanya ni leseni, na leseni zimegawika katika mafungu kama matatu la kwanza kuna mtu anakuja kuvua kwa muda miezi mmoja, mitatu analipa dola 18,000 kwa leseni anakuja kuvua kwa mwaka mmoja analipa dola 36,000 kwa leseni moja anayochukua hayo ndio mapato hasa tunayopata. Wakati Mheshimiwa namjibu Mhe. Omar nilisema meli ambazo zipo sasa hivi zinavua ni meli 26. Zilizokuwepo kwenye *deep sea* na zenyewe zinavua zinapata leseni hizo halafu wanaendelea hata mapato yetu mara hii yameteremka kutoka milioni 3,000,000 dola tumefika dola 600,000 kwa sababu meli ambazo zimekuja kuchukua leseni zilikuwa ni chache sasa. Huu ndio utaratibu uliopo Mheshimiwa wa *deep sea*.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri hana haja kuinuka tena natoa ushauri wangu kodi mnayoikusanya nahisi itakuwa Serikali haipati mapato ya kutosha ningeshauri kwamba mwende kwenye mfumo wa kukusanya kodi kwa samaki kwa samaki per *peace* au per *tone*, kwa samaki wa jodari na tuna bei mbaya sana nje wanauzwa. Serikali inakosa mapato dolla 18,000, 36,000 ni fedha ndogo sana kwa meli ambayo kubwa inayovua samaki kwa *deep sea*.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante ushauri.

Mhe. Waziri wa Kilimo Mali asili, Mifugo na Uvuvi: Napokea ushauri wake Mhe. Mwenyekiti ila kodi hazitozwi kwa samaki kwa samaki zinatozwa kwa *tone* kwa hizo nchi ambazo zinatoa, lakini nasema tutalipokea na tutalifanyia kazi, halafu tutamjibu.

PL0104 Programu kuu ya Maendeleo ya Uvuvi
13,698,676

PL0105

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hidaya, nawataja kabisa halafu mtakwenda kwa utaratibu huu Mhe. Maryam Thani Juma, Mhe. Suleiman Sarahan Saidi hujanyanyuka hata mara moja, Mhe. Machano, Mhe. Abdalla Maulidi Diwani, Diaspora, Suleiman.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Mwenyekiti wakati nilipokuwa nikichangia nilimtaka Mhe. Waziri aje atufafanunulie hivi vikundi vya vijana 127 vya vijana wa wilaya zote za Zanzibar. Nikamtaka sana Mhe. Waziri aje

atufafanulie hivi vikundi vya vijana katika hizi wilaya atufafanulie wilaya ya Kaskazini 'A' vikundi vingapi, wilaya ya Kaskazini 'B' hajatwambia na sisi tunapata changamoto kubwa huko kwa vijana tunaulizwa na hatujui la kujibu. Kwa hivyo ningemuomba sana Mhe. Waziri atufafanulie hivi vikundi vijana vikoje katika hizi wilaya wamechukua vipi ili tujuwe majibu ya kuwajibu. Lakini pia Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikichangia nilimuomba sana Mhe. Waziri kwenye...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hidaya tutajie kifungu hasa ambacho unakuwa umekilenga sio hotuba yako ulivyokuwa umejibiwa kwa sababu hapa ni mafungu ya fedha ndio tunashulika nayo.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Sawa Mhe. Mwenyekiti hilo la mwanzo la vikundi ni kikundi

HL01050202 Utatuzi wa Changamoto Kiuchumi na Kijamii. Lakini hii ya sasa hivi naizungumzia kifungu HL01050205 Kuimarisha Miundo Mbinu ya Masoko na Mazao ya Kilimo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. kwa sababu nimetaja watu wengi utaongelea jambo moja tu kwa hivyo hilo la kikundi ambalo umezungumza kwenye hiyo HL01050203 ndio iwe ya msingi kwa hivyo tumpe nafasi Mhe. Waziri ajibu usiende kwenye chengine tena.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Lakini yote yanayohusiana na hapa hapa Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Yanahusiana na

Mhe. Hidaya Ali Makame: Yanahusiana na kifungu hichi hichi.

Mhe. Mwenyekiti: Ndio atakujibu yeye Waziri kwa hicho hicho kimoja ulichouliza.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Uendeshaji wa Utaratibu wa Wizara ya Kilimo.

Mhe. Mwenyekiti: Nishakufahamu kwamba ndani ya hili fungu kuu wewe una vifungu viwili unataka kuvihoji,

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ndio

Mhe. Mwenyekiti: Sasa hoji hicho kimoja kwanza halafu umsikilize.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Kilimo Mali asili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, wakati nikiijibu hoja nilisema kwamba vikundi ni 127, 68 Unguja na 57 Pemba *press down* ya kila Wilaya nitamletea kwa maandishi.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante ndio nafikiri iko sawa. Mhe. Hidaya.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Mhe. Mwenyekiti, ndio niendelee hicho kifungu cha pili au nimalizie kwa hapa naomba tuendelee, lakini majibu yawe ni mazuri tu. Mhe. Mwenyekiti ili tujue nini tunajibu.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Maryam Thani Juma.

Mhe. Maryam Thani Juma: Ahsante Mhe. Mwenyekiti katika mchango wangu wa maandishi nilizungumzia kuhusu suala la shamba la kilimo la Vikutani, nilimtaka Mhe. Waziri anieleze, kwa sababu Shamba hili la kilimo ni shamba ambalo linazalisha nazi na machungwa kwa wingi pamoja na chenza, lakini mazao haya yanaibiwa sana. Nilitaka Mhe. Waziri anijuilishe Wizara ina mpango gani ya kuweka walinzi katika shamba hili la vikutani.

Vile vile nilizungumzia kuhusu sehemu ya kukaa wafanyakazi hawa.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mariyam Thani, kwanza tutajie kifungu gani, lakini kwenye mchango wako wa maandishi, kwa sababu kikawaida mnapozungumza humu lazima Spika ajue unakusudia kuzuia kifungu. Sasa kusudio lako hilo sidhani kama kwenye mchango wako wa maandishi lilikuwepo.

Mhe. Maryam Thani Juma: Kipo kifungu SL010503 Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Kilimo, Maliasili, Mifugo, Wizara Pemba.

Mhe. Mwenyekiti: Eheee.

Mhe. Mariyam Thani Juma: Suala la pili ni kwamba nilisema wafanyakazi wale wa shamba hili hawana sehemu ya kukaa katika shamba lile na wanapata tabu, hawana sehemu ya kujisaidia wala ya kumpumzikia. Nimeiomba Wizara na kutaka kujua kwamba wana mpango gani ya kuwajengea kiofisi kidogo wafanyakazi wa shamba hili la Kikutani.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvvi: Mhe. Mwenyekiti, nataka nimuahidi Mhe. Mwakilishi tutashirikiana kwenda pale kuangalia hali hiyo halafu tutafanya *assessment* tuone namna gani tunaweza kusaidia.

Mhe. Suleiman Sarahani: Nashukuru Mhe. Mwenyekiti, na mimi nasimama kwenye fungu SLN010503 Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Kilimo, Maliasili, Mifugo Pemba. Mimi kwanza nimpongeze Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini nilikuwa nataka muelekeo kidogo wa bonde la Tibirinzi kuhusu wenyewe watu waliokuwa wanamiliki pamoja na utafiti wake. Lakini pia na Kiwanda cha Matrekta ametukaribia hapa lakini kile cha Pemba hajatukaribisha sijui ana malengo gani.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvvi: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka niseme nawakaribisha vile vile kwenye Kiwanda cha Matrekta cha Pemba na chenyewe tumeshakifanyiwa ukarabati kwa kiasi fulani na matreketa utayakuta pale yamekaa tuliyoyafanyia *service* tayari, karibuni mkaangalie hatua ambazo tumechukua hatujabagua hata kidogo.

Kuhusu shamba la Tibirinzi amenambia Mheshimiwa kwamba kuna tatizo kubwa sana la maji chumvi katika shamba lile na akatushauri basi ni vizuri tukaligeuza liwe la kufuga samaki. Nimuahidi tumpatia wataalamu wakaangalie halafu wataalamu watatushauri kwamba je, tuligeuze kuwa la kufugia samaki au tufanyaje. Hiyo ni kazi ya kitaalamu tutaufuata ushauri wa kitaalamu na tutalifanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Machano Othmani Said.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Mwenyekiti, mimi nazungumzia fungu hili katika sehemu ya Utawala wa Wizara. Wala sitaki kuzuia fungu nataka ufafanuzi tu kwamba katika maelezo yangu niliyochangia nilizungumzia mradi wa barabara za MIVA barabara ambazo zilijengwa kupitia Wizara ya Kilimo. Barabara hizi zinaonekana hazikuwa za kiwango kile ambacho kinakielewa kama Wizara ya Mawasiliano. Nyingi yao zimeharibika kwa mvua za masika na zinahitaji matengenezo na sina uhakika kama Wizara ya Mawasiliano imeshakabidhiwa au bado.

Je, Wizara ya Kilimo ina mpango gani wa kuzifanyia matengenezo barabara hizi baada ya mvua ya masika na kuweka macalvat ili wananchi wapate kufikia lile lengo linalokusudiwa na serikali kuwapelekea miundombinu katika maeneo ya Kilimo kama Mwakaje, Mwachealale, Bumbwisudi na kadhalika. Barabara zimeharibika kwa hivyo nilikuwa nataka kusikia kauli ya Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvvi: Nimshukuru sana Mheshimiwa kwa kuulizia suala hili la barabara ya kijijini ili kusaidia kupata mazao yaweze kutoka. Bahati nzuri programu ile imemalizika kwa upande wetu sisi. Tutazungumza na wenzetu kuwakabidhi pamoja na serikali Wizara ya Tawala za Mikoa ili tuone namna gani watawaweza kusaidia zile barabara. Kwa bahati mbaya ni barabara za changarawe na kama mvua ikitokea zinaharibika kwa kiwango kikubwa sana. Lakini tuwashukuru wenzetu waliotusaidia pale ambapo jua lilikuwa zuri na barabara zilikuwa nzuri. Hatimaye zimeharibika sasa tutashirikiana na wenzetu kwa sababu zimeshatoka kwetu ili tukae namna gani tujue wataweza kusaidia.

Tunawaomba waliotusaidia kama ni vizuri wakaangalie tena utaratibu wa kuhakikisha kwamba tunajenga barabara za lami badala ya hizi za changarawe, kwa sababu hazichukui muda mrefu kuharibika. Tuendelea na mazungumzo nao lakini kwa sasa hizi ambazo tumeshazikabidhi tutashirikiana na Wizara tuone namna gani tunaweza kuzikarabati ili ziweze kupitika vizuri. Tunakubaliana na wazo lako Mheshimiwa.

Mhe. Machano Othaman Said: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake kwa hivyo hiyo ni ahadi kwamba yeye na Waziri wa Tawala watashirikiana kuhakikisha kwamba barabara zile zinarudia katika hali inayokusudiwa. Baada ya hayo naomba tuendelee.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, mimi nakamata kifungu cha LH01050104 Kusimamia Mali za Wizara na Manunuzi ya Mujibu wa Sheria. Nilipochangia nilizungumza kadhia nzima ya gari ya SMZ namba 6927 ambalo lile gari alihama nalo Mteuzi wa Rais kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyengine lile gari likamfuata. Watakati tunakwenda kule kukagua katika *asset register* la Wizara ya Kilimo lile gari lipo pale, lakini uhalisia lile gari halipo. Katika majibu yako sijalipata jibu, naomba kwanza nipe jibu halafu tujue kinachoendelea.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa hichi kitengo naona hata pesa hakina, yaani hakijatengewa kwa mwaka huu.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Katika usimamizi wa mali, hii ni mali au gari si mali?

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvvi: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nikubaliane na Mheshimiwa kwamba hili gari lilikuwa la Wizara ya

Kilimo na Mkurugenzi aliyekuwa wakati ule akateuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais wakate ule Wizara ni kweli hakukuwa na huduma zozote. Gari nyingi zilichukuliwa katika sehemu mbali mbali kuweza kuwahudumia Wizara ile. Ilipoamalizika shughuli ile gari zote zimerudi Ikulu haikurudi tena Wizarani kwetu.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kwamba yeye amekuwa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara alikuwa akitumia lakini gari ilibaki *State House*. Utaratibu wote mwengine tulibakisha *State House* baada ya mali zote zile za Makamu wa Kwanza wa Rais, mali zao na vitu vyao vyote vilirudi Ikulu. Kwa upande wetu sisi Wizara hatuna jengine la kusema kwa sababu mali zote ni mali za serikali. Ahsante sana Mwenyekiti.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Sawa ahsante mimi nilichokamata hapa ni kwamba *asset register* buku la mali, ile gari ipo Wizara ya Kilimo, sasa unavyonambia kwamba ipo Ikulu *physically* lakini kwenye buku la mali ipo pale, hapa hatuoni kama kuna mchanganyiko kidogo. Kwa sababu kama mali husika ni lazima ibakie katika sehemu husika unapokwenda kufanya *physically* uione hii hapa na gari yenyewe hii hapa. Lakini leo ananambia gari ile imepelekwa kule halijafutwa ndani ya *asset register* na hizi mali zote za serikali zisajiliwe katika buku moja la kughibiti mali. Sasa je, hili suala liko vipi.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa nafikiri ni kurekebisha hiyo asset register ya serikali kwa sababu bado linaonekana lipo.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvvi: *asset register* ya Serikali ipo Hazina ndiyo inayoshughulikia mambo yote ya mali za serkali. Kwa hivyo tutawasiliana na wenzetu wa Hazina. Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa fursa hii. Nasimama kwa SL010501. Siku ya tarehe 9/6/2016 Mhe. Waziri alisema kwamba kama alivyomwambia Mhe. Rais Nyerere alimwambia kwamba miezi sita kama hatoweza kuwalisha magereza atajiuzulu na pia alitwambia kwamba apewe miaka mitatu kama hatoweza kusitisha mchele usiagizwe hapa atajiuzulu.

Mhe. Mwenyekiti, nimeanza kupata wasi wasi mkubwa, kwenye kitabu chake Mhe. Waziri alichokileta ukurasa wa 5 kinasema hivi:

"Kutoka tani 29,000 kwa mwaka 2015 hadi tani 4,000 mwaka huu".

Wasiwasi wangu uko hapa kutokana na ahadi na maneno ya Mhe. Waziri yaliyokuwa mazuri lakini mbona tunakukwenda *backward instead* ya kwenda *forward* tulizalisha tani 29,000 lakini sasa tumezalisha tani 4,000. Ahadi nzuri Mhe. Waziri kaziweka, haoni tangu tulipompa Wizara tunategemea twende mbele kumbe tunarudi nyuma. Sasa nataka Mhe. Waziri anambie ana mkakati gani wa kunasibisha na maneno yake ya kufanya Zanzibar tuweze kuzalisha mchele wetu wenyewe *at least* asilimia 50 ya tunaoagizia. Maneno yake amesema mazuri.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri alisema kama atapewa zana na zana hapa ndio tumempa, tunampa bilioni 70 hizi, lakini ni lazima aweze kutuhakikishia Wazanzibari mchele ndiyo chakula chetu, asilimia 50 ataweza kuilima kwa miaka hii. Naomba majibu.

Mhe. Mwenyekiti: Hoja yako nadhani ilikuwa ije mwanzo, maana kilimo kimetajwa kweli hapa lakini ukiangalia hivyo vifungu vidogo vyote hivyo hakuna ambacho kinakubaliana.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, tulivyopewa semina tumeambiwa katika Utawala na Uendeshaji unaweza ukakamata mambo haya na mimi nimetumia kipengele hicho tulichopewa semina kunako Utawala.

Mhe. Mwenyekiti: Maendeleo ya kilimo tumepita Mheshimiwa ni nyuma huku. Ukifungua tu ule ukurasa wa juu kabisa ambako tumeshapita nafikiri hoja yako ingekuwa sahihi ikaja pale.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, sibishani na kiti *with do respect of Mr. Speaker sir but*, Utawala na Uendeshaji wa Kazi za Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvu, *what I know* hapa ndipo panapo kila kitu, lakini kiti sibishani nacho kama utaniambia nikae nitakaa.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa hebu angalia hivyo vifungu (h) vyote, wewe umekuja ku-*quote* hii huku SL01050 mara nyingi mnatakiwa msimamie hizi (h) wenzio wote waliokuwa wananyanyuka ana-*quote* kifungu H, L, zile *sub program* ndiyo unapoleta ile hoja yako. Sasa wewe ukiangalia hapa yaani ule ukurasa niliokuonyesha wa nyumba ndiyo hiyo *issue* yako ndio ingekuwa iko *valueable* pahali hapo. Ningependa sana ujibiwe lakini tumeshapita huko Mheshimiwa.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti:

Mhe. Mwenyekiti: Asante Mheshimiwa. Mhe. Suleiman.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Mhe. Mwenyekiti, mimi ningepata majibu wala nisingenyanyuka mara kwa mara.

Mhe. Mwenyekiti, nipo kwenye kuratibu shughuli za uvuvi Pemba HL010503011. Nilipokuwa nikichangia nilizungumza kuhusu kule kule Ndagoni ndani ya jimbo langu wananchi wangu wa Ndagoni asilimia 80 ni wavuvi Mhe. Waziri, lakini wanapata tabu kwenye uuzaji wa mazao yao uvuvi wao yaani samaki, pweza na mambo mengine, wanakwenda kuuza Wesha na wengine hawendi kabisa. Mapato yale ya serikali yaliyotakikana yapatikane pale yanapotea kwa sababu watu wanauziana kiholela holela kwa mikono kwa kuchelea yale masafa ya kwenda Wesha.

Mhe. Mwenyekiti, nikitaka kujua Mhe. Waziri ndani ya bajeti hii wanawafikiriaje wananchi wangu wa Ndagoni kuwajengea soko la kuuzia bidhaa zao zile wanazozipata baharini.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvvi: Katika programu hizi Mhe. Mwenyekiti hatuna soko la Ndagoni lakini tunalo soko la Chake Chake ambalo sio mbali sana na Ndagoni. Naomba atumie soko ambalo tunalijenga Chake Chake pale litawasaidia wavuvi kuuza bidhaa zao kwa urahisi.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana Mhe. Waziri nadhani Ndagoni unakujua, Ndagoni na Wesha ni pua na mdogo lakini ni mbali ni kilomita 9.8. Sasa ukimwambia aende Chake Chake unazidi kumuongezea hayo masafa zaidi. Kwa sababu unanambia wende Chake Chake, kwa hivyo Wesha na Chake Chake na Wesha na Ndagoni hata ukipima kwa kamba Ndagoni na Wesha ni karibu, basi ni bora ungenambia niende Wesha kwa sababu ndiyo kwenye Soko la Samaki, kulikoni kwenda Chake Chake. Ahsante Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvvi: Mhe. Mwenyekiti, suala hapa ni soko na pahala penye soko kubwa ni Chake Chake kuliko hata anakosema. Watu watakaonunua samaki Wesha ni wachache sana. Soko kubwa lipo Chake Chake, ndio ukaona wavuvi wetu wa kojani wanakwenda kuuza samaki Dar-es-Salaam wanafuata soko, yaani soko lile jengo, soko la watu wanaoweza kununua. Kama suala la kujenga jengo, ni suala moja lakini suala

la kupata watu kununua bidhaa zako ni jengine. Tunaona soko la Chake Chake kwa kuanzia waanzie hapo halafu tutaangalia kama tunaweza tukafungua soko kenye eneo lako. Tutashirikiana Mheshimiwa tuone kama tunaweza kufanya hivyo. Pengine tunaweza kuwashirikisha watu kufanya kazi hiyo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Nadir naona umerudi tena vipi, ala unapita njia. Mhe. Hidaya sasa lete ile hoja yako. Mhe. Hidaya vipi tuendelee.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia nilimuomba sana Mhe. Waziri aliangalie sana zao madoriani. Zao hili sasa hivi lina soko kubwa na linauendelevu mkubwa lakini tukiliangalia kwa umakini zaidi zao hili huenda likapotea ndani ya nchi yetu. Kwa sababu midoriani ambayo inazalisha mazao hao kwa sababu hivi imeshakuwa mipevu ina karne kama 200 na zaidi.

Je, kajipanga vipi kuhusu kuatika au kuimarisha kilimo cha zao hili la madoriani, hajanipa majibu Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvvi: Mhe. Mwenyekiti, tumechukua ushauri wake na tutakaa na wataalamu wetu wa utafiti wa kilimo tuone vipi tunaweza tukaliendeleza zao hili kwa kutumia utafiti.

Mhe. Nadir Abdulatif Yussuf: Mhe. Mwenyekiti, lile suala langu la Soko nililete hapa au nisubiri L0132.

Mhe. Mwenyekiti: Tumemaliza lakini suala la soko lilijibiwa wakati wewe humo ndani.

Mhe. Nadir Abdulatif Yussuf: Lilijibiwa?

Mhe. Mwenyekiti: Alikujibu *actually* alipokuwa anakujibu mimi nikakuangalia lakini ulikuwa hupo, ulitoka nje kidogo.

Mhe. Nadir Abdulatif Yussuf: Sasa si vibaya akanipa kidogo.

Mhe. Mwenyekiti: Mimi nafikiri kwa sababu wewe na Mhe. Waziri mnamaelewano mazuri nafikiri unaweza ukamfata baadaye.

Mhe. Nadir Abdulatif Yussuf: Haya hamna tabu, basi tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana tunaendelea.

Kifungu PL0105 Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Kilimo 15,672,561,000

Jumla Kuu ya Matumizi yote

70,605,467,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvvi: Mhe. Spika, kwa kuwa Baraza lako tukufu limepitia bajeti ya Wizara ya Mifugo, Maliasili na Uvuvi kifungu kwa kifungu bila ya mabadiliko sasa naomba Baraza lako liidhinishe. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa hoja imetolewa sasa naomba tena niwahoji wale wanaokubaliana na hoja Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe kabla sijamkaribisha Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, kwanza nitoe shukurani zangu za dhati sana kwa Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, kwa kukamilisha hoja yake. Lakini pia nitoe shukurani zangu kwa serikali kwa ujumla namna ambavyo wameweza kushirikiana na tukaweza kuhitimisha hii hoja. Lakini pia nitoe shukurani zangu za dhati sana kwenu nyinyi Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa michango yetu ambayo imeweza kujenga na kutufikisha hapa tulipofika kuweza kupitisha hoja ya hii Wizara.

Kabla sijamwita Mhe. Waziri wa Biashara naomba nisome wageni waliofika ni wageni wake yeye Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, wageni hao ni:

Makamo Mwenyekiti *Chamber of Commence*

Mwenyekiti wa Body ya ZSTC Maalim Kassim - anyanyuke kama yupo hapo watakuwa
hawajaingia.
Mwenyekiti wa Bodi ya Baraza la Leseni la Zanzibar- Kama yupo naomba anyanyuke,
bado hawajaingia.

Baada ya maelezo hayo sasa naomba kuchukua nafasi hii kumkaribisha Mhe. Waziri wa Biashara Viwanda na Masoko ili sasa awasilishe hoja yake. Mhe. Waziri karibu sana.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2017/208 - Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lakoTukufu sasa likae kama Kamati ya Mapato na Matumizi kwa ajili ya kupokea, kupitia, kuzingatia, kuchangia na hatimae kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa kazi za kawaida na maendeleo kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mhe. Spika, kwanza naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutuwezesha kufika katika Baraza hili tukiwa wazima na afya njema. Aidha naomba kuchukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi pamoja na wajumbe wa Baraza lako tukufu hasa kupitia kamati ya Fedha, Biashara, na Kilimo kwa mashirikiano makubwa na kwa michango na ushauri mliotupatia kwa lengo la kufanikisha utekelezaji wa program za Wizara kwa mwaka wa fedha 2016/2017 na pia kwa ushauri na maelekezo yenu kwa utekelezaji wa program za Wizara kwa mwaka 2017/2018.

Mhe.Spika, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza kwa dhati ya moyo wangu Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dk. Ali Mohamed Shein kwa kuongoza nchi yetu kwa hekima na upendo na kuhakikisha kwamba amani na utulivu wa nchi yetu inaendelea kudumishwa na kuwafanya wananchi kuweza kuendelea kutekeleza shughuli zao za kiuchumi, biashara na uwekezaji. Pia kwa kusimamia mabadiliko ya nchi kwa vitendo hatua kwa hatua. Aidha, napenda kumpongeza pia kwa kuwa mstari wa mbele

katika kuhakikisha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inawatumikia wananchi kwa uadilifu. Kadhalika, nachukua fursa hii kumpongeza Makamu wa Pili wa Rais, Mhe. Balozi Seif Ali Iddi na kumshukuru kwa jitihada zake za dhati anazozichukua za kumsaidia Mhe. Rais wetu wa Zanzibar katika kuwatumikia wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, Aidha, nawashukuru kwa dhati Katibu Mkuu wa Wizara hii, Ndg. Bakar Haji Bakar pamoja na Wakuu wa Taasisi na Mashirika, Wakurugenzi wa Maidara, na wafanyakazi wote wa Wizara kwa juhudi zao kubwa za kuchapa kazi pamoja na mashirikiano makubwa wanayonipatia ambayo yananisaidia kufanya kazi zangu ipasavyo na nawaomba wazidishe mashirikiano yao kwangu ili tuweze kutekeleza majukumu yetu ya kuendeleza uchumi wa nchi yetu kwa mafanikio makubwa zaidi.

Mhe. Spika: Kumradhi Mhe. Waziri naomba nimkaribishe sasa Mhe. Naibu Spika aje kuchukuwa kiti.

(Hapa Mhe. Naibu Spika, alikalia kiti)

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri endelea.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe.Naibu Spika, Naomba kuwapa pole wananchi wote waliopatwa na maafa ya mafuriko na upepo mkali uliyotokea na kusababisha vifo, majeruhi, ulemavu na uharibifu mkubwa wa mali. Namuomba Mwenyezi Mungu awatie nguvu na kuwapa faraja na ahueni haraka ili warejee katika hali njema na tuendelee kujenga uchumi wa nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, katika kutayarisha bajeti hii ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko, nyenzo muhimu zilizozingatiwa ni kama hivi:-

i. Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2020
ii. Mpango wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar (MKUZA)
iii. Maelekezo ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika hotuba yake ya ufunguzi wa Baraza la Wawakilishi mwaka 2016.
iv. Ilani ya Uchanguzi wa CCM mwaka 2015/2020
v. Mpango kazi (*strategic Plan*) wa Wizara
vi. Miongozi ya kisera inayosimamiwa na Wizara
vii. Ukomo wa rasilimali fedha uliowekwa kwa Wizara

Mhe. Naibu Spika, Aidha, katika hatua za awali za utayarishaji wake, mapendekezo ya bajeti hii yamepitia na kuzingatiwa katika hatua na ngazi mbali mbali muhimu na hususan Kamati ya Baraza la Wawakilishi ya Fedha, Biashara na Kilimo. Naomba kutanguliza shukurani zangu za dhati kwa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi inayoongozwa na Mheshimiwa Yussuf Hassan Iddi, Mwakilishi wa Jimbo la Fuoni kwa kushirikiana na Wizara yangu katika kushauri, kukosoa na kutoa mawazo ya kujenga yaliyotusaidia kufanya kazi kwa ufanisi na pia kuchambua mapendekezo ya bajeti ya Wizara, kuikubali na hatimae kuiridhia kuwasilishwa mbele ya Baraza lako Tukufu.

Katika hotuba hii, Mhe.Naibu Spika, nitafanya mapitio kuhusu hali ya maendeleo ya biashara, uwekezaji na Viwanda katika dunia na muelekeo wa sekta hii Afrika ya Mashariki na Tanzania. Pia utekelezaji wa bajeti ya Wizara kwa mwaka 2016/2017, mwenendo wa mashirika na taasisi za Serikali zinazosimamiwa na Wizara yangu, kubainisha changamoto mbali mbali na hatimae kubainisha program za Wizara yangu na sura ya bajeti ya Wizara kwa kipindi cha mwaka 2017/2018.

MWENENDO WA BIASHARA, UWEKEZAJI NA VIWANDA KATIKA DUNIA

Hali ya Uchumi na biashara ulimwenguni:

Mhe. Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2016 mwenendo wa uchumi na biashara duniani uliongezeka kwa asilimia 2.7 kutoka asilimia 2.3 mwaka 2015. Mbali na ukuaji huo wa uchumi wa dunia, taarifa zinaonesha kupungua kwa uwiano baina ya uchumi na biashara kwa asilimia 1.1 kwa mara ya kwanza tokea mwaka 2001. Hali hiyo imeendelea kuathiri biashara duniani ambayo mchango wa sekta hiyo katika uchumi wa dunia yaani *(World Merchandise Trade Percentage of GDP)* ulipungua kutokaasilimia 2.7 mwaka 2015 na kufikia asilimia 1.3 mwaka 2016, ingawa taarifa inaonesha mategemeo ya kukua kwa mwaka 2017 na kufikia 2.4. kama inavyoonekana katika Jadweli Nam. 1 hapo chini.

Jadweli Nam. 1:
MchangowaBiasharakatikaUchumi wa Dunia 2013 – 2016:

Mwaka	**2013**	**2014**	**2015**	**2016**

Asilimia	2.4	2.7	2.6	1.3

Chanzo: Shirika la Biashara la Duniani – WTO, 2017

Mhe. Naibu Spika, usafirishaji wa bidhaa duniani kwa kipindi cha mwaka 2016 ulifikia USD 15,464 bilioni, ambapo ulikuwa ni pungufu kwa asilimia 3.3 ikilinganishwa na usafirishaji uliofanyika mwaka 2015. Katika usafirishaji huo, nchi za Ulaya ziliendelea kuongoza kwa usafirishaji wa bidhaa duniani kwa kusafirisha bidhaa zenye thamani ya USD 5,942 bilioni sawa na asilimia 38.4 ya usafirishaji wote wa bidhaa duniani. Nchi za Asia zilifuatia kwa kusafirisha bidhaa zenye thamani ya USD 5,262 bilioni sawa na asilimia 34 ya usafirishaji wote. Aidha, nchi za Marekani ya Kaskazini zilikuwa katika nafasi ya tatu kwa kusafirisha bidhaa zenye thamani ya USD 2,219 bilioni sawa na asilimia 14.4 ya usafirishaji wote.

Mhe. Naibu Spika, Nchi za Mashariki ya Kati zilisafirisha bidhaa zenye thamani ya USD 766 billioni (5%), Nchi za Marekani ya Kusini zilisafirisha bidhaa zenye thamani ya USD 511 billioni (3.3%). Kwa upande wa nchi za Afrika, zimeendelea kutoa mchango mdogo sana wa usafirishaji wa bidhaa ambapo kwa mwaka 2016 ilisafirisha bidhaa zenye thamani ya USD 346 bilioni za usafirishaji wote sawa na asilimia 2.2.

Mhe. Naibu Spika, uagiziaji wa bidhaa duniani kwa mwaka 2016 ulifikia thamani ya USD 15,799 bilioni, ambapo nchi za Ulaya ziliongoza kwa kuagiza bidhaa zenye thamani ya USD 5,920 bilioni sawa na asilimia 37.5 ya uagiziaji wote duniani. Aidha, katika uagiziaji huo nchi za Asia ziliagiza bidhaa zenye thamani ya USD 4,781 bilioni sawa na asilimia 30.3, nchi za Marekani ya Kaskazini ziliagiza bidhaa zenye thamani ya USD 3,062 bilioni sawa na asilimia 19.4, na nchi za Mashariki yaKati ziliagiza bidhaa zenye thamani ya USD 665 bilioni sawa na asilimia 4.2. Kwa upande wa nchi za Afrika, jumla ya bidhaa zenye thamani ya USD 501 bilioni sawa na asilimia 3.2 ziliagizwa katika kipindi hicho.

Mhe. Naibu Spika, mwenendo huo wa usafirishaji na uagiziajiwa bidhaa duniani katika kipindi cha mwaka 2016 unaonekana katika Jadweli Nam. 2 kama ulivyotolewa na Shirika la Biashara Duniani – WTO. Hali ya bei za mazao ya biashara imeonekana kuanza kuwa nzuri ukilinganisha na miaka ya nyuma.

Jadweli Nam. 2:
UsafirishajinaUagiziajiBidhaaDuniani 2016
(USD bil):

Kanda	Usafirishaji	Asilimia	Uagiziaji	Asilimia
Ulaya	5,942	38.42	5,920	37.47
Asia	5,262	34.03	4,781	30.26
Marekani/ kaskazini	2,219	14.35	3,062	19.38
Masharikiya Kati	766	4.95	665	4.21
JumuiyayaMadola	418	2.70	335	2.12
Marekani/Kusini	511	3.30	535	3.39
Afrika	346	2.24	501	3.17
Jumla	**15,464**	**100**	**15,799**	**100**

IMF/World Bank na WTO.

Mwenendo wa Biashara na Uwekezaji katika Kanda wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki

Mhe. Naibu Spika, hali ya biashara kwa mwaka 2016/2017uliingiliwa na mwenendo wa biashara katika ukanda wa Afrika ya Mashariki kwa vile uagiziaji wa bidhaa unafuata Sera ya Umoja wa Forodha wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki ambao umeweka viwango vya pamoja vya ushuru wa forodha *(Common External Tariffs – CET).*

Mhe. Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2015, nchi za Afrika ya Mashariki zilisafirisha baina yao bidhaa zenye thamani USD 3,207.4 milioni na kuagizia bidhaa zenye thamani ya USD 1,533.1 milioni, na kupelekea kuwepo kwa ziada *(surplus)* ya USD 1,677.5 milioni. Tanzania, Kenya na Uganda zilioneshaziada *(surplus)* katika urari wa biashara, na nchi za Rwanda na Burundi zilikuwa na upungufu *(deficit)* katika urari wa biashara. Hali hiyo ilisababisha kuwepo na utulivu katika upatikanaji wa vyakula muhimu na bei ziliendelea kubakia katika hali iliyoridhisha kwa vile hazikubadilika sana.

Aidha, katika robo ya tatu ya bajeti ya 2016/2017 kutokana na hali ya ukame ulioukumba ukanda wa Afrika ya Mashariki ikiwemo Tanzania Bara, umesababisha uhaba wa vyakula na bei ya vyakula kutoka maeneo hayo kupanda. Matumaini yetu ni kwamba, kutokana na mvua zinazoendelea uzalishaji wa bidhaa hizo utaongezeka na hatimae kurejesha hali ya bei za bidhaa kuwa za wastani.

Hali ya Biashara Zanzibar

Usafirishaji na Uagiziaji wa Bidhaa:

Mhe. Naibu Spika, Hali ya kibiashara kwa ujumla inaonesha kwamba Zanzibar imefanya biashara yenye thamani ya TZS263,322.90 milioni kwa mwaka 2016 ikilinganishwa na biasharaya TZS 199,348.20 milioni mwaka 2015 sawa na ongezeko la asilimia 32.10. Biashara hiyo ilikuwa ni usafirishaji wa bidhaa kwenda nje ya Zanzibar na uagiziaji wa bidhaa kuja Zanzibar. Bidhaa ambazo Zanzibar ilifanya biashara na nchi za nje ni pamoja na karafuu na mwani.

Mhe. Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2016, nchi yetu ilisafirisha nje bidhaa zenye thamani ya TZS 96,234.9 milioni. Kiwango hicho cha usafirishaji ni sawa na ongezeko la asilimia 126.9 kwa kulinganisha na usafirishaji wa bidhaa zenye thamani ya TZS 42,407.0 milioni uliofanyika kipindi cha mwaka 2015. Katika usafirishaji huo, zao la karafuu lilikuwa na thamani ya TZS 64,723 milioni sawa na asilimia 67.30 ya usafirishaji wote.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa uagiziaji bidhaa, nchi yetu iliagiza bidhaa zenye thamani ya TZS. 167,088.0 milioni kwa mwaka 2016 ikilinganishwa na uagiziaji wa TZS. 156,941.1 milioni mwaka 2015. Mwenendo huo umeonesha matumaini ya kuimarika kwa urari wa biashara kwa kupunguza nakisi yake kutoka TZS 114,534.1 milioni hadi TZS 70,853.1 milioni. Jadweli Nam.3 hapa chini linatoa ufafanuzi zaidi.

Jadweli Nam. 3:
Mwenendo wa Biashara Zanzibar (2012 – 2016):
TZS. (Millioni)

O	**2012**	**2013**	**2014**	**2015**	**20**
imports)	271,273.1	208,051.9	279,552.8	156,941.1	16
ji (exports)	67,390.5	87,799.6	133,587.7	42,407.0	96
iashara (Volume of Trade)	338,663.6	295,851.5	413,140.5	199,348.2	26
Biashara (Trade Balance)	**-203,882.5**	**-120,252.2**	**-145,965.0**	**-114,534.1**	**-7**

Chanzo: Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, 2017

Biashara Bainaya Zanzibar na Tanzania Bara *(Inter-state Trade Balance):*

Mhe. Naibu Spika,biashara baina ya Zanzibar na Tanzania Bara inahusisha utoaji wa bidhaa kutoka Zanzibar kwenda Tanzania bara na uingizaji wa bidhaa kutoka Tanzania Bara kuja Zanzibar. Biashara hiyo inahusisha bidhaa za mchele, mbatata, maharage, vitunguu, tungule na mboga mboga nyengine, vitu vya elektroniki, na magari na bidhaa nyingi zengine zinazohitajika hapa nchini.

Mhe. Naibu Spika, kwa kipindi cha mwaka 2016 Zanzibar ilipeleka Tanzania Bara bidhaa zenye thamani ya TZS 84,760.9 milioni, ikilinganishwa na bidhaa zenye thamani ya TZS 401,219.4 milioni zilizopelekwa mwaka 2015. Kiwango hicho cha bidhaa ni zile bidhaa ambazo zinapelekwa katika mfumo ulio rasmi wa kiforodha. Hali hiyo imesababishwa na kupungua upelekaji wa bidhaa za magari na vifaa vyengine vya kielektroniki kutokana na mabadiliko ya usimamiaji wa baadhi ya kodi zikiwemo VAT na kadhalika huko Tanzania Bara na kutokubaliana juu ya usajili wa magari yanayotoka Zanzibar kwenda Tanzania Bara.

Aidha, katika kipindi hicho hicho cha mwaka 2016, Zanzibar iliagizia kutoka Tanzania Bara bidhaa zenye thamani ya TZS138,059.5 milioni ikilinganishwa na uagiziaji wa bidhaa zenye thamani ya TZS 94,650.3 milioni kwa mwaka 2015.

Mhe. Naibu Spika, katika kipindi hiki biashara kutokaZanzibar zimepungua kupelekwa Bara na hivyo kusababisha urari wa biashara kati ya Zanzibar na Tanzania Bara kupungua na nakisi yake kuongezeka ukilinganisha na mwaka 2015 kama inavyoonekana katika Jadweli Nam 4. hapa chini.

Jadweli Nam. 4:
BiasharaBainaya Zanzibar na Tanzania Bara:
TZS. (Milioni)

waka	**2012**	**2013**	**2014**	**2015**	**2016**
ja Zanzibar	98,871.6	82,906.2	81,384.4	94,650.3	134,059.5
enda Tanzania Bara	224,400.5	501,204.2	366,354.2	401,219.4	84,760.9
ariwaBiashara	125,528.9	418,298.0	284,969.8	306,569.1	-49,298.6

Chanzo:OfisiyaMtakwimuMkuuwaSerikali

Hali ya Chakula na Bei katika Soko la Zanzibar
Hali ya Chakula:

Mhe. Naibu Spika, hali ya uwepo wa chakula hapa Zanzibar kwa mwaka 2016 ilikuwa ya kuridhisha. Kwa mujibu wa takwimu za uingizaji chakula zilizopo zinaonesha kwamba jumla ya Tani 88,903.60 za mchele, Tani 24,185.10 za sukari, na tani 39,882 za unga wa ngano zilikuwepo katika kipindi hicho kwa ajili ya matumizi ya soko la ndani, kama inavyoonekana katika Jadweli Nam. 5 hapo chini.

Jadweli Nam 5:
Wastaniwauingizajiwachakulamuhimu
katika soko la Zanzibar 2016 (Tani):

	Mchele	**Sukari**	**UngawaNgano**	**Jumla**
UingizajiwaChakula	88,903.6	24,185.1	39,882	156,970.7
Matumizi	63,108	12,645	19,368	95,121.0
Bakaa	25,795.6	15,540.1	20,514.0	61,849.7

Chanzo: WizarayaBiashara, ViwandanaMasoko, 2016

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa bei za bidhaa muhimukama vile mchele, unga wa ngano pamoja na sukari katika soko la ndani zilikuwa za utulivu ikilinganishwa na bei za bidhaa hizo kwa Tanzania Bara, Kenya na Uganda licha ya kuwepo kwa ongezeko la jumla la bei za bidhaa hizo katika masoko ya dunia. Napenda kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba Serikali inaendelea na utaratibu wa kusimamia bei za bidhaa muhimu (mchele, sukari na unga wa ngano) kwa kuwashirikisha wafanyabiashara wenyewe na kutoa unafuu maalum wa kodi ili wananchi waweze kupata nafuu ya bidhaa zilizo muhimu hasa ukilinganisha na vipato duni walivyonavyo wananchi wengi wa Zanzibar.

Kwa kiasi kikubwa, Mheshimiwa Spika, utaratibu huu umesaidia kuweka nidhamu katika upangaji bei za bidhaa hizo. Aidha, nafuu ya kodi inayotolewa na Serikali kwa bidhaa hizo imesaidia kuzifanya bei za bidhaa hizo kuwa chini na hivyo kuwawezesha wananchi wengi kumudu ununuzi wa bidhaa hizo.

Mhe. Naibu Spika, kwa jumla wastani wa bei za reja reja za bidhaa hizo kwa mwaka 2016 katika masoko ya Zanzibar ni kama zinavyoonekana katika Jadweli Nam 6 hapa chini:

Jadweli Nam 6:
Wastani wa Bei za Reja Reja za Chakula muhimu katika soko la Zanzibar:
(TZS/Kilo)

Bidhaa	Julai - Sept	Okt – Dis	Jan –Machi
Mchele	1,200	1,250	1,250
Sukari	1,800	1,850	1,850
UngaNgano	1,200	1,200	1,200
UngawaSembe	1,200	1,800	2,000

Chanzo: WizarayaBiashara, ViwandanaMasoko, 2016

Mhe. Naibu Spika, kwa kuchunguza hali ya mwenendo wa bei za chakula muhimu katika masoko ya Zanzibar kama inavyoonekana katika Jadweli la hapo juu, itagundulika kuwepo kwa ongezeko la bei ya unga wa sembe kwa kila baada ya miezi mitatu. Hali hiyo imesababishwa na uzalishaji mdogo wa mahindi uliotokana na kukosekana kwa mvua za kutosha huko Tanzania Bara kwa mwaka 2016 na pia tatizo liliibuka baada ya utaratibu wa kodi ya VAT kubadilika jambo ambalo limeongeza kodi ya biashara na kuathiri bei ya unga wa sembe.

HALI YA VIWANDA NA UWEKEZAJI:

Mhe. Naibu Spika, moja ya malengo makubwa ya Serikali ni kujenga uchumi wa viwanda ili kuchochea mageuzi ya uchumi na kuleta maendeleo ya wananchi. Uchumi wa viwanda utasaidia kurasimisha sekta isiyo rasmi, kupunguza uagiziaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi, kuongeza usafirishaji wa bidhaa, kuongeza thamani malighafi za hapa nchini, kuongeza ajira kwa Wazanzibari, kuongeza wigo wa walipa kodi na hivyo kuongeza makusanyo ya mapato ya Serikali.

Mhe. Naibu Spika, Nchi nyingi ikiwemo Tanzania imewekadhamira ya kuwekeza kwenye viwanda na hivyo kuleta mapinduzi katika uchumi. Katika

kipindi cha mwaka 2015 Uwekezaji katika Bara la Afrika ulifikia USD 66.5 bilioni. Kwa upande wa Zanzibar hali ya uwekezaji haikuwa ya kuridhisha katika kipindi cha mwaka 2016/2017, hivyo Serikali inajitahidi kufanya mazungumzo na wawekezaji wakubwa kuja kuwekeza kwenye viwanda.

Mhe. Naibu Spika, Katika kuhakikisha kuwa dhana ya kujenga uchumi wa viwanda katika nchi yetu inafanikiwa, Wizara yangu kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Viwanda *(United Nations Industrial Development Organization - UNIDO)* imefikia hatua nzuri ya kufanya mapitio ya Sera namkakati wa Viwanda ambao itapelekea kuimarisha uzalishaji wa bidhaa za ndani na uwekezaji katika maeneo mengine mapya ikiwemo la bahari kwa kutumia vizuri maliasili ya bahari *"Blue Economy"* na kusarifu mazao ya kilimo na mifugo ikiwemo mradi wa kusarifu mwani ikiwa ni wa majaribio.

Mhe. Naibu Spika, katika kutekeleza MKUZA III kwenye bajeti ya 2017 – 2018, lengo kubwa ni kuendeleza viwanda vitakavyo weza kuongeza ajira na kukuza sekta ya utalii, mkakati pacha wa kuendeleza sekta ya utalii *(TWIN ENGINE)*. Wizara yangu imepata wataalam ambao wanaangalia uwezekano wa kukuza viwanda vikiwemo vya nguo maalum kwa soko la ndani na nje kwa kukuza utalii, pia kutengeneza vipodozi, manukato na bidhaa za asili kwa kuwauzia watalii kwa kutumia viungo na mazao mengine yanayozalishwa hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, Mkakati huo pia, una dhamira ya kukuzaviwanda na uzalishaji wa arki za mimea na dawa za mimea, vipodozi, bidhaa maalum zikiwemo picha za kitalii na bidhaa za mapambo za kutumia malighafi za Zanzibar kwa ajili ya soko la utalii. Aidha, lengo jengine la mkakati huo ni kulitumia vizuri jina la Zanzibar kama *brand* kwa ajili ya kutengeneza bidhaa zinazoweza kupatikana Zanzibar pekee. Napenda kuliarifu Baraza lako Tukufu kwamba, Wizara yangu inaendelea kushughulikia mkakati huu kwa kushirikiana na Wizara ya Habari, Utalii, Michezo na Utamaduni na utatoa nafasi za ajira kwa vijana walio wengi nchini kujiajiri.

Mhe. Naibu Spika, katika mkakati huo pia viwanda vitakavyotengeneza bidhaa za madawa vitapewa kipaumbele vikiwemo viwanda vya chumvi na kutengeneza dawa kutokana na za hili la chumvi.

Kadhalika, tafiti zitafanywa kwa kuangalia uwezekano wa kukuza viwanda vya kufunganisha asali na kuuza nje ya nchi. Soko la asali limepatikana na wizara

yangu katika kipindi hiki cha bajeti itashajihisha wajasiriamali kuwezeshwa kuwa na viwanda vya kutengeneza asali na kuiuza nje ya nchi.

Mhe. Naibu Spika, katika kufanya mapitio ya kufanya mapinduzi ya viwanda kwa kuangalia hali ya Zanzibar kimkakati, wizara yangu inapitia tena taarifa ya kitaalam ya maeneo ya kiuchumi (*SEZ*) kwa ajili ya kuanzishwa eneo maalum la kufungua ofisi za kimataifa na mabenki hatimae kuifanya Zanzibar nzima kuwa ni kituo kikuu cha biashara katika ukanda wa Afrika ya Mashariki.

Eneo limekwishatengwa kwa shughuli hizo na kwa sasa tunaendelea kuzungumza na wawekezaji ili mradi huu uanzishwe sheria zake zitaharakishwe ili ziende sambamba na ujenzi unaoendelea katika eneo la Fumba. Hatimae Zanzibar iwe ni ya kisasa itakayo fungua milango kwa vijana kupata ajira na kuishi vizuri.

Mhe. Naibu Spika, Zanzibar ni visiwa vilivyojaaliwa kuwa na rasilimali itakayowezesha kutumia teknolojia na kuweza kuleta maendeleo ya viwanda. Hivyo suala zima la ubunifu *(innovation)* na kutumia ubunifu kibiashara na kwa kuendeleza teknolojia hususan ya TEHAMA (*ITC*) itakuwa ni eneo la lazima kwa maendeleo na kuiwezesha Zanzibar kuingia uchumi wa viwanda, na kufikia uchumi wa kati kama ilivyo katika dira ya 2020. Kwa vile serikali imekwisha weka mkonga wa mawasiliano na miradi iliyopangwa itawezekana hivyo suala la ubunifu *'INNOVATION'* na TEKNOLOJIA kwa kuwawezesha vijana wajiajiri inawezekana na hii ndio azma kubwa ya serikali kuona vijana wanajiajiri kwa kutumia biashara ya TEHAMA. Serikali imeanzisha Tamizi *(Incubator)* na *start up* kwa kuwapa uwezo wa kujiajiri

Mhe. Naibu Spika, naomba niwashukuru Kamisheni ya Sayansi na Teknolojia ya Tanzania *(COSTECH)* hususan Mkurugenzi Mtendaji Dkt. Hassan Mshimba kwa mashirikiano ya karibu na wizara yangu kwa kutuelimisha juu ya umuhimu wa kuwawezesha vijana kujiajiri kwa kushiriki kwenye *start up* na tamizi ambazo kituo cha serikali cha tamizi *(Incubation)* kinafanya vizuri katika kukuza teknolojia hiyo na biashara.

Mhe. Naibu Spika, wizara yangu itaendelea kufuatilia mradi huu ili kuwawezesha vijana wengi wajiajiri katika kutumia teknolojia. Pia kuangalia maeneo mengine ya kutengeneza taarifa za biashara *(*Vituo cha vya Tekinolojia - *Business Process Outsourcing - BPO)* kwa kuwa na eneo maalum la kufanyiashughuli hiyo na wawekezaji wa ndani na wa nje.

Mhe. Naibu Spika, ninawaomba vijana wawe na subra nawakubali kujifunza na kukubali ushauri wa serikali yao katika kupata elimu ya amali *(vocational and skills development)* ili iwawezeshe kupata jawabu zitakazoweza kutatua changamoto za nchi yetu na kuweza kufanya kazi kimataifa na kupata faida.

Mhe. Naibu Spika, katika kipindi hiki cha bajeti 2016-2017, thamani ya uzalishaji viwandani imeimarika kwa kufikia 487.9 bilioni kwa mwaka 2016 ukilinganisha na 417.0 bilioni mwaka 2015. Ukuaji huo umetokana na kuimarika kwa uzalishaji katika Viwanda vya Usarifu wa Nafaka, Kiwanda cha Maziwa cha Azam, Kiwanda cha Sukari Mahonda, Usarifu wa Matunda na Mboga Mboga, Viwanda vya Chai na Madawa, Viwanda vya Maji ya Chupa, Viwanda vya Kokoto na Matofali na venginevyo.

Aidha, uzalishaji huo umepelekea kuongeza mchango wa sekta ya viwanda katika Pato la Taifa kutoka asilimia 18.1 kwa 2015 na kufikia asilimia 18.6 mwaka 2016. Aidha, mchango wa uzalishaji *(manufacturing)* uliendelea kukuwa kutoka asilimia 6.7 kwa mwaka 2015 hadi kufika asilimia 6.9 kwa mwaka 2016. Ni matarajio yangu kwamba katika kipindi cha bajeti ya 2017-2018 mafanikio makubwa yatapatikana katika sekta hii ya viwanda na mchango wake katika Pato la Taifa utaongezeka.

Mhe. Naibu Spika, dalili za kuimarika zaidi kwa sekta ya viwanda zinaendelea kujitokeza kutokana na mambo yafuatayo:

i. Kuanza uzalishaji wa sukari katika kiwanda cha sukari, Mahonda, baada ya kukamilika ufungaji wa mitambo mipya na mikubwa zaidi ya kiwanda na utanuzi wa mashamba ya miwa.

ii. Kuongezeka kwa uzalishaji katika kiwanda cha *Zanzibar Milling Corporation* kufuatia ukarabati mkubwa na uwekezaji zaidi katika mradi huo;

iii. Kuimarika uzalishaji wa maziwa katika mradi wa *Azam Dairy Products uliopo Fumba*;

iv. Kuimarika kwa uzalishaji na ubora wa bidhaa za viwanda vidogo vidogo vikiwemo vya kutengeneza masala kwa kutumia viungo, sabuni za viungo na mwani, madawa na arki za asili, manukato, na chai za viungo mbali mbali, mazao hai yatokanayo na karafuu, pilipili hoho, mdalasini, pilipili manga, na mazao mengine yanayofanywa na wajasiriamali wadogo wa sehemu mbalimbali za

Unguja na Pemba; Naomba niwape shukurani na pongezi nyingi wajasiriamali wadogo wadogo kwa kuongeza uzalishaji katika sekta hii ya viwanda.

v. Kuendeleza uekezaji wa kiwanda cha uzalishaji mtindi *(yoghurt)*, Kiwanda cha kutengezea mifuko *(shopping bags)*, Kiwanda cha kubangulia korosho, kiwanda cha kusindika mafuta ya nazi, na kiwanda cha kutengeneza rangi. Viwanda hivi baadhi yake vimeekezwa katika eneo la *Amaan Industrial Park*;

vi. Kuimarisha usarifu wa chumvi inayozalishwa kisiwani Pemba;

vii. Vile vile hatua za kuanzisha kiwanda cha kusarifu samaki *(fish processing)* zinaendelea;

viii. Kiwanda cha kusarifu mwani;

ix. Kiwanda cha kutengeneza majiko yanayotumia spirit ya kiwanda cha sukari;

x. Kufufuliwa kiwanda cha makonyo Pemba na kujenga kiwanda chengine kama hicho Unguja mazungumzo na waliotia nia ya kujenga yanaendelezwa.

Mhe. Naibu Spika, kwa uzito wa kipekee bajeti hii, tutasimamiakwa jitihada zote miradi ya kukiendeleza Kiwanda cha Chumvi kilichopo Wawi na pia shamba kubwa la chumvi la ushirika la Shengejuu, Kiwanda cha Makonyo na kuendeleza mkakati wa kuanzisha kituo cha kuendeleza viwanda *(Industrial & ICT Park)* pamoja na TEHAMA katika eneo Tengefu la Kiuchumi (*SEZ*) kwa kuweka sera na sheria ili kuanza kuleta manufaa kwa Taifa.

Aidha, wizara kuendelea kuviendeleza na kuvisaidia viwanda vilivyopo vya maziwa, sukari na vya maji na vyengine kwa kupunguza changamoto za kukwama kuuza bidhaa zao Tanzania Bara kwa kukwamua vikwazo wanavyopata. Pia kutafuta masoko mengine ya Afrika, na Afrika Mashariki na nchi za nje kama vile nchi za Ghuba, nchi za Mashariki ya mbali kama China na kwengineko. Pia kutafuta njia ya maridhiano ya kuwezesha bidhaa zinazozalishwa Zanzibar kupata soko Tanzania Bara ili wawekezaji wasivunjike moyo.

Mhe. Naibu Spika, utaalamu wa hali ya juu unatakiwa upatikane wa kuweza kutengeneza bidhaa zenye viwango vya kimataifa vinavyokubalika kwa bei nzuri na kupatiwa masoko. Ni imani yangu kwamba chini ya Uongozi wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohamed Shein ambaye ndiye muungaji mkono wa juu wa dhana ya kujenga viwanda Zanzibar *(champion)* dhana hii itafanikiwa kwani kila mara husema Zanzibar yenye viwanda inawezekana. "Sasa tujenge Zanzibar ya Viwanda tukielekea kuwa na jamii yenye kipato cha kati ifikapo 2020". Namnukuu.

Mhe. Naibu Spika, sekta binafsi ndiyo muhimili mkuu katikaujenzi wa uchumi wa viwanda, hivyo tunategemea shughuli zao za uzalishaji bidhaa zenye viwango vya mahitaji ya ndani kuongezeka pamoja na kuuza nje ya nchi ili kupata fedha za kigeni. Kwa kuzingatia hilo wizara yangu imekuwa ikishirikiana kwa karibu na Jumuiya ya Wafanyabiashara na wenye Viwanda na Wakulima (*ZNCCIA*) pamoja na Mamlaka ya Ukuzaji Vitega Uchumi (*ZIPA*), na sekta nyengine katika kuongeza ubora na kujenga uchumi wa viwanda. Ushirikiano huo upo katika ngazi zote kuanzia uandaaji wa sera na mikakati ili kupata suluhu ya changamoto za kila siku

Mhe. Naibu Spika, napenda kukuhakikishia kuwa wizara yangu itaendelea kushirikiana na Jumuiya ya Wafanyabiashara, wenye Viwanda na Wakulima (*ZNCCIA*) na Taasisi nyengine za sekta binafsi katika kutekeleza majukumu yetu ili kuhamasisha wawekezaji katika ujenzi wa viwanda na katika sekta nyengine za uzalishaji na huduma.
Mhe. Naibu Spika, Sera ya Sekta Binafsi pamoja na ile yadhana ya viwanda kwa kutumia utaratibu wa mnyororo wa thamani (*value chain*) itafanyiwa kazi katika kipindi hiki cha bajeti kwa msaada wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AfDB*) pamoja na Jumuiya ya Ulaya (*EU*) kupitia Mradi wa *Tradecom* II kwani mkakati wa wizara juu ya mapinduzi ya viwanda ni kuunganisha viwanda katika ngazi zote ili kila kiwanda kikubwa kiweze kuunganishwa na viwanda vyengine kwenye mnyororo wa thamani kwa kuleta tija kwa wote.

Mhe. Naibu Spika, kwa kutekeleza dhana hiyo wizara imepanga kwa kila Wilaya iwe na mradi wake utakaojumuisha kilimo cha mazao ambayo ndio yanalimwa katika eneo hilo au ni malighafi ya asili na mwisho wake kuwepo na kiwanda cha Wilaya kwa kushirikiana na vijana na Halmashauri za wananchi. Mabaraza ya vijana yana uwezo mkubwa wakuwatumia vijana kwa uzalishaji kwa kushirikiana na Serikali Kuu na Serikali za wananchi ngazi za Wilaya na Halmashauri. Hii ni dhana itakayowapa muamko vijana na kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa Taifa.

Mhe. Naibu Spika, takwimu za viwanda Zanzibar zinaonyesha kwamba kuna asilimia 95% viwanda vidogo na vya kati. Hivyo mkakati uliofuatwa katika kupitia Sheria ya Viwanda ya mwaka 1998 na Sera na Sheria ya ujasiriamali ya mwaka 2006, kwa wizara kupendekeza kuanzishwa kwa chombo kitakachoweza kusimamia uendeshwaji wa viwanda vidogo vidogo na vya kati kwa kuvipa ushauri na teknolojia ya kujiendesha kwa ufanisi.

UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2016 – 2017:

Mhe. Naibu Spika, baada ya utangulizi huo, naomba sasa uniruhusu kueleza utekelezaji wa bajeti ya wizara kwa mwaka 2016 – 2017 na baadae kuwasilisha mapendekezo ya makadirio ya bajeti ya wizara kwa mwaka 2017 – 2018.

Mhe. Naibu Spika, kama unavyoelewa kuwa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko imepewa jukumu la kusimamia utekelezaji wa malengo ya maendeleo ya sekta kuu za uchumi wa Zanzibar ambazo ni biashara, uendelezaji viwanda na ukuzaji masoko. Katika kutekeleza majukumu hayo wizara yangu imejipangia kutekeleza Programu Kuu nne ambazo kwa ujumla zinakusudia kutekeleza malengo ya uimarishaji mazingira ya biashara, maendeleo ya viwanda, kuimarisha misingi ya ushindani wa kibiashara, ubora wa bidhaa na huduma zinazoingizwa katika soko la Zanzibar, kukuza ushirikiano baina ya Sekta binafsi na Serikali na kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa kuhusu biashara na maendeleo yake.

Ukusanyaji wa Mapato

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2016 – 2017, wizara yangu ilipangiwa kukusanya kiasi cha TZS. 371.23 milioni kutoka katika vyanzo vyake kama inavyoonekana katika Jadweli Nam. 7 hapo chini. Hadi kufikia mwezi wa Machi, 2017, jumla ya TZS. 221.50 milioni zilikwisha patikana ikiwa ni makusanyo ya ada zitokanazo na vyanzo hivyo na kuingizwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Kiasi hicho cha makusanyo ni sawa na asilimia 59.67 ya makisio ya makusanyo yote kwa mwaka wa fedha 2016– 2017.

Jadweli Nam. 7:
MapatoyaWizarakwakipindi cha Julai 2016 – Machi 2017

Kifungu	MaelezoyaMapato	Makadirio Julai – Juni 2017	Makusanyo Julai – Machi, 2017	AsilimiayaMakusanyo Julai - Machi
1422014	VipimonaMizani	100,000,000	38,157,000	38

1422077	KazizaBiashara	60,000,000	27,525,000	46
1146002	Ada yamalimaiti	400,000	329,000	82
1422030	AlamazaBiashara	90,500,000	78,530,400	87
1422031	UandikishajiMakampuni	56,332,000	48,529,700	86
1422032	UandikishajimajinayaBiashara	43,500,000	15,129,400	35
1422034	Ujirawakutengenezanyaraka	20,500,000	13,300,000	65
	JUMLA KUU	**371,232,000**	**221,500,500**	**59.67**

Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2016 – 2017

Mhe. Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2016 – 2017, wizara ilipangiwa kutumia kiasi cha TZS. 6,884.4 milioni kwa ajili ya matumizi ya shughuli zilizopangwa kutekelezwa katika program kuu ambazo zinahusisha matumizi ya kazi za kawaida, kazi za maendeleo, pamoja na matumizi ya ruzuku. Mgawanyo na upatikanaji wa fedha hizo kwa kila Programu kuu na program ndogo kwa ujumla ulikuwa ni TZS. 3,561.4 milioni sawa na asilimia 52 ya makadirio. Jadweli Nam. 8 hapa chini linatoa ufafanuzi zaidi juu ya utekelezaji wa program za Wizara.

Jadweli Nam 6:
MatumiziyaFedhakwakipindi cha Julai 2016 – Machi 2017

ukuu/Programundogo	**FedhayaBajeti 2016/17**	**Fedhailiyopatikana Julai -Machi 2016/17**	**Asilimiayafedhailiyopat - Machi 2016/17**
ya Utawala na Uendeshaji			
ndeshaji wa shughuli za Biashara, Masoko	1,370,575,000	1,062,851,094	78
atibu waMipango, Sera naUtafiti	313,060,000	225,984,173	72
fisiKuu – Pemba	341,670,000	299,404,670	88
go	**2,025,305,000**	**1,588,239,937**	**78**
ya Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali			
uzaji Viwanda	297,604,000	206,506,390	69
aendeleoyaUjasiriamali	56,821,000	8,163,000	14

go	**354,425,000**	**214,669,390**	**61**
yaUkuzajinaUendelezajiBiashara			
kuzajiMasokonaUsafirishaji	834,497,000	140,496,873	17
hindani asharanaKumlindaMtumiaji	116,640,000	2,064,006	2
iBiasharanaUkuzajiBiasharazandani	2,024,533,000	1,226,727,986	61
go	**2,975,670,000**	**1,369,288,865**	**46**
yaViwangonaUthibitiUbora			
TathminiyaUborawaBidhaa.	1,529,000,000	389,216,300	**25**
go	**1,529,000,000**	**389,216,300**	**25**
UU	**6,884,400,000**	**3,561,414,492**	**52**

Utekelezaji wa Programu za Wizara

Mhe. Naibu Spika, utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko ulifanyika kulingana na shughuli zilizowekwa katika programu za wizara kama ifuatavyo:

PROGRAMU KUU YA UTAWALA NA UENDESHAJI WA

WIZARA YA BIASHARA, VIWANDA NA MASOKO

Mhe. Naibu Spika, Programu Kuu ya Utawala na Uendeshaji wa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko imeundwa na Programu ndogo tatu ambazo ni Utawala na Uendeshaji wa Wizara; Programu ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti; na Programu ndogo ya ofisi kuu Pemba. Katika kutekeleza majukumu yake, program hii ilipangiwa matumizi ya TZS 2,025.31 milioni kwa mwaka wa fedha 2016 - 2017.

Napenda kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba, hadi kufikia Machi, 2017 programu hii imeingiziwa jumla ya TZS 1,588.24 ikiwemo mishahara na kazi nyengine za uendeshaji. Utekelezaji wa kazi zilizopangwa katika kila program ndogo nilizozitaja ni kama ifuatavyo:

Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji wa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko:

Mhe. Naibu Spika, programu hii ndogo ya Utawala na Uendeshaji inasimamiwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi. Kwa mwaka wa fedha 2016 - 2017 programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji wa wizara ilikuwa na jukumu la kutoa huduma ya uimarishaji wa mazingira mazuri ya kufanyia kazi, utoaji wa huduma kwa idara zote za wizara, na uratibu wa mikutano ya majadiliano ya ndani, ya kikanda na ya kimataifa. Program hii ndogo ilipangiwa matumizi ya TZS 1,370.58 milioni kwa mwaka wa fedha 2016 - 2017.

Hadi kufikia Machi, 2017, programu hii ndogo imeingiziwa jumla ya TZS 1,062.85 milioni ikiwemo mishahara na kazi nyengine za uendeshaji. Program ndogo ya Utawala na Uendeshaji ilitekelezwa kama ifuatavyo:-

a. Uimarishaji wa mazingira mazuri ya kufanyia kazi:

Mhe. Naibu Spika, kwa madhumuni ya kuweka mazingira mazuri ya kufanyia kazi, wizara iliendelea kuwalipa wafanyakazi wake wote mishahara yao kama inavyostahiki. Aidha, wizara iliwapatia wafanyakazi wake likizo zao na stahiki za likizo hizo, ambapo jumla ya wafanyakazi kumi (10) walipatiwa likizo za kawaida, wafanyakazi 4 likizo za dharura na mfanyakazi mmoja (1) likizo la uzazi. Kadhalika, wizara imefanya ukarabati wa mfumo wa maji, umeme pamoja na kupaka rangi, kuimarisha mfumo wa ulinzi kwa kuweka vyuma vya kuzuia wezi *(grill gate)* katika jengo la Makao Makuu ya Wizara.

b. Utoaji wa huduma kwa Idara

Mhe. Naibu Spika, shughuli zilizotekelezwa katika huduma hii ni kufanya tathmini ya mahitaji ya wafanyakazi kwa lengo la kuwa na idadi ya kutosha ya kuendesha shughuli za wizara kwa ufanisi na tija. Kwa lengo la kuimarisha ufanisi katika utendaji kazi kwa kuwajengea uwezo wafanyakazi, wizara iliendelea kutekeleza mpango wake wa mafunzo, ambapo jumla ya wafanyakazi kumi na sita (16) wanaendelea kupatiwa mafunzo ya muda mrefu katika fani za Sheria, Uongozi wa Biashara na Uchumi, na wafanyakazi wawili (2) wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi katika masuala ya biashara na ujasiriamali katika nchi za India na China.

Kwa upande wa manunuzi, Mhe. Naibu Spika, wizara kupitia mpango wake wa manunuzi *(annual procurement plan)* kwa madhumuni ya kusimamia vyema matumizi ya fedha za umma kwa mujibu wa sheria ya manunuzi, ilifanya manunuzi ya vifaa vya kuandikia, mafuta, kompyuta, samani na vifaa vya usafi

pamoja na huduma za umeme, maji na simu. Vifaa vyote hivi na huduma vimepatikana kwa wakati.

c. Uratibu wa mikutano ya majadiliano ya kibiashara

Mhe. Naibu Spika, katika kuendeleza ushiriki wa viongozi wa wizara katika Mikutano ya Sekta ya Biashara na Viwanda nchini, Kikanda na Kimataifa, wizara ilishiriki Mikutano ya majadiliano ya biashara katika ngazi za wataalamu na Mawaziri. Mikutano hiyo ya majadiliano ilifanyika katika kanda za Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya *SADC*, pamoja na majadiliano yanayoendelea ya kuanzisha Eneo moja la Biashara baina ya Jumuiya ya *EAC*, *SADC* na *COMESA*.

Aidha, wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ya Jamhuri ya Muungano ilishiriki vikao mbali mbali vikiwemo vya Tume ya Pamoja ya Mashirikiano (*JPC*) baina ya Tanzania na Muungano wa Falme za Kiarabu (UAE) kilichofanyika Abudhabi, na kile cha matayarisho kati ya Tanzania na Iran kilichofanyika Dar es Salaam. Vikao hivi vilizungumzia masuala ya urahisishaji wa biashara (*Trade Facilitation*) pamoja na mkataba unaohusu urahisishaji wa biashara *(World Trade Organisation Trade Facilitation Agreements).*Vile vile wizara ilishiriki katika mkutano wa *SADC* uliopanga siku maalum ya kushajiisha viwanda kwa kuwa na maonyesho nchini Swaziland na pia mkutano wa kuwasilisha mkakati wa viwanda kwa nchi za *SADC*.

A-2: Programu ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti

Mhe. Naibu Spika, programu ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti ilikuwa na jukumu la kutayarisha, kuchambua na kutathmini utekelezaji wa mipango na malengo maalum ya wizara. Program hii ndogo ilipangiwa matumizi ya TZS 313.060 milioni kwa mwaka wa fedha 2016 - 2017, ambapo hadi kufikia Machi 2017, imeingiziwa jumla ya TZS 225.98 milioni ikiwemo mishahara na kazi nyengine za kawaida.

Mhe. Naibu Spika, huduma ambazo zilitekelezwa katika programu ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti ni kama ifuatavyo:-

a. Mapitio na Uandaaji wa Sera za Biashara na Viwanda

Mhe. Naibu Spika, katika kutekeleza huduma hii, wizara inaendelea na matayarisho ya kuandaa Sera za Biashara na Viwanda ili kurahisisha uwekezaji

na biashara Zanzibar. Katika kufanikisha hayo wizara imepokea rasimu ya awali ya Sera ya Biashara kwa ajili ya kuzingatiwa na wataalamu pamoja na kutoa maoni kwa ajili ya utayarishaji na ukamilishaji wa sera hiyo.

Aidha, kwa upande wa kuandaa Sera ya Kumlinda Mtumiaji kutokana na bidhaa zisizo na ubora, wizara inaendelea na ukusanyaji wa taarifa muhimu kutoka kwa wadau ambazo zitasaidia katika kuandaa taratibu za kumpata mshauri mwelekezi atakae andaa sera hiyo. Taarifa hizo Mhe. Naibu Spika, zinahusiana na utambuzi wa sheria zinazotekelezwa Zanzibar ambazo zinamgusa mtumiaji.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa kazi ya kuifanyia mapitio Sheria ya Leseni ya Mwaka 1983, wizara yangu imekamilisha uandaaji wa Rasimu ya mapitio ya Sheria hiyo pamoja na dhana ya kufanya mapitio hayo ambavyo vinatarajiwa kuwasilishwa serikalini kwa mazingatio.

b. Utambuzi wa vikwazo katika kuongeza usafirishaji wa bidhaa nje

Mhe. Naibu Spika, **w**izara kwa msaada wa EU kupitia mradi wa *TradeCom II* imeshampata mshauri elekezi wa kuanza utafiti wa kuongeza ushindani kwa mazao yanayozalishwa ili tuweze kusafirisha katika masoko ya kimataifa "*Value Chain Analysis on Agro Processing Industries*". Aidha, katika kuondoa vikwazo vya kibiashara, wizara kwa kushirikiana na Jumuiya ya Wafanyabaishara, Wenye Viwanda na Wakulima (*ZNCCIA*) kwa ufadhili wa *TradeMark East Africa* (*TMEA*) tayari imeunda kamati ya kitaifa ya kusimamia vikwazo vya biashara visivyo vya kiushuru *(Non Tariff Barriers – NTBs)* na tayari kamati hiyo imeshapata mafunzo juu ya masuala ya *NTBs*.

c. Utayarishaji wa ripoti za utekelezaji wa bajeti

Mhe. Naibu Spika, kazi za kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo pamoja na kazi za kawaida zinaendelea kufanyika kwa kushirikiana na Tume ya Mipango ambapo ripoti za utekelezaji wa miradi na kazi za kawaida kwa kipindi cha robo tatu (3) zimeandaliwa. Aidha, katika kufanya matayarisho ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2017 – 2018, wizara imeandaa vipaumbele kwa Sekta ya Biashara na Viwanda. Vipaumbele hivyo ni utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Viwanda pamoja na uanzishwaji wa Shirika la Kusimamia Ulezi na Ukuzaji wa Miradi ya Viwanda Vidogo Vidogo na vya Kati *(Small and Medium Industry Development Organization - SMIDO),* Kufanya utafiti wa

mchango wa leseni katika uchumi na kuimarisha na kuongeza thamani bidhaa za viungo, chumvi na mwani.

d. **Uimarishaji wa uwezo wa wafanyakazi katika ukusanyaji taarifa na utumiaji wa teknolojia ya habari na mawasiliano**

Mhe. Naibu Spika, wizara imewapatia wafanyakazi wawili mafunzo ya takwimu yanayohusiana na *(Harmonised System Code- HS Code)* kwa lengo la kujua aina za bidhaa za kimataifa kwa mfumo wa *HS code*. Aidha, wizara imeweza kukusanya taarifa za idadi ya maduka katika mikoa yote ya Unguja na Pemba na kukusanya takwimu za bidhaa na aina ya biashara zinazoingizwa kutoka Tanzania Bara na nje ya nchi.

e. Ukondoweshaji wa Masuala Mtambuka

Mhe. Naibu Spika, katika kutekeleza huduma hizi, wizara ilifanya warsha kwa wafanyakazi 105 kwa lengo la kuwakumbusha madhara ya ugonjwa wa UKIMWI/AIDS na faida ya kujitambua. Aidha, mafunzo hayo yalifanikiwa kwa asilimia 90 ya wafanyakazi waliohudhuria walifanya vipimo kwa ajili ya kutambua afya zao.

A-3: Programu ndogo ya Ofisi kuu Pemba

Mhe. Naibu Spika, programu ndogo ya Ofisi Kuu Pemba ina jukumu la kutekeleza na kusimamia shughuli zote za Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa upande wa kisiwa cha Pemba. Program hii ndogo ilipangiwa matumizi ya TZS 341.67 milioni kwa mwaka wa fedha 2016 - 2017, na hadi kufikia Machi 2017, programu hii ndogo imeingiziwa jumla ya TZS 299.40 milioni ikiwemo mishahara na kazi nyengine za kawaida. Huduma zilizopangwa kutolewa na Programu hii ndogo ni kama zifuatazo:-

a. Utoaji wa huduma na ununuzi wa vifaa

Mhe. Naibu Spika, katika kutekeleza shughuli hii, wizara kupitia Afisi Kuu Pemba ilifanya ununuzi wa vifaa vya kufanyia kazi, ununuzi wa huduma za umeme, maji na mawasiliano ya simu na mtandao, matengenezo ya magari, ununuzi wa mafuta na kutoa huduma ya usafiri kwa maafisa wa wizara wa afisi ya Pemba kwa ajili ya ufuatiliaji wa kazi mbali mbali za wizara.

b Uimarishaji wa mazingira ya kazi

Mhe. Naibu Spika, katika kuimarisha mazingira ya kazi, Afisi Kuu Pemba iliwapatia wafanyakazi wawili (2) mafunzo ya muda mfupi na wafanyakazi wanne (4) mafunzo ya muda mrefu, katika ngazi ya shahada ya kwanza na ya pili yanayohusiana na masuala ya uchumi, biashara na ujasiriamali. Aidha, wizara kupitia Afisi kuu Pemba iliwapatia likizo wafanyakazi kumi na saba (17) pamoja na kuwapatia wafanyakazi malipo ya posho ya baada ya saa za kazi kwa shughuli zilizofanyika baada ya muda wa kazi.

c. Ukuzaji wa maendeleo ya wajasiriamali

Mhe. Naibu Spika, katika hatua ya kuwakuza na kuwaendeleza wajasiriamali wadogo wadogo na wakati, Afisi kuu Pemba iliratibu shughuli zote zinazohusiana na ukuzaji wa maendeleo ya wajasiriamali ambazo kazi zake zinatekelezwa kwa mujibu wa *program* husika.

d. Uhakiki na ukaguzi wa vifaa vya mezani, vipimo, maduka, mabekari, maghala na *supermarket*

Mhe. Naibu Spika, katika hatua ya kumlinda mtumiaji, Afisi kuu Pemba iliratibu shughuli zote zinazohusiana na ukaguzi wa vifaa vya mizani na vipimo, maduka, mabekari, maghala na *supermarket*.

B. PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA VIWANDA NA UJASIRIAMALI

Mhe. Naibu Spika, Programu kuu ya Maendeleo ya Viwanda ambayo utekelezaji wake unasimamiwa na Idara ya Maendeleo ya Viwanda pamoja na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti inajumuisha Programu ndogo mbili ambazo ni Ukuzaji Viwanda na Uendelezaji Wajasiriamali. Program hii kuu ilipangiwa jumla ya TZS 354.42 milioni kwa mwaka wa fedha 2016 – 2017. Hadi kufikia Machi 2017, programu hii kuu imeingiziwa jumla ya TZS214.67 milioni ikiwemo mishahara na kazi nyengine za kawaida. Program ndogo hizo utekelezaji wake ni kama ufuatavyo:-

B-1: Programu Ndogo ya Ukuzaji Viwanda

Mhe. Naibu Spika, Programu ndogo ya Ukuzaji Viwanda ina jukumu la kukuza na kuendeleza viwanda. Program hii ndogo ilipangiwa jumla ya TZS 297.60 milioni kwa mwaka wa fedha 2016 – 2017, na hadi kufikia Machi 2017, programu hii ndogo imeingiziwa jumla ya TZS 206.50 milioni ikiwemo

mishahara na kazi nyengine za kawaida. Utekelezaji wa program ndogo ya Ukuzaji Viwanda ulikuwa kama ifuatavyo:-

a. Uimarishaji wa Teknolojia ya uzalishaji kwa wazalishaji wadogo wadogo

Mhe. Naibu Spika, katika kutekeleza huduma hii, Wizarailiandaa na kufanya mikutano ya wazalishaji na wadau wa chumvi kisiwani Pemba. Lengo la mikutano hiyo ni kujadili matokeo na mapendekezo ya tafiti mbili zilizofanywa na wizara kwa ajili ya kuendeleza uzalishaji na usarifu wa chumvi nchini. Tafiti hizo zilizowasilishwa, moja ilihusu haja ya kuufanyia mabadiliko muundo wa Jumuiya ya Wazalishaji Chumvi wa Zanzibar (*AZASPO*) ili iweze kujiendesha kibiashara na tafiti ya pili ilihusu njia bora za kuimarisha soko la chumvi inayozalishwa nchini. Aidha, katika kuimarisha zao la mwani, wizara ilishiriki kikamilifu katika utafiti wa zao la mwani ambapo mapendekezo ya utafiti huo yamewasilishwa Baraza la Mapinduzi kwa kutolewa uamuzi.

b. Ukuzaji wa Sekta ya Viwanda

Mhe. Naibu Spika, Rasimu ya awali ya Sera ya Maendeleo yaViwanda imeandaliwa ambapo Wizara inaendelea na hatua ya ukusanyaji wa maoni ya wadau kwa hatua ya kupata sera kamili. Aidha, katika suala la kukuza viwanda wizara imewasilisha serikalini wazo la Zanzibar kuwa na Sheria yake ya kusimamia na kutoa leseni kwa miradi ya viwanda ili kurahisisha uanzishaji na usimamizi wa viwanda kufanyiwa maamuzi. Kadhalika, wizara imeandaa na kuiwasilisha Serikalini dhana *(concept)* ya kuanzisha Shirika la Kusimamia Ulezi na Ukuzaji wa Miradi ya Viwanda Vidogo Vidogo na vya Kati *(Small and MediumIndustry Development Organisation – SMIDO).* Napenda kuliarifu Baraza lako kuwa dhana hiyo bado inazingatiwa na serikali.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa ukusanyaji wa takwimu za viwandani, wizara imeendelea kukusanya takwimu hizo za uzalishaji viwandani kwa mwaka 2016. Maafisa wa Idara walishiriki katika kamati mbali mbali na kuangalia changamoto zinazoikabili miradi ya viwanda na iliangalia zaidi kiwanda cha kuzalisha sukari Mahonda. Changamoto ambazo zinazikabili Kiwanda cha Mahonda ambazo ziliainishwa ni pamoja na upatikanaji wa maeneo kwa ajili ya kuongeza ulimaji wa miwa na nyumba ambazo zinatakiwa kukabidhiwa wawekezaji ikiwa ni makubaliano yaliyomo katika mkataba wa ukodishwaji wa kiwanda hicho.

Mhe. Naibu Spika, napenda kuliarifu Baraza lako tukufu kuwa serikali imeanza kuchukua hatua za kuainisha maeneo hayo pamoja na nyumba zilizokuwa zinamilikiwa na Kiwanda cha Mahonda kwa ajili ya kuwakabidhi wawekezaji waliopo. Wizara yangu imekabidhiwa rasmi usimamiaji wa kiwanda cha Mahonda na imeunda kamati ya wataalam ya kuangalia kwa uzito wake kiwanda kinavyoendeshwa pamoja na changamoto ziliopo ikiwemo kupatiwa eneo, suala la usimamizi na uendeshaji wa kiwanda, pamoja na uhai wa kiwanda kwa kukipa uwezo wa kuuza sukari yao Zanzibar ili kiweze kumudu ushindani. Tunatarajia kukiwezesha kiwanda hiki kitoe mchango mkubwa katika kuendeleza uchumi wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, serikali ilifanya mapitio ya viwanda vyote vilivyokuwepo huko nyuma ili kuona kama vitaweza kuendelezwa. Hadi sasa ni viwanda viwili tu ndivyo vinavyofuatiliwa kuona kama vinaweza kupewa motisha ili vianze uzalishaji, vikiwemo Kiwanda cha Soda na Kiwanda cha Nguo cha *COTEX*. Aidha, mazungumzo yanaendelea kuona kwamba tutaweza kuviendeleza na kurudi katika hali yake au kuweza kufanya uzalishaji mwengine.

B-2: Programu ndogo ya Maendeleo ya Ujasiriamali

Mhe. Naibu Spika, Programu ndogo ya Maendeleo ya Ujasiriamali ina jukumu la ukuzaji wa ujasiriamali na ushindani. Program hii ndogo ilipangiwa jumla ya TZS 56.82 milioni kwa mwaka wa fedha 2016 – 2017. Hadi kufikia Machi, 2017 programu hii ndogo imeingiziwa jumla ya TZS8.16 milioni kwa kazi za kawaida. Utekelezaji wa program ndogo ya Maendeleo ya Ujasiriamali ulikuwa kama ifuatavyo:-

a. Ukuzaji wa Ujasiriamali na Ushindani

Mhe. Naibu Spika, wizara yangu kwa msaada wa *UNIDO* imefanya mapitio ya Sera ya Ujasiriamali ya 2006 na Sheria ya Ujasiriamali ambayo ni matarajio yetu kuiwasilisha katika Baraza lako tukufu katika kipindi cha robo ya mwanzo ya mwaka huu wa fedha 2017-2018. Katika sera hiyo utaratibu mzuri unawekwa kwa kuleya na kukuza wajasiriamali na viwanda vidogo na vyakati kwa lengo la kuwaunganisha na mnyororo wa thamani kwenye viwanda vikubwa kwa kuuza bidhaa zao, na pia kuwatafutia masoko ya kuuza bidhaa zao nje. Aidha, wizara itafanya tafiti ili kujua bidhaa zinazohitajika na zenye ubora unaotakiwa pamoja na kuwapatia mafunzo ya kuongeza ubora wa bidhaa hizo ili kuweza kuendeleza biashara zao.

Kadhalika, kwa vile suala la mitaji ni kikwazo kikubwa kwa wajasiriamali na wenye viwanda wadogo, Sera hii na Sheria itaweka masharti ya kuweza kuwapatia wajasiriamali mitaji ya kuendeleza biashara zao na ili waweze kukua na kufikia miradi mikubwa.

Mhe. Naibu Spika, katika kuwaendeleza wajasiriamali, wizara imetoa usaidizi na ushauri wa kitaalamu kwa vikundi saba vya uzalishaji kutoka Pemba ili waweze kushiriki katika Tamasha la Biashara la Zanzibar katika mwezi wa Januari 2017. Vikundi hivyo vinajihusisha na uzalishaji wa bidhaa za kusindika, kazi za mikono, samani, dawa za asili, sabuni, bidhaa za viungo na asali, na vyenginevyo.

Aidha, wizara ilifanya ukaguzi wa miradi 92 midogo midogo ya Viwanda pamoja na wajasiriamali kwa lengo la kutathmini maendeleo yao pamoja na kuwapatia ushauri wa kitaalamu kwa changamoto zilizopo.

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyoeleza hapo awali, kuhusiana na uzalishaji wa chumvi, wizara yangu ilitembelea mashamba 78 kisiwani Pemba kwa ajili ya kutathmini utendaji wao, ajira zinazotolewa na mashamba hayo na jinsi ya kuendeleza miundombinu yao. Inakisiwa kuwa kiasi cha wananchi 2,500 hupata ajira za moja kwa moja katika mashamba ya chumvi, na pia jumla ya wananchi 10,000 hupata ajira ambayo sio ya moja kwa moja kupitia mashamba hayo ya chumvi.

b. Usaidizi wa kuanzisha biashara kwa Wajasiriamali

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa kutoa usaidizi wa kuanzisha biashara kwa wajasiriamali, wizara imefanya utafiti mdogo juu ya uzalishaji wa asali katika mkoa wa Kusini Pemba. Utafiti huo ulibaini kuwa kiasi cha watu 85 wanajishughulisha na kazi ya uzalishaji asali. Aidha, kwa upande wa dagaa, wizara imeandaa dhana ya mradi ili kuongeza thamani kwa zao hilo ambapo itaongeza kipato kwa Wajasiriamali.

Mhe. Naibu Spika, katika kutekeleza Mpango wa Kurasimisha *(formalization)* biashara, wizara ilitoa mafunzo kwa wajasiriamali wa Wilaya ya Kati kwa lengo la kuwahamasisha ili kurasimisha biashara zao. Mafunzo hayo yalijumuisha mafunzo ya biashara, utunzaji wa kumbukumbu, usajili wa biashara, umuhimu wa kuweka akaunti maalum ya biashara na mengineyo ambapo tayari wafanyabiashara wameshaanza taratibu za kufanya usajili wa biashara zao.

C. PROGRAMU KUU YA UKUZAJI NA UENDELEZAJI WA BIASHARA

Mhe. Naibu Spika, Programu Kuu ya Ukuzaji na Uendelezaji wa Biashara inajumuisha programu ndogo tatu ambazo ni Ukuzaji wa Masoko na Usafirishaji; Ushindani wa Kibiashara na kumlinda Mtumiaji; pamoja na Urahisishaji wa Biashara na Ukuzaji biashara za ndani. Program hii ilipangiwa matumizi ya TZS 2,975.67 milioni kwa mwaka wa fedha 2016 - 2017.

Hadi kufikia Machi, 2017 programu hii imeingiziwa jumla ya TZS 1,369.28 milioni ikiwemo mishahara, Ruzuku, Miradi nakazi nyengine za uendeshaji. Utekelezaji wa kazi zilizopangwa katika kila program ndogo nilizozitaja ni kama ifuatavyo:

C-1: Programu ndogo ya Ukuzaji wa Masoko na Usafirishaji

Mhe. Naibu Spika, Programu ndogo ya Ukuzaji wa Masoko na Usafirishaji inasimamiwa na Idara ya Biashara na Masoko pamoja na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Huduma ambazo zimesimamiwa na kutekelezwa na Programu hii ndogo ni Fursa za Masoko na Urahisishaji biashara; Mradi wa Kujenga uwezo wa Kukondoesha Biashara; Uratibu wa Mkakati wa Usafirishaji bidhaa nje; na Mradi wa Mkakati wa Maendeleo ya Karafuu.

Program hii ndogo ilipangiwa jumla ya TZS 834.49 milioni kwa mwaka wa fedha 2016 - 2017. Hadi kufikia Machi 2017 programu hii ndogo imeingiziwa jumla ya TZS 140.49 milioni kwa Mradi wa Mkakati wa Maendeleo ya Karafuu na kazi za kawaida.

Mhe. Naibu Spika, katika kuangalia suala la masoko, wizara yangu inafanya utafiti kwa usaidizi wa *Trade Mark East Africa* ya muundo bora katika kusimamia suala la kukuza masoko kwa bidhaa na huduma zinazotolewa Zanzibar. Changamoto kubwa iliyopo ni kutumia jina la Zanzibar linalotambulika na kukubalika kimataifa kutokana na historia yake kwa kuendeleza maendeleo ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, suala la kukuza jina la Zanzibar *(Brand Name)* linafanyiwa kazi na kuangalia muundo gani utatuwezesha kujitambulisha kwa jina la Zanzibar, kwa bidhaa au huduma zote tutakazoziuza katika maeneo ya utalii, bidhaa za viwandani, utamaduni na michezo ikiwemo michezo ya asili pamoja na vitu vya asili kama vile vyakula, mavazi kama kanzu na kofia za viuwa za Zanzibar. Hatua hiyo inalenga kuzalisha ajira kwa ajili ya vijana wetu.

Mhe. Naibu Spika, wizara yangu inafanya utafiti kwa kuleta maana mpya ya Zanzibar kwamba ni mahali unapopata bidhaa hai za asili ambazo hazina madawa wala athari za kiafya *(Zanzibar is the Spice of Life).* Pia utafiti huo unakusudia kuonyesha kwamba Zanzibar ni mahala ambapo utapata starehe za kukumbuka milele na pia kupata utamaduni asilia wa watu wa ukanda wa pwani (utamaduni na mila za waswahili wa leo na wa kale). Hatua za awali zimeanza kwa kuifanyia *branding* karafuu na viungo vyengine.

a. Fursa za Masoko na Urahisishaji Biashara

Mhe. Naibu Spika, wizara ilifanya mapitio ya hali ya masoko kwa bidhaa zetu na kuangalia changamoto zilizopo. Shughuli mbali mbali za kupanua masoko ya bidhaa za Zanzibar na fursa zilizopo zinachunguzwa ili tuweze kuingia katika masoko ya kanda yakiwemo Afrika ya Mashariki, *SADC* pamoja na nchi za nje zikiwemo nchi za Mashariki ya mbali, nchi za Ghuba ikiwemo UAE, Oman, Kuwait, Iran, na kadhalika.

Aidha, wizara iliratibu ushiriki wa Zanzibar katika Maonesho ya 40 ya Kimataifa ya Biashara (Saba Saba) yaliyofanyika huko Dar es salaam mwezi wa Julai 2016. Taasisi zilizoshiriki ni pamoja na Shirika la Biashara la Taifa – *ZSTC*, Shirika la Bima la Zanzibar, Mamlaka ya Ukuzaji Vitega Uchumi ya Zanzibar – *ZIPA* na wajasiriamali wengine kutoka Zanzibar. Bidhaa ambazo zilionyeshwa na wajasiriamali walioshiriki katika maonesho hayo ni pamoja na bidhaa za kusindika, kazi za mikono, samani, dawa za asili, sabuni, bidhaa za viungo na nyenginezo.

Mhe. Naibu Spika, wizara yangu kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania iliandaa Kongamano maalum la Kibiashara kati ya Tanzania na Comoro lililofanyika katika mwezi Novemba 2016. Kongamano hilo lilikutanisha takriban wafanyabiashara 50 kutoka Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Comoro. Aidha, kupitia Kongamano hilo, nchi zetu hizi zilikubaliana kuanzisha safari za Tanzania na Comoro kwa kutumia Meli yetu ya M.V Mapinduzi II.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba hivi sasa Meli yetu ya Mapinduzi imeshaanza safari kwa kwenda Comoro. Aidha, wizara yangu imepeleka wataalamu wa kurahisisha biashara *(trade facilitation)* kwa kufanya utafiti juu ya kukuza biashara baina ya Comoro na Tanzania. Ninawaomba wafanyabiashara wote waangalie fursa zilizopo Comoro kwa kuendeleza biashara kwa maslahi ya pande zote mbili.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa ushiriki wa maonesho ya Kikanda ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, wizara yangu iliratibu ushiriki wa wajasiriamali kutoka Zanzibar katika Maonesho ya Jua Kali/Nguvu kazi yaliyofanyika nchini Uganda ambapo wajasiriamali 10 walilipiwa gharama za ushiriki wa maonesho hayo ili kuweza kutangaza bidhaa zao. Wizara itajiandaa vizuri pamoja na kushirikiana na Wizara ya Uwezeshaji kwa maonesho yanayokuja kwa kuwawezesha washiriki wengi na bidhaa nyingi zaidi zipate soko.

Mhe. Naibu Spika, wizara inaandaa utaratibu wa kuwa na ratiba ya matamasha ili iwawezeshe wajasiriamali kupata fursa ya kuuza bidhaa zao na pia kuiwezesha Zanzibar kuwemo katika ratiba ya tamasha za kimataifa. Utaratibu tunauandaa wa kuunganisha matamasha yote na kuwa na ratiba itakayotangazwa mapema ili ijulikane kimataifa. Serikali imeongeza maeneo ya kufanyia matamasha ikiwemo mradi wa wizara yetu wa kujenga kituo cha mikutano na maonesho huko Nyamanzi, Mnara wa Mapinduzi Michenzani, Ngome Kongwe na maeneo ya mahoteli ya Mji Mkongwe na nje ya mji. Lengo likiwa ni kuongeza maeneo ya masoko kwa bidhaa za wajasiriamali na kukuza utalii.

Mhe. Naibu Spika, katika hatua nyengine ambayo imechukuliwa ya kuhakikisha wajasiriamali wanaweza kupata masoko ya bidhaa zao, wizara ilitayarisha Tamasha la Biashara ambalo hufanyika kila mwaka kama ni sehemu ya kuadhimisha Sherehe za Mapinduzi ya Zanzibar. Tamasha la Biashara la mwaka huu lilihusisha jumla ya wajasiriamali wapatao 145 kutoka Zanzibar na nje ya Zanzibar.

Aidha, wizara imekamilisha taratibu za zabuni kwa ajili ya ununuzi wa magazebo na vifaa vyengine ambavyo vitatumika kwa ajili ya utayarishaji wa matamasha na maonesho mengine ya kibiashara hapa Zanzibar. Magazebo hayo yanatarajiwa kuwasili hapa Zanzibar mwishoni mwa mwezi wa Agosti, 2017.

b. Uratibu wa Mkakati wa Usafirishaji bidhaa nje

Mhe. Naibu Spika, kwa lengo la kuongeza usafirishaji wa bidhaa nje. Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ya Jamhuri ya Muungano inaendelea na kazi ya kufanyia mapitio Mkakati wa Usafirishaji bidhaa Nje (*NES*), ambapo taarifa za awali zinazohusiana na biashara zimekusanywa. Maeneo ambayo yamezingatiwa zaidi katika mapitio

ya Mkakati huo ni kilimo, na utalii. Mapitio hayo yanafanyika kwa ufadhili wa Benki ya Dunia.

c. Mradi wa Mkakati wa Maendeleo ya Karafuu

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyokuwa nikiliarifu Baraza lako kwamba wizara yangu inaendelea kuandaa mkakati wa kuifanyia karafuu ya Zanzibar utambulisho maalum unaofahamika kama *Branding*, kwa kushirikiana na Shirika la Biashara la Kimataifa *(International Trade Center – ITC)* pamoja na Shirika la Haki Miliki la Kimataifa (*WIPO*). Napenda kuliarifu Baraza lako kwamba kazi hiyo imekamilika katika hatua ya awali na uzinduzi wake umefanywa na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein mwezi wa Januari, 2017.

Mkakati huo utasaidia kuongeza thamani kwa bidhaa za viungo vyengine mbali na karafuu. Hivyo natoa wito kwa wananchi wa Zanzibar kulima kwa wingi mazao hayo ya viungo kwa ajili ya kuweza kuuza bidhaa hizo katika masoko ya kimataifa na pia katika soko la ndani la utalii. Shirika la *ZSTC* kwa mwaka huu litatangaza bei ya mazao haya mara utafiti utakapo kamilika ili wananchi waweze kulima zaidi na kuongeza fedha za kigeni.

d. Mradi wa Kujenga uwezo wa Kukondoesha Biashara

Mhe. Naibu Spika, katika kutekeleza huduma hii, wizara yangu ilitekeleza mradi wa kujenga uwezo wa kukondoesha Biashara kwa kujadili ripoti ya utafiti wa sekta ya biashara ya Zanzibar ijulikanao kama *'Diagnostic Trade Integration Study'* (*DTIS*) na kutoa mapendekezo kwa lengo la kuimarisha sekta ya biashara nchini. Utafiti huo ulifanywa na wataalamu waelekezi kutoka Benki ya Dunia ambapo wataalamu kutoka sekta ya umma na sekta binafsi walishiriki katika kujadili Ripoti hiyo.

Aidha, kupitia mradi huu, wizara imetoa mafunzo yanayohusiana na uimarishaji wa Takwimu za Biashara na upatikanaji na ukusanyaji wa taarifa za biashara kwa taasisi zinazohusiana na biashara (Taasisi za umma na binafsi) ambazo zitasaidia kutumika katika masula ya uchambuzi wa hali ya uchumi pamoja na kuandaa sera maalum za kuimarisha sekta.

Mhe. Naibu Spika, kwa lengo la kurahisisha ufanyaji biashara nchini, wizara imetoa mafunzo yanayohusiana na umuhimu wa kuanzisha biashara katika mtandao *(e-commerce)* ambayo itarahisisha biashara nchini. Katika mafunzo hayo wataalamu kutoka sekta zinazohusiana na uzalishaji walishiriki na

kujadiliana hatua za kuchukuliwa katika kuanzisha Biashara katika mtandao. Aidha, uimarishaji wa uzalishaji wa bidhaa zenye ubora ambao utapelekea ushindani wa kibiashara ili kukidhi mahitaji ya soko ni moja wapo ya hatua za uanzishwaji wa biashara katika mtandao.

Aidha, Wizara ikishirikiana na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ya Tanzania bara wanaendelea kufanya mapitio ya Mkakati wa Usafirishaji Bidha Nje (*NES*) ambapo taarifa za awali zinazohusiana na biashara kwa sekta za uzalishaji zikiwemo sekta ya Kilimo, Mifugo, Maliasili, Biashara zimekusanywa na kuwaasilishwa mbele ya wataalamu katika kikao kilichofanyika Arusha na Zanzibar. Mapitio hayo yanafanyika kwa ufadhili wa Benki ya Dunia.

C-2: Programu ndogo ya Ushindani wa Kibiashara na kumlinda Mtumiaji

Mhe. Naibu Spika, Programu ndogo ya Ushindani wa Kibiashara na kumlinda Mtumiaji ina jukumu la kutoa huduma za ukaguzi na uhakiki wa vifaa; mizani na vipimo; ukaguzi wa Maduka ya Sonara; ukaguzi wa biashara na maghala; ushajihishaji na utoaji wa elimu kwa watumiaji; na uimarishaji wa mazingira ya kazi. Program hii ndogo ilipangiwa jumla ya TZS 116.64 milioni kwa mwaka wa fedha 2016 - 2017. Hadi kufikia Machi 2017, programu hii ndogo imeingiziwa jumla ya TZS 2.06 milioni kwa ajili ya kazi za kawaida. Huduma hizo zilitekelezwa kama ifuatavyo:-

Ukaguzi na uhakiki wa Vifaa, Mizani na Vipimo

Mhe. Naibu Spika, Wizara ina jukumu la kufanya ukaguzi wamizani, vipimo, vituo vya mafuta, magari ya mafuta, matangi ya mafuta, pampu za kuuzia mafuta na mita kubwa za mafuta Kwa mwaka wa fedha 2016 - 2017 Wizara ilifanya ukaguzi kama inavyoonekana katika Jadweli Nam 9 la hapo chini.

Jadweli Nam 9:

HudumayaUkaguzi

Eneo la Ukaguzi	**Jumla**
Mezani	2,215
Weigh bridge	2
Pampuzakuuziamafuta	331
Matangiyakuuziamafuta	12
Magariyakusambazamafuta	7

Crane zakupimiauzitowaKontena	2

Chanzo: WizarayaBiashara, ViwandanaMasoko

Ukaguzi wa biashara na maghala

Mhe. Naibu Spika, kwa madhumuni ya kusimamia mwenendo wa biashara na kumlinda mtumiaji wizara imefanya ukaguzi wa maduka, maghala, bekari na supermarket ili kubaini ubora wake pamoja na bei za bidhaa hizo kama inavyoonekana katika Jadweli Nam 10 hapo chini.

Jadweli Nam 10:

HudumazaUkaguzi

Eneo la ukaguzi	**Jumla**
Maduka	4,180
Maghala	176
Bekari	45
Supermarket	6

Chanzo: WizarayaBiashara, ViwandanaMasoko, 2016

Mhe. Naibu Spika, Katika ukaguzi uliofanyika, bidhaa mbalimbali zenye thamani ya TZS 16.5 milioni zilipatikana zikiwa zimepitwa na muda wake wa matumizi na zilikamatwa na kuondolewa madukani na zikaangamizwa. Bidhaa zilizokamatwa ni pamoja na vyakula vya makopo, taulo za watoto na watu wazima, magodoro, nguo za ndani, juisi, dawa za kuulia mbu na bidhaa nyengine za matumizi ya majumbani.

C-3: Programu ndogo ya Urahisishaji wa Biashara na Ukuzaji biashara za ndani

Mhe. Naibu Spika, Program ndogo ya Uendeshaji Biashara naUkuzaji Biashara za Ndani ilitekelezwa na Baraza la kusimamia mfumo wa Utoaji Leseni, Baraza la Taifa la Biashara na Idara ya Biashara na Ukuzaji Masoko, ambapo ilipangiwa kutumia jumla ya TZS 2,024.53 milioni kwa mwaka wa fedha 2016 - 2017.

Hadi kufikia Machi 2017, programu hii ndogo imeingiziwa jumla ya TZS 1,226.72 milioni kwa ajili matumizi ya kazi za kawaida, Ruzuku na kazi za

maendeleo. Programu ndogo ya Urahisishaji wa Biashara na Ukuzaji biashara za ndani ina jukumu la kutekeleza huduma zifuatazo:-

a. Uwekaji wa taratibu za Utoaji na Udhibiti wa Leseni

Mhe. Naibu Spika, **k**atika kutekeleza huduma hii, Baraza limeandaa Kanuni *(regulations)* kwa ajili ya utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa mfumo wa utoaji leseni ya mwaka 2013 na kuchapisha nakla 180 za muongozo na kusambazwa kwa Mamlaka za utoaji wa leseni na wadau wengine. Aidha, Baraza limefanya uchambuzi na kuandaa taarifa za Mamlaka 34 za utoaji leseni za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, pamoja na kuandaa mpango wa mageuzi ya mfumo wa utoaji leseni utakaotekelezwa 2017 - 2018.

Mhe. Naibu Spika, Kwa upande wa ukusanyaji takwimu, Baraza lipo katika hatua za awali za kuanzisha '*data base'* za ukusanyaji wa taarifa za utoaji wa leseni kutoka katika Mamlaka zinazohusiana na utoaji leseni zikiwemo taarifa za sheria, kanuni, tozo na miongozo. Kwa upande wa utafiti Baraza linaendelea na utafiti wa kutambua mchango wa utoaji leseni katika uchumi wa Zanzibar.

b. Utoaji wa Huduma za Utawala na Uendeshaji wa Baraza la Leseni

Mhe. Naibu Spika, Katika kutekeleza huduma hii, Baraza limeandaa rasimu ya Kanuni za Utumishi na Fedha ili kuimarisha mfumo wa utawala na uendeshaji. Baraza limewapatia
Wafanyakazi watano (5) mafunzo yanayohusiana na masuala ya usimamizi pamoja na sheria mpya ya usimamizi wa utoaji leseni na kufanya Ununuzi wa vifaa vya ofisi na huduma ikiwemo ununuzi wa viyoyozi, vifaa vya habari na mawasiliano *(ICTequipment)*, friji, malipo ya huduma ya mafuta, internet, maji na umeme na kufanya matengenezo ya ofisi.

c. Ushauri na Uhamasishaji kwa Wadau

Mhe. Naibu Spika, katika kutekeleza huduma hii, Baraza limeandaa mikutano minane (8) ya mashauriano na Mamlaka za utoaji leseni kwa lengo la kuandaa taarifa zinazohusiana na utaratibu wa utoaji leseni, vibali na ruhusa nyengine zinazohusiana na Biashara. Pia, Mikutano mitatu ya Baraza imefanyika kwa madhumuni ya kupitia Mamlaka za utoaji leseni kwa lengo la kuweka vigezo, misingi, na taratibu za utoaji leseni ili kurahisisha upatikanaji wa leseni. Baraza

lilishiriki mikutano miwili ya majadiliano ya masuala ya leseni iliyofanyika Dar es Salaam.

Aidha, Baraza liliandaa warsha nne (4) ili kutoa elimu kwa Mamlaka za utoaji leseni, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi na wafanyabishara, kushiriki katika tamasha la Biashara na kufanya ukaguzi kwa mamlaka za utoaji leseni na uanzishaji wa tovuti ya Baraza.

d. Utekelezaji wa Sheria ya Biashara ya Zanzibar Na.11 ya mwaka 2013

Mhe. Naibu Spika, katika kutekeleza huduma hii, Wizarailitoa elimu ya ushajihishaji kwa wafanyabiashara juu ya bidhaa zilizomaliza muda wa matumizi ili kuepusha wananchi wasioelewa kutumia bidhaa hizo.

Kusimamia Utawala na uendeshaji wa Baraza la Taifa la Biashara

Mhe. Naibu Spika, Baraza la Taifa la Biashara ni chombo muhimu katika kukuza biashara hapa Zanzibar. Wizara imeendelea kusimamia shughuli mbali mbali za uendeshaji wa Baraza la Taifa la Biashara pamoja na kutoa huduma muhimu za kuendeshea ofisi ya Baraza hilo kwa kununua vifaa vya ofisi. Aidha, Wizara imeandaa Sheria mpya inayohusiana na usimamizi wa Baraza la Taifa la Biashara ambayo inatarajiwa kuwasilishwa katika Baraza la Wawakilishi.

Kadhalika, kikao kimoja cha Kamati Tendaji ya Baraza la Taifa la Biashara kimekutana kwa ajili kupitia Sheria hiyo pamoja na kuandaa Mkutano wa Baraza unaokuja.

f. Usimamizi wa Usajili wa Biashara na Mali

Mhe. Naibu Spika, Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali (*BPRA*) kwa kushirikiana na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko imepata mshauri elekezi kutoka *"Norway Register Development"* kwa ajili ya kuandaa mfumo wa usajili wa biashara'Business Registration System'. Mkataba wa utekelezaji wa kazi hiyo umekamilika baada ya kupitiwa na Afisi ya Mwanasheria Mkuu na kuthibitishwa kuendelea na kazi. BPRA imeshakamilisha kazi hiyo kwa kuwekeana saini na mshauri mwelekezi.

Mhe. Naibu Spika, Katika kufanya mapitio ya sheria ya Usajiliwa Majina ya Biashara *Cap. 168, BPRA* imekamilisha kazi ya kupitia sheria ya Usajili wa

Majina ya Biashara na kuandaa rasimu ya awali ambayo itajadiliwa kwa pamoja na wataalamu wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu. Aidha, katika kutekeleza kazi ya kuandaa kanuni za sheria ya Kampuni namba 15 ya mwaka 2013, rasimu ya awali ya kanuni hizo pamoja na marekebisho ya sheria hiyo yamekamilika. Kwa sasa BPRA inaendelea kushirikiana na watendaji wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu kukamilisha kazi hiyo.

Mhe. Spika, *MPRA* itaifanyia marekebisho Sheriaya kuanzisha ofisi ya Wakala wa Biash Naibu ara na Mali Nam. 13 ya mwaka 2012, Sheria ya Haki Miliki *(Industrial Property -IP)* pamoja na kutengeneza kanuni za Sheria ya Ufilisi *(Insolvency).* Aidha, Wizara yangu kwa kushirikiana na Shirika linalosimamia Malibunifu kanda ya Afrika (*ARIPO*) tunaandaa semina ya malibunifu *(roving seminar)* ambayo inatarajiwa kufanyika mwezi wa Julai, 2017. Semina hiyo itawashirikisha taasisi mbali mbali za Serikali na watu binafsi kwa kushajihisha katika masuala ya malibunifu, alama za biashara na haki miliki.

PROGRAMU KUU YA VIWANGO NA TATHMINI YA UBORA

Mhe. Naibu Spika, Programu kuu ya Viwango na tathmini ya ubora inajumuisha Programu moja ambayo ni Viwango na Udhibiti wa Ubora. Programu hii ilipangiwa matumizi ya TZS1,529.0 milioni kwa mwaka wa fedha 2016 - 2017. Hadi kufikia Machi 2017, programu hii imeingiziwa jumla ya TZS 389.21 ambayo ni Ruzuku ya mishahara na ya kazi za kawaida. Utekelezaji wa huduma zilizopangwa katika program ndogo nilizozitaja ni kama ifuatavyo:

Programu ndogo ya Viwango na Udhibiti wa Ubora

Mhe. Naibu Spika, Programu ndogo ya Viwango na Udhibitiwa Ubora inasimamiwa na Taasisi ya Viwango Zanzibar na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Programu ndogo ya Viwango na Udhibiti wa Ubora ilikuwa na jukumu la kutekeleza huduma zifuatazo:-

a. Uandaaji na Ukuzaji wa Viwango

Mhe. Naibu Spika, Viwango 41 vimeandaliwa na 40 vikokatika hatua ya rasimu ambapo lengo la mwaka ilikua ni kuandaa viwango 80 vya Zanzibar. Aidha, Maombi 23 ya leseni ya matumizi ya alama ya ubora ya *ZBS* yamepokelewa na kati ya hayo bidhaa tisa (9) zimepatiwa leseni ya matumizi ya alama ya ubora ya ZBS na bidhaa tatu (3) zimepewa cheti kwa mara nyengine *(Renewal).*

Kadhalika, Sampuli 59 zimekusanywa na kupelekwa maabara kwa hatua za upimaji wa ubora wa bidhaa hizo ambapo bidhaa mbili zilikosa viwango na ubora unaotakiwa na hatua za kuziondosha sokoni zilichukuliwa. Kati ya bidhaa zilizoondoshwa sokoni ni Mafuta ya injini *(engine oil)* lita 12,859 na tende katuni 30. Aidha, Taasisi ya Viwango imepata uanachama wa uangalizi *(observer)* katika Bodi ya Shirika la Viwango ya Afrika *ARSO*, katika kikao cha 22 kilichofanyika Arusha tarehe 22/06/2016.

b. Huduma ya Tathmini ya Ubora wa Bidhaa

Mhe. Naibu Spika, Taasisi ya Viwango imefanikiwa kutoa Vyeti vya ubora 2,671 kupitia mawakala wake kwa Ukaguzi unaofanywa nje ya nchi (PVoC). Kati ya vyeti hivyo, vyeti 2,238 ni vya magari yaliyotumika na vyeti 433 ni bidhaa nyengine zisizokua magari. Aidha, Taasisi ilifanya ukaguzi wa shehena *(consignments)* 288 za bidhaa baada ya kufika bandarini *(Destination Inspection).*

c. Utoaji wa huduma za Utawala na Uendeshaji wa Taasisi

Mhe. Naibu Spika, Huduma za uendeshaji wa ofisi zimeendelea kuimarishwa ikiwemo kuima Naibu risha tovuti ya Taasisi ya Viwango na kuifanya kuwa na muonekano wenye ubora zaidi pamoja na kuwekewa taarifa. Aidha, Taasisi imefanya ununuzi wa kompyuta 9, printer 5, umeme, mafuta ya gari, samani za ofisi pamoja na kukamilisha matengenezo ya ofisi za *ZBS* ziliopo Bandarini na Chake Chake ambazo zimeanza kutoa huduma baada ya kuwekewa huduma zote za msingi. Aidha, Taasisi iliwapatia mafunzo ya muda mfupi wafanyakazi 23 ikiwemo mafunzo maalum ua mifumo ya usimamizi ubora.

d. Mradi wa Kuimarisha Taasisi ya Viwango Zanzibar

Mhe. Naibu Spika, Taasisi ya Viwango imekamilisha taratibu za manunuzi kwa kazi za maendeleo ikiwemo kukamilisha na kusainiwa kwa mikataba ya awamu ya kwanza ya ujenzi wa ofisi na maabara Maruhubi na ununuzi wa vifaa vya maabara ya kemia kwa ajili ya bidhaa za petrol na utekelezaji wake umeshaanza katika maeneo yote mawili.

SHIRIKA LA BIASHARA LA TAIFA *ZSTC*:

a. Uvunaji na usafirishaji Karafuu:

Mhe. Naibu Spika, Shirika la *ZSTC* lilijiwekea lengo la kununua Karafuu tani 2,810 kwa thamani ya TZS. 39 bilioni kwa msimu wa mwaka 2016 - 2017. Hadi kufikia tarehe 30.03.2017 jumla ya tani 2,257.7 za Karafuu zimenunuliwa kutoka kwa wakulima kwa thamani ya TZS**.** 31**.7** bilioni.

b. Bei ya kununulia Karafuu:

Mhe. Naibu Spika, Shirika bado linaendelea kununua Karafuukulingana na Sera ya Serikali ya kununua Karafuu kwa bei ya asilimia 80 ya bei ya kuuzia nje. Katika msimu wa mwaka 2016

– 2017 bei ya kununulia Karafuu ilikuwa kama ifuatavyo:-

Daraja la	1	-	TZS 14,000
Daraja la	2	-	TZS 12,000
Daraja la	3	-	TZS 10,000

Aidha, Kwa upande wa mauzo ya karafuu, Shirika liliuza jumla ya tani 2,156 zenye thamani ya *USD* 16.67 Millioni sawa na TZS 36.0 bilioni hadi 31/3/2017.

c. Uzalishaji wa Mafuta ya Makonyo na Mimea

Mhe. Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2016 - 2017, kiwanda cha makonyo kilikadiriwa kuzalisha jumla ya tani 27.3 za mafuta ya makonyo. Hadi kufikia Machi 2017, jumla ya tani za mafuta ya makonyo na mimea yenye thamani ya TZS milioni zilizalishwa, na tani 25.4 za mafuta hayo zenye thamani ya TZS 534.2 milioni ziliuzwa.

d. Mradi wa Kukuza Biashara

Mhe. Naibu Spika, Shirika la Biashara la Taifa kwa mwaka huuwa fedha limepanga kuwekeza zaidi kwa kufanya matengenezo ya Kiwanda cha Makonyo kwa kuweka vifaa vipya katika mashine zao ili kuongeza ufanisi. Hatua hii itakiwezesha kiwanda kuweza kutengeneza mafuta mengi kwa ajili ya kuuzwa nje ya nchi na pia kukidhi mahitaji mbali mbali kwa viwanda vya ndani. Mkakati huo unaenda sambamba na upanuzi wa shamba la mtakata kwa kulima ekari 100 kwa kuanzia ili pia liweze kutoa malighafi za kutosha kwa

ajili ya uzalishaji wa kiwanda kwa kutumia ukulima wa kisasa na umwagiliaji maji .

Mhe. Naibu Spika, upanuzi huu pia utawapa nafasi wakulimahasa vikundi vya uzalishaji wa vijana kujipanga na kutafuta mashamba kwa ajili ya kulima mazao hayo muhimu. Shirika limejipanga kwa kutayarisha mbegu zitakazohitaji kwa shughuli hii zikiwemo mchai chai, mirehani na majani mengine. Mkakati huo pia kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi itawezesha kuanza kidogo kidogo kurudi katika uzalishaji wa viungo na kuweza kukamata soko letu la asili kisiwa chetu cha Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, vile vile Shirika katika kufanya biashara linajipanga kuangalia biashara nyengine na pia kuangalia uwezekano wa kufanya biashara kwa upande wa Tanzania Bara. Wizara yangu inafanya utafiti kuangalia maeneo ya kuanzia yatakayoleta manufaa zaidi na faida kubwa.

CHANGAMOTO:

Mhe. Naibu Spika, katika utekelezaji wa malengo na majukumu mbali mbali ya Wizara kwa mwaka 2016 – 2017 yapo mafanikio makubwa yaliyopatikana. Hata hivyo, pamoja na mafanikio hayo, zipo pia changamoto kadhaa ambazo ziliendelea kuathiri utekelezaji wa malengo yaliyopangwa na ufanisi wa sekta ya biashara na maendeleo ya viwanda. Miongoni mwa changamoto hizo ni kama ifuatavyo:-

(i) Mwenendo wa biashara katika masoko ya kimataifa ambao kwa kiasi kikubwa umeendelea kutibuliwa na matokeo mbali mbali ya majanga ya kimaumbile ikiwemo ukame na mafuriko, matukio ya kisiasa na vita vinavyoendelea katika nchi za kiarabu na kuathiri bei za mafuta duniani, uharamia katika pembe ya Afrika, kasi ndogo ya kuimarika chumi za magharibi kunatokana na mtikisiko wa kifedha uliojitokeza hivi karibuni na athari zake kwa mwenendo wa bei za chakula katika soko la Zanzibar. Hata hivyo, kuna mabadiliko katika uuzaji wa bidhaa za kilimo duniani inategemewa hali inaweza kuwa nzuri kwa mujibu tafiti wa Benki ya Dunia.

ii. Uwezo mdogo wa uzalishaji wa ndani wa bidhaa na udhaifu wa kutumia fursa za masoko ya kikanda kuongeza usafirishaji pamoja na thamani ya uzalishaji huo.

iii. Mwitikio mdogo wa sekta binafsi kuwekeza katika viwanda na kuongeza pato la sekta hiyo. Kadhalika, utaalamu mdogo katika uendeshaji viwanda, mitaji, gharama kubwa za umeme na uhaba wa malighafi, utaratibu wa ghafla wa kubadilisha viwango vya kodi, na malipo mengine bila ya kuwapa muda wafanyabiashara na wajasiriamali zimeendelea kuainishwa kama ni kikwazo katika maendeleo ya viwanda hapa Zanzibar.

iv. Mfumo na utekelezaji wa sheria za kodi ambao unaacha mwanya kwa bidhaa za nje ambazo pia huzalishwa nchini, kuingia na kuuzwa kwa bei za chini kuliko gharama halisi za kuzalisha bidhaa hizo hapa nchini.

v. Utayari na uwezo wa wafanyabiashara wa Zanzibar kuzitumia fursa za kibiashara zilizopo katika masoko ya Jumuiya za Kikanda kama vile *SADC* na *EAC* na nchi zengine.

vi. Uwezo mdogo wa watendaji katika sekta ya biashara na upungufu wa wataalam kwa ujumla inaweza kuwa ni kikwazo cha kutekeleza Sera na Mikakati hii mipya.

Ufinyu wa bajeti wa kuweza kuendeleza na tafiti na kufanya tafiti za masoko na bidhaa zinazohitajiwa zitakwamisha mikakati mipya kufanikisha kwa ufanisi.

Mhe. Naibu Spika, kuna haja ya kuwashirikisha wananchi wote ikiwemo Serikali kuu, Serikali za mitaa, vyombo visivyo vya Serikali, Sekta binafsi, Jumuiya mbali mbali na makundi ya vijana wanawake na wote kwenye jamii ili waelewe hizi dhana mpya na mkakati inayopendekezwa na pia kujiandaa kujitoa ili fursa hizi ziweze kupatikana na Taifa liende mbele. Kuna haja ya kufanya kazi kwa pamoja na kuwa na ari ya kuirudisha Zanzibar katika hadhi yake iliyokuwa zamani kama wao waliweza na sisi tutaweza tu.(*Makofi*)

Kwa ujumla Mhe. Spika, changamoto hizo bado zipo na zinaendelea kuwa na athari katika utekelezaji wa mikakati na malengo tunayojipangia.

VI. PROGRAMU ZA WIZARA KWA MWAKA 2017 – 2018

Mhe. Naibu Spika, Kwa mwaka wa fedha 2017 – 2018, Wizara imeweka umbele wa mgawanyo wa rasilimali katika maeneo ya msingi ya majukumu yake ya ukuzaji biashara, uendelezaji wa viwanda, uwekaji wa mazingira ya kuhamasisha biashara, usarifu wa bidhaa, na usaidizi wa wajasiriamali na wawekezaji wadogo wadogo. Aidha, kazi nyengine ambazo zitapewa umbele ni

pamoja na utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Viwanda pamoja na uanzishwaji wa Shirika la kusimamia ulezi na ukuzaji wa miradi ya viwanda vidogo vidogo na vya kati *(Small and Medium Industry Development Organization - SMIDO)*, na kufanya utafiti wa mchango wa leseni katika uchumi.

Kadhalika kwa upande wa ukusanyaji mapato, Wizara itaendelea kupanua wigo wa vianzio vya mapato yake kwa kukagua bidhaa zilizofungashwa *(pre – packed goods)*, bidhaa zinazoingizwa nchini na za viwandani pamoja na usajili wa biashara mpya na mali.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2017 – 2018 Wizara yangu itaendelea kutekeleza program kuu nne (4) kama zifuatavyo:

i. Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya BVM

ii. Programu ya Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali

iii. Programu ya Ukuzaji na Uendelezaji Biashara

iv. Programu ya Viwango na Uthibiti Ubora

A. PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA BIASHARA, VIWANDA NA MASOKO

Mhe. Naibu Spika, Programu kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Biashara, Viwanda, na Masoko imegawika katika Programu ndogo tatu kwa mujibu wa huduma ambazo inazitoa. Program hizo ndogo ni kama zifuatazo:

i. Uendeshaji wa shughuli za Biashara, Viwanda na Masoko

ii. Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti

iii. Uratibu na Utekelezaji wa shughuli za Wizara Pemba

Mhe. Naibu Spika, Programu ndogo ya Uendeshaji wa shughuliza Biashara, Viwanda na Masoko ambayo inatekelezwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi itakuwa na jukumu la usimamizi wa rasilimali watu na huduma kwa ujumla pamoja na ununuzi wa vifaa.

Ili kutekeleza majukumu yake, program hii ndogo imepangiwa matumizi ya TZS 1,613.13 milioni kwa mwaka wa fedha 2017– 2018.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa program ndogo ya Uratibuwa Mipango, Sera na tafiti za Wizara ambayo utekelezaji wake utasimamiwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti itakuwa na jukumu la uandaaji na uibuaji wa sera na tafiti za Wizara, uandaaji na utekelezaji wa mipango ya Wizara pamoja na usimamizi wa takwimu za Biashara na Viwanda.

Katika kutekeleza huduma hizo programu ndogo ya uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti imepangiwa matumizi ya TZS 340.92 milioni kwa mwaka wa fedha wa 2017 – 2018.

Mhe. Naibu Spika, Program ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara Pemba ambayo ina ratibu shughuli za uendeshaji wa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa upande wa Pemba imepangiwa matumizi ya TZS 390.31 milioni kwa mwaka wa fedha wa 2017 – 2018.

Mhe. Naibu Spika, Ili kuweza kutekeleza shughuli zilizopangwa kutekelezwa katika Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa mwaka 2017– 2018, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha matumizi ya TZS 2,344.36 kwa program hii.

B. PROGRAMU YA MAENDELEO YA VIWANDA NA UJASIRIAMALI

Mhe. Naibu Spika, Programu ya Maendeleo ya Viwanda naUjasiriamali itakuwa na majukumu ya kuandaa na kutekeleza sera na mikakati ya maendeleo ya Viwanda na ukuzaji ujasiriamali. Programu hii imegawika katika program ndogo mbili kulingana na majukumu na huduma inazokusudia kuzitoa ambazo ni:

i. Ukuzaji Viwanda
ii. Maendeleo ya Ujasiriamali

Mhe. Naibu Spika, Programu ndogo ya ukuzaji Viwanda itakuwa na jukumu la kutoa huduma za Uimarishaji wa Uzalishaji kwa wazalishaji wadogo wadogo pamoja na Uimarishaji wa Sekta ya Maendeleo ya Viwanda, ambazo utekelezaji wake utasimamiwa na Idara ya Maendeleo ya Viwanda.

Ili kutekeleza huduma hizo, programu hii ndogo imepangiwa matumizi ya TZS 644.99 milioni kwa mwaka 2017 – 2018.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa programu ndogo ya Ukuzaji Ujasiriamali, ambayo itakuwa na jukumu la kutoa huduma za kutoa msaada kwa wajasiriamali ambapo utekelezaji wake utasimamiwa na Idara ya Maendeleo ya Viwanda. Ili kutekeleza huduma hizo, programu hii ndogo imetengewa TZS 267.59 milioni kwa mwaka 2017 – 2018.

Mhe. Naibu Spika, ili kutekeleza majukumu ya Program yaMaendeleo ya Viwanda na Ukuzaji Ujasiri amali kwa mwaka 2017 – 2018, naomba Baraza lako liidhinishe matumizi ya TZS912.58 milioni kwa ajili ya kutekeleza shughuli za programu hii.

C. PROGRAMU YA UKUZAJI NA UENDELEZAJI BIASHARA

Mhe. Naibu Spika, Programu ya tatu itakayotekelezwa naWizara kwa mwaka 2017 – 2018 ni Ukuzaji na Uendelezaji Biashara. Kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa malengo yake, programu hii imegawanyika katika Programu ndogo ndogo nne (4) kama zifuatavyo:

ii. Ukuzaji Masoko na Usafirishaji
iii. Ushindani Halali wa Biashara na Kumlinda Mtumiaji
iii. Urahisishaji Biashara na Ukuzaji Biashara za ndani
iv. Usajili wa Biashara na Mali

Mhe. Naibu Spika, Programu ndogo ya Ukuzaji Masoko nausafirishaji itakuwa na jukumu la kutoa huduma za uwekaji na uimarishaji wa mazingira mazuri ya biashara pamoja na kuongeza fursa za masoko na urahisishaji biashara ambapo utekelezaji wake utasimamiwa na Idara ya Biashara.

Ili kutekeleza huduma hizo programu ndogo ya Ukuzaji wa Masoko na Usafirishaji kwa mwaka 2017 – 2018, naliomba Baraza lako liidhinishe matumizi ya TZS 316.20 milioni.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa programu ndogo yaUshindani Halali wa Kibiashara na Kumlinda Mtumiaji ambayo itakuwa na jukumu la kuimarisha ushindani halali wa kibiashara na kumlinda mtumiaji kwa kuendelea kutoa huduma za ukaguzi na uhakiki wa vifaa vya mizani, vipimo, ukaguzi wa biashara na maghala pamoja na Ushajihishaji na Utoaji wa Elimu kwa

Watumiaji, ambapo utekelezaji wake utasimamiwa na Idara ya Ushindani Halali wa Biashara.

Ili kutekeleza huduma hizo, naliomba Baraza lako liidhinishe matumizi ya TZS 143.34 milioni kwa mwaka wa fedha 2017 – 2018.

Mhe. Naibu Spika, Programu ndogo ya Urahisishaji Biasharana Ukuzaji Biashara za Ndani itakuwa na jukumu la usimamizi wa mamlaka zinazotoa leseni pamoja na uimarishaji wa majadiliano baina ya sekta ya Umma na Sekta Binafsi.

Ili kutekeleza huduma hizo ambazo zimepangwa kutekelezwa chini ya Programu hii ndogo, naliomba Baraza lako liidhinishe matumizi ya TZS 502.20 milioni.

Mhe. Naibu Spika, Programu ndogo ya Usajili wa Biashara na Mali ambayo itakuwa na jukumu la usimamizi wa usajili wa biashara na mali. Ili kutekeleza huduma hizo, naliomba Baraza lako liidhinishe TZS 507.72 milioni kwa mwaka 2017 – 2018.

Mhe. Naibu Spika, ili kutekeleza huduma zilizopangwakutekelezwa katika Programu hii ya Ukuzaji na Uendelezaji Biashara kwa mwaka 2017 – 2018, naliomba Baraza lako liidhinishe TZS 1,469.46 milioni.

D. PROGRAMU YA VIWANGO NA TATHMINI YA UBORA

Mhe. Naibu Spika, Programu ya nne itakayotekelezwa naWizara kwa mwaka 2017 – 2018 ni Viwango na Tathmini ya Ubora. Kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa malengo yake, programu hii imepangiwa kuwa na programu ndogo moja ya Uthibiti wa ubora ambayo itakuwa na huduma za Uandaaji na Ukuzaji wa Viwango pamoja na huduma za Tathmini ya Ubora wa Bidhaa. Utekelezaji wake utasimamiwa na Taasisi ya Viwango Zanzibar (*ZBS*). Ili kutekeleza shughuli zilizopangwa katika programu hii, naliomba Baraza lako liidhinishe TZS 2,483.80 milioni kwa mwaka wa fedha 2017 – 2018.

Mhe. Naibu Spika, Taarifa kamili ya Wizara hii imeelezwa katika kitabu cha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Bajeti inayotumia Programu (*PBB*) kwa mwaka wa fedha 2017/2018 – 2020/2021 kutoka ukurasa wa R-1 mpaka ukurasa wa R-21.

SHIRIKA LA BIASHARA LA TAIFA – *ZSTC*

Shughuli za Shirika kwa mwaka wa fedha 2017 – 2018:

Mhe. Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2017 - 2018, Shirika la *ZSTC* linatarajia kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Kununua karafuu kutoka kwa wakulima kwa msimu wa mwaka 2017 - 2018 na kuandaa mikakati ya upatikanaji wa fedha kwa ajili ya ununuzi huo;

ii. Kutekeleza mageuzi ya Shirika kwa mujibu wa Mkakati wa Mageuzi wa miaka kumi (2011 – 2021) na hasa katika maeneo yafuatayo:

   a. kufanya *branding* ya karafuu;
   b. kufanya ukarabati wa baadhi ya vituo;
   c. kufuatilia masoko ya karafuu nje ya nchi.
   d. kufanya mabadiliko ya muundo ili kuongeza ufanisi

iii. Kuimarisha biashara ya Karafuu katika soko la ndani, soko la utalii na masoko ya kikanda, pamoja na kuimarisha ufungashaji wa bidhaa za karafuu, makonyo na viungo vyengine;

iv. Kutoa mikopo kwa wakulima pamoja na kuwakatia Bima ya kuanguka mikarafuu;

v. Kufanya usajili wa wakulima na wadau wa zao la Karafuu pamoja na mashamba ya mikarafuu kwa mujibu wa Sheria ya Maendeleo ya Karafuu Namba 2 ya mwaka 2014;

vi. Kuchangia gharama za uatikaji wa miche ya mikarafuu;

vii. Kuwapatia zawadi wakulima na wauzaji bora wa karafuu;

viii. Kuanzisha kilimo cha umwagiliaji maji katika Shamba la Mtakata *(Irrigation System)*. Kazi hiyo itahusisha uchimbaji wa visima viwili (2) pamoja na kufunga vifaa vya umwagiliaji wa hekta arubaini (40) za awali;

ix. Kufanya upandaji wa miche mipya ya mimea ya mlangilangi (5 hekta), Mchaichai (10 hekta) na mrehani (5 hekta);

x. Kufanya utafiti wa mazao ya Shamba la Mtakata pamoja na Utafiti wa maradhi ya Mchaichai;

xi. Kuweka kamera za ulinzi *(CCTV Camera)* katika Kiwanda cha Makonyo; na kuhudhuria maonesho ya Biashara nje na ndani ya nchi.

xii Kufanya utafiti wakupanuwa wigo wa biashara ikiwemo kuimarisha kituo cha ZSTC Dar-es-Saalam kwa biashara na Tanzania Bara

Mhe. Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2017– 2018, Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika la Biashara la Taifa limeidhinisha matumizi ya Jumla ya TZS 125.6 billioni katika kutekeleza kazi za kawaida na Maendeleo.

SHUKRANI:

Mhe. Naibu Spika, mafanikio ya wizara yaliyopatikana ni matokeo ya mashirikiano makubwa ya Wajumbe wa Baraza hili chini ya uongozi wako mahiri. Ninakushukuru wewe binafsi, Wenyeviti wa Kamati za kudumu za Baraza na Wajumbe wote kwa ushauri na michango mliyotupa katika kipindi cha utekelezaji wa bajeti iliyopita.

Mhe. Naibu Spika, sinabudi kukiri vile vile kuwa mafanikio ya kiutendaji yaliyojitokeza katika kipindi cha mwaka 2017– 2018 ni matokeo ya ushirikiano mkubwa uliopatiwa Wizara yangu kutoka wadau mbali mbali wa ndani na nje ya nchi yetu ikiwa pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu pamoja na Kamati zake za kudumu. Kwa madhumuni ya kutambua mchango mkubwa wa Wadau mbali mbali kwa Wizara, naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa nchi na taasisi za ndani na nje zifuatazo:-

i. Jamhuri ya Watu wa China;

ii. India;

iii. Shirika la Kimataifa la Kusimamia Malibunifu *(WorldIntellectual Property Organisation – WIPO);*

iv. Kituo cha Biashara cha Kimataifa *(International Trade Center– ITC)*

v. Jumuiya ya Ulaya (EU);

vi. USAID;

vii. Korea Kusini;

viii. Mpango wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa (UNDP);

ix. Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Viwanda (UNIDO);

x. Benki ya Maendeleo ya Afrika – AfDB

xi. TradeMark East Africa – TMEA

xii. Benki ya Dunia *(World Bank);*

xiii. Shirika la Biashara Duniani (WTO);

xiv. Sekretarieti ya Jumuiya ya Madola *(Commonwhealth Secretariat);*

xv. Jumuiya za Wafanyabiashara, Wenye Viwanda na Wakulima za Zanzibar na Tanzania Bara;

xvi. Baraza la Biashara la Tanzania (*TNBC*); na

xvii. Wafanyabiashara wote wakubwa na wadogo na Wawekezaji wa Viwanda na Wajasiriamali wote wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri umebakiza dakika 4 malizia.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Msoko: Namaliza.

Mhe. Naibu Spika, napenda nichukue fursa hii kwa maranyengine tena kuwapongeza kwa dhati wafanyakazi wote wa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa kazi kubwa yenye ufanisi mzuri wanayoifanya kila siku licha ya kukabiliwa na changamoto mbali mbali, ni matarajio yangu kwamba wataongeza juhudi zao, ili kuzidisha ufanisi kwa kuwahudumia wananchi na kutekeleza majukumu yao ipasavyo. Kadhalika, napenda kuwapongeza wafanyakazi wote walioshiriki katika maandalizi ya hotuba hii kwa kazi nzuri waliyoifanya, nawaombea dua njema katika kazi zao.

Mhe. Naibu Spika, naomba niwashukuru wafanyabiashara wote wakubwa, wakati, wadogo na Juakali na wengine kwa juhudi zao kubwa za kuwahudumia wananchi kwa kuwapatia huduma mbali mbali pamoja na bidhaa muhimu za nguo, chakula, vyombo vya moto, na vifaa vya ujenzi. Nawaomba waendelee kushirikiana na Wizara yangu kwa kufanya kazi pamoja kwa lengo la kuimarisha biashara na kutoa huduma bora kwa wananchi.

Nawaomba wafanyabiashara wote kuwahurumia wananchi kwa kuwawekea bei nafuu ili wamudu maisha yao katika mwezi huu mtukufu wa Ramadhani. Aidha, nawaomba wafanyabiashara waekeze katika viwanda, biashara, kilimo na usarifu wa mazao ya kilimo ikiwemo viungo *(spices)* kama vile mdalasini, manjano na viungo vyengine kwani vinafaida kubwa katika kuendesha biashara na kuongeza ajira.

VIII. MAOMBI YA FEDHA KWA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2017 – 2018

Mapato ya Serikali:

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2017 – 2018, Wizaraimepanga kukusanya jumla ya TZS 455 milioni. Mapato hayo yatakusanywa kutoka vianzio vifuatavyo kama inavyoonekana katika Jadweli Nam 11:-

1
3
5

Jadweli Nam 11:
VyanzovyaMapatokwamwaka 2017 - 2018

KIFUNGU	MAELEZO	MAKADIRIO (mil)
R 0104	**IdarayaBiasharanaUkuzajiMasoko**	**160.00**
1422014	Ukaguziwamezaninavipimo	95.00
1422077	Malipoyakazizabiashara	65.00
R0106	**WakalawaUsajiliwaBiasharana Mali**	**294.00**
1146002	Ada ya Mali Maiti	1.00
1422030	AlamazaBiashara	156.00
1422031	UandikishajiwaMakampuni	81.00
1422032	Uandikishajiwamajinayabiashara	31.00
1422034	Ujirawakutengenezanyaraka	26.00
JumlaKuu		**455.00**

Matumizi:

Mhe. Naibu Spika, Kwa upande wa matumizi na ili Wizarayangu iweze kutekeleza programu zake ilizojiwekea kwa mwaka wa fedha 2017 – 2018, naiomba Baraza lako liidhinishe matumizi ya jumla ya TZS 7,210.20 milioni kwa programu nne (4) kama inavyoonekana katika Jadweli Nam 12:

Jadweli Nam 12:
MaombiyaFedha (TZS Mil)

Geresho (Code)	ProgramuKuu/Programundogo	Makadirio 2017 - 2018 (mil)
PR0101	**UtawalanaUendeshajiwaUratibuwaWizarayaBiashara, ViwandanaMasoko**	**2,344.36**
SR010101	UendeshajiwaWizarayaBiashara, ViwandanaMasoko.	1,613.13
SR010102	UratibuwaMipango, Sera naUtafiti	340.92
SR010103	UratibunaUtekelezajiwashughulizaWizara Pemba	390.31
PR0102	**Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali**	**912.58**
SR010201	UkuzajiwaViwanda	644.99
SR010202	MaendeleoyaUjasiriamali	267.59
PR0103	**UkuzajinaUendelezajiwaBiashara**	**1,469.46**
SR010301	UkuzajiwaMasokonaUsafirishaji	316.20
SR010302	UshindaniHalaliwakibiasharanaKumlindaMtumiaji	143.34

SR010303	UrahisishajibiasharanaUkuzajiBiasharazandani	502.20
SR010304	UsajiliwaBiasharana Mali	507.72
PR0104	**ViwangonaTathminiyaUborawabidhaa**	**2,483.80**
SR010401	ViwangonaUthibitiUbora	2,483.80
JUMLA KUU		**7,210.20**

HITIMISHO:

Mhe. Naibu Spika, nawaomba wafanyabiashara wote kuwahurumia wananchi kwa kuwawekea bei nafuu ili wamudu maisha yao katika mwezi mtukufu wa Ramadhan.

Aidha, nawaomba wafanyabiashara wawekeze katika viwanda, biashara, kilimo na usarifu wa mazao ya kilimo. Vikiwemo viungo vya *spice* kama vile mdalasini, manjano na vyenginevyo.

Mhe. Naibu Spika, naomba kwa mara nyengine tena kukushukuru wewe binafsi pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu na wananchi kwa ujumla kwa kunisikiliza.

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko. Hongera sana Mhe. Waziri umesoma hotuba yako yote kwa *one hour* kama ilivyo ndani ya kitabu, hongera sana.

Waheshimiwa Wajumbe, sasa nimwite bado tuna saa nzima. Kwa hivyo, naomba nimwite Mhe. Mwenyekiti wa Kamati inayoshughulikia Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko. Mwenyekiti karibu sana.

Mhe. Hamad Abdalla Rashid: (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo): Mhe. Naibu Spika, awali ya yote napenda nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mola Mtukufu mwenye kustahiki kushukuriwa na viumbe vyote kwa kutujaalia uhai na afya njema tukaweza kukutana katika

Baraza hili Tukufu, kwa lengo la kuendelea kuwatumikia wananchi wa Zanzibar, kwa kutekeleza majukumu yetu mbali mbali kwa niaba yao, ambapo leo tupo hapa kuipitia na kuijadili Bajeti ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mhe. Naibu Spika, pongezi za pekee nazitanguliza kwake Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein, pamoja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ujumla kutokana na juhudi wanazozichukua za kuwaendeleza Wajasiriamali wetu, kwani wamekuwa wakitekeleza kazi zao pasi na kuwepo vikwazo vya aina yoyote. Kwa kuzingatia juhudi hizo, nawaomba Wajasiriamali hao waongeze ubunifu wa kuzalisha bidhaa zenye ubora, ili ziwezeshe kunufaisha wao katika soko liliopo ndani na nje ya nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, kwa namna ya pekee naomba kutumia nafasi hii kumshukuru na kumpongeza Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Mheshimiwa Balozi Amina Salum Ali; Katibu Mkuu, Wakurugenzi pamoja na watendaji wengine wote wa wizara hii kwa juhudi wanazozichukua katika kutekeleza majukumu yao, pamoja na mashirikiano yao ya dhati waliyoipatia Kamati wakati wote tulipokuwa tukipitia na kujadili Bajeti ya Wizara hii.

Mhe. Naibu Spika, Kwa niaba ya Kamati ya Kudumu inayoshughulikia Fedha, Biashara na Kilimo, napenda kukushukuru kwa dhati kabisa, wewe binafsi Mhe. Naibu Spika, kwa kunipatia nafasi hii ya kuwasilisha Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mhe. Naibu Spika, kadhalika, napenda niwapongeze Waheshimiwa Wawakilishi wote waliomo katika Baraza lako Tukufu, kwa juhudi wanazozichukua za kuwawakilisha wananchi wao, juhudi zao zimewawezesha wananchi kujenga imani kubwa kwa Baraza lako, nasi tunawaahidi kwamba tutaendelea kuwatumikia kwa dhati kama ambavyo walivyotuamini kutuchagua na kutuleta katika chombo hiki kwa lengo la kutetea maslahi yao.

Mhe. Naibu Spika, kwa heshima na taadhima, kwa kuthamini michango na ushauri mkubwa katika kutekeleza kazi za Kamati hii, naomba sasa niwatambue kwa kuwataja majina yao Waheshimiwa Wajumbe wafuatao wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo:-

1.	Mhe. Yussuf Hassan Iddi	-	Mwenyekiti
2.	Mhe. Hamida Abdalla Issa	-	Makamo Mwenyekiti
3.	Mhe. Hamad Abdalla Rashid	-	Mjumbe
4.	Mhe. Mohammed Mgaza Jecha	-	Mjumbe
5.	Mhe. Ali Salum Haji	-	Mjumbe
6.	Mhe. Ussi Yahya Haji	-	Mjumbe
7.	Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-	Mjumbe.

Aidha, Kamati yetu pia inafanyakazi kwa karibu sana na makatibu wawili (2) ambao kwa kiasi kikubwa wamekuwa wakitusaidia kutekeleza majukumu yetu, kwa heshima naomba niwatambue makatibu hao ni:-

1.	Ndugu Ramadhan Khamis Masoud	-	Katibu
2.	Ndugu Said Khamis Ramadhan	-	Katibu

Mhe. Naibu Spika, kamati yangu ya Fedha, Biashara na Kilimo imefanya kazi ya kuchambua na kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa kuzingatia matakwa ya Jadweli la Kwanza la Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, Toleo la mwaka 2016.

Mhe. Naibu Spika, kwa mujibu wa Programu inayozingatia matokeo yaani (*PBB*), Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko imeundwa na Fungu Kuu moja la R01 na limepangiwa kutekeleza Programu kuu nne, zenye Programu ndogo kumi (10), ambazo kwa ujumla zinajumuisha shughuli na huduma zote zinazokusudiwa kutolewa na wizara hii katika mwaka ujao wa fedha 2017/2018.

Mhe. Naibu Spika, kwa heshima na taadhima, sasa naomba nitoe maoni ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa Programu Kuu na Programu ndogo za wizara hii ambazo Kamati yangu imezitolea maelekezo na ushauri kama ifuatavyo:

PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA VIWANDA NA UJASIRI AMALI

Mhe. Naibu Spika, Programu hii ya Maendeleo ya Viwanda na Ujasiri amali imeundwa na Programu ndogo mbili zinazojumuisha Programu ndogo ya Ukuzaji wa Viwanda na Programu ndogo ya Maendeleo ya Wajasiriamali. Programu hii inatekelezwa na Idara ya Viwanda.

Aidha, malengo makuu ya Programu Kuu hii ni kuongeza pato la Sekta ya Uzalishaji Viwandani pamoja na kuimarisha mazingira mazuri ya Wajasiriamali wadogo. Kadhalika, Kamati inaipongeza Wizara kwa kuwasaidia Wajasiriamali kwenda katika maonesho Tanzania Bara na hapa Zanzibar. Tunaiomba Wizara kuendelea kuwasaidia Wajasiriamali wetu ili waweze kujiendeleza kimaisha.

Mhe. Naibu Spika, Programu hii ndogo inayoshughulika na kuwaimarisha na kuwaendeleza Wajasiriamali wanaoendesha shughuli zao hapa Zanzibar. Kwa bahati mbaya, kamati yangu imesikitishwa sana kutokana na kuwepo malalamiko makubwa kutoka Kampuni ya Uzalishaji wa Sabuni ya MKIPIMILIKI kuhusu kutopatiwa kupata alama ya ubora kwa bidhaa wanazozalisha ambayo imekuwa kikwazo kwao kuingiziwa jumla ya Tzs. 300,000,000/- Milioni kwa ajili ya kuendeleza shughuli za uzalishaji wa bidhaa zao. Hivyo, Kamati yangu imeitaka Wizara kupitia Taasisi yake ya Viwango wakutane na kufanya mazungumzo na Uongozi wa Kiwanda hicho kwa lengo la kuwaelekeza kinachotakiwa kufanyiwa marekebisho na watendaji wa kiwanda hicho ili bidhaa zao zikidhi viwango vinavyokubalika na mkopo uliokusudiwa kutolewa upatikane na utumike kama ilivyokusudiwa.

Mhe. Naibu Spika, katika Bajeti ya mwaka 2017/2018, Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko imejipangia kukusanya mapato ya Tzs. 455,224,000 kupitia vyanzo mbali mbali, kikiwemo chanzo cha Mali Maiti. Kamati yangu inaishauri Wizara hii kukutana na Wizara ya Fedha na Mipango ili kukihamisha chanzo hiki na kukipeleka Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana ambayo ipo chini ya Wizara ya Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mhe. Naibu Spika, kamati yangu pia inaiomba Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko ichukue juhudi zaidi ya kuimarisha ukusanyaji wa mapato kupitia vyanzo vyake mbali mbali, ambapo hadi kufikia Machi, 2017 imekusanya jumla ya Tzs. 222 Milioni sawa na asilimia 59.7. Makusanyo hayo ni kidogo ukilinganisha na mapato yaliyokusudiwa kukusanywa ya Tzs. 371.2 Milioni. Hivyo, kwa mwaka wa fedha ujao wizara ihakikishe inaongeza mapato hasa kwa kuwasimamia vyema maofisa wanaoshughulikia na ukusanyaji mapato hayo.

PROGRAMU KUU YA UKUZAJI NA UENDELEZAJI BIASHARA

Mhe. Naibu Spika, Programu Kuu ya Ukuzaji na Uendelezaji Biashara imeundwa na Programu ndogo nne zinazojumuisha Programu ndogo ya Ukuzaji wa Masoko, Programu ndogo ya Ushindani Halali wa Kibiashara na Kumlinda Mtumiaji, Programu ndogo ya Urahisishaji Biashara na Ukuzaji Biashara za ndani pamoja na Programu ndogo ya Usajili wa Biashara na Mali. Programu zote hizi kwa pamoja zinatekelezwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, Idara ya Biashara na Ukuzaji Masoko, Idara ya Ushindani Halali wa Kibiashara, Baraza la Usimamizi wa Utoaji Leseni na Baraza la Biashara Zanzibar. Aidha, Programu Kuu hii ina lengo la kusimamia Mitaji ya Umma ili kuhakikisha inakwenda sambamba na mabadiliko ya uchumi pamoja na kuwepo kwa uwazi na usawa wa tathmini ya bidhaa zinazonunuliwa kupitia taratibu za manunuzi.

Mhe. Naibu Spika, miongoni mwa jukumu la msingi la Wizara hii ni kuyasimamia na kuyaendeleza maghala mbali mbali yanayomilikiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kwa kutathmini hilo na umuhimu huo, kamati yangu imeitaka Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kuyafuatilia na kuyatambua idadi halisi ya maghala hayo maeneo yalipo pamoja na kujua kodi za maghala hayo yanayokodishwa, kwani imeonekana mapato mengi ya Serikali yanapotea ama kwa waliokodishwa kutolipa kiwango kidogo au fedha za kutolipa kabisa vile vile tuna wasi wasi kwamba maghala mengine yanamikiwa na watu binafsi kinyume na utaratibu.

Program kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Biashara Viwanda na Masoko, Mhe. Naibu Spika, program kuu hii ya uendeshaji ya uratibu wa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko imeundwa na program ndogo tatu zinazojumuisha program ndogo ya utawala, uendeshaji wa Wizara, program ndogo ya uratibu na Mipango, Sera na Utafiti wa Wizara na program ndogo ya uratibu wa mipango sera na Tafiti za Wizara na program ndogo ya uratibu wa utekelezaji wa Shughuli za Wizara Pemba. Aidha program hii inatekelezwa na

Idara ya Uendeshaji ya Utumishi, Idara ya Mipango Sera na Utafiti na Idara ya Afisi Kuu Pemba ambayo ina lengo la kutoa huduma za uendeshaji na manunuzi kwa ufanisi.

Mhe. Naibu Spika, Wakati Kamati yangu ikipitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii, iligundua kwamba kuna kasoro za kiuandishi kwa kutofautiana majina ya Programu Kuu na Programu ndogo ziliomo katika kitabu ambacho Kamati inakitumia na kile walichokiandaa Wizara. Hivyo basi, Kamati ilishauri ni busara kasoro hizo ziondolewe ili kuwepo uwiano na usahihi katika vitabu hivyo.

PROGRAMU KUU YA VIWANGO NA TATHMINI YA UBORA

Mhe. Naibu Spika, Programu Kuu ya Viwango na Tathmini ya Ubora imeundwa na Programu ndogo moja ya Viwango na Tathmini ya Ubora ambayo inatekelezwa kupitia Idara ya Taasisi ya Viwango Zanzibar *ZBS*. Huduma inayotarajiwa kutolewa na Programu hii ni uandaaji na ukuzaji wa viwango pamoja na tathmini ya ubora wa bidhaa. Aidha, Programu Kuu hii ina lengo la kuandaa na kuimarisha viwango ili kumlinda mtumiaji.

Mhe. Naibu Spika, katika kupitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa Fedha 2017/2018 ambapo Kamati yangu inalisimamia hilo, Kamati ilielezwa kwamba kuna fedha za Miundombinu zilizohitajika kutumiwa na Taasisi ya Viwango Zanzibar kwa ajili ya kuziimarisha Maabara zilizomo ndani ya Taasisi hiyo lakini hadi kufikia Machi, 2017 fedha hizo bado hazijaingizwa kutokana na ZBS kushindwa kukamilisha baadhi ya taratibu na kukwamisha utekelezaji huo. Hivyo, Kamati yangu imeitaka Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kuhakikisha inakamilisha taratibu hizo haraka iwezekanavyo ili fedha hizo ziingizwe ZBS na kazi hiyo ianze kabla ya kumalizika mwaka huu wa fedha.

Mhe. Naibu Spika, napenda kuitanabahisha Wizara kwamba fedha ambazo Baraza lako Tukufu itaziidhinisha kwa Wizara hii ya Biashara, Viwanda na Masoko ni fedha za kodi zinazotozwa kutoka kwa Wananchi. Hivyo, Kamati yangu inaitaka Wizara kuwa makini kwa kila shilingi wanayoitumia ili yale malengo waliyoyapanga yaweze kutekelezwa na Wananchi nao wanufaike ipasavyo kwa mrejesho utakaofanywa kwa matumizi mazuri ya fedha zao.

Mhe. Naibu Spika, mwisho napenda kuwashukuru na kuwapongeza tena Viongozi na Watendaji wa Wizara hii kwa juhudi wanazochukua katika kutekeleza kazi zao pamoja na ushirikiano waliotupatia wakati wa kuipitia

Bajeti yao. Aidha, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa utulivu wa hali ya juu wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha hotuba hii.

Mhe. Naibu Spika, kwa vile Kamati yangu ya Fedha, Biashara na Kilimo imepitia, imejadili na kuyakubali mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya hii ya Biashara, Viwanda na Masoko ya mwaka wa fedha 2017/2018. Kamati inawaomba Waheshimiwa Wajumbe wote nao watumie fursa iliyopo kuijadili, kutoa mapendekezo yao na hatimae kuiunga mkono na kuipitisha Bajeti hii ili tumuwezeshe Waziri aende kutekeleza yale waliyojipangia katika mwaka ujao wa Fedha.

Mwisho nawatakia waumini wote wa Dini ya Kiislam mfungo mwema wa mwezi mtukufu wa ramadhani na tunawatakia saumu iwe maghabul**.**

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache, kwa niaba ya Mwenyekiti na Kamati yangu ya Fedha, Biashara na Kilimo, naunga mkono hoja.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mwenyekiti wa kamati sasa nina wachangiaji wanane nianze na mchangiaji Mhe. Suleiman Sarahan Said, nadhani muda utatosha ikisha atachangia Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata).

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa fursa hii kuchangia hotuba ya Wizara ya Biashara Viwanda na Masoko. Awali ya yote naweza kusema kwamba nimpongeze sana Waziri kwa kitabu chake jinsi alivyokipangilia na kutoa mwelekeo a mafanikio katika kuendeleza nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, mimi nataka niongezee kwa sababu Waziri wangu kutokana na alivyojipanga katika kitabu hichi nimemuona ana mwelekeo mzuri sana wa mafanikio. Kwa hivyo mimi nianze tu kidogo kwa kuja na mwelekeo wa Kiwanda cha Makonyo cha Wawi, niliona katika hotuba yake katika ukurasa wa 15 alizungumzia habari ya kiwanda cha Makonyo na vile vile anataka kujenga kiwanda kipya.

Lakini mimi hapa kidogo nilikuwa nataka atakapokuja kukamilisha mambo yake basi aje aniambie vizuri kuhusu hili suala la kiwanja cha makonyo kwamba pale bado panaendelea kuwa kiwanja cha makonyo pale Wawi au kile Kiwanda cha Wawi kitaondoka kwa sababu kinamaneno mengi kutokana na

hali ya mambo yaliyoko pale baina ya wananchi wanaoishi maeneo yale hali ya moshi na mambo mengine, sasa nilisikia tu kwamba kuna utaratibu wa kukiondoa sijui kukisogeza makaani au vipi au kuboresha humu niliona ana misingi ya kuboresha. Lakini baadhi ya maneno maneno ya nje yako hivyo sasa sijui atakavyokuja aje aweze kukiweka ile hali halisi ya kwamba anaonaje kwamba hali ya kiwanda kile katika mji sasa hivi.

Lakini jambo jengine nataka nimwambie Mhe. Waziri kwamba sasa hivi sisi binaadamu tuliokuwa na mawazo finyu akili zinakuwa hazijapata upembuzi zaidi jambo dogo likiwa hupati faida pale kwa pale unakuwa kama vile unachanganyikiwa au unaona kitu kile hakina maana bila ya kupima athari zake na upeo wake, kuna kipindi cha miaka ya nyuma sisi kule Pemba tulikuwa tunaona Karafuuilikuwa bei ya chini ilikuwa bado hatujajua thamani ya karafuu basi tukatokezea kuingia na hamu ya kuikata tukasema bora mabungo kuliko karafuu, athari zile zimekuja kutuumiza wenyewe kuja kuikata mikarafuu sasa karafuu tunawaniana haipo tena mikarafuu tumeshaikata tunatafunana wenyewe kwa wenyewe.

Sasa ilikuwa Waziri nimwambie kwamba sasa hivi tuna miembe mingi hasa maeneo ya Ole mpaka wakati mwengine tunafanya mpira watoto wanacheza mpira zile embe, inaweza ikawa wale hawajajua tena kwamba Serikali ina mpango gani au Wizara ina mpango gani au halisi ya zile embe thamani yake ni kubwa sana, maana yake nataka nikwambie kwamba Mhe. Naibu Spika, miembe yote ile inayozaa hatujaipanda sisi imepandwa na wazee wetu tunaona faida tu ya kula lakini hatujui thamani na miaka iliyopandwa miembe ile. Lakini inaweza ikafika hata miaka mia moja kwenda mbele lakini mpaka leo inazaa kama vile ndio inaanza sasa, sasa wengine mpaka sasa hivi tumeshaanza kuingia kiburi cha kuikata tukaona bora mlango au mapau au kupiga tanu kuliko muembe.

Sasa ningemuomba Waziri kwamba utizamwe mwelekeo hawa watu wakapata elimu kwamba hii miembe wasiikate tena kwa sababu *fruit* au *juice* zitakapokuja tena itakuja kuwa miembe yenyewe haipo, kwa hivyo ningeomba sana elimu hii ikafikishwa. Lakini pia niseme tu kwamba Waziri kama kutakuwa na uwezekano mimi nakuaminia sana basi tuwahi kutafuta viwanda vidogo vidogo vyenye *packed* hata vilivyokuwa vina vikundi kwa ajili ya hizi embe za *juice*, kwa sababu naona mpaka kule Arusha watu wanafanya *packed* nzuri tu kwenye mambo ya tomato, sasa ningeomba kutafuta wataalam nimeona kwenye kitabu umejipanga vizuri lakini huu utaalam ningeomba kwa sababu kule Arusha wenzetu wameendelea kidogo lakini sisi huku utaalam wa mambo ya viwanda bado haujakamilika. Kwa hivyo ningeomba Waziri timu

yako ikaipeleka kule Pemba ili ikafanye utafiti zaidi na kuwapa hamasa wale watu, kwa hivyo ningekuomba hili suala ulitizame zaidi katika mambo haya.

Mhe. Naibu Spika, lakini pia nilimuona katika utengenezaji wa vipodozi na manukato Waziri hili mimi naku-*support* sana unajua Zanzibar ni nchi ambayo unasema kwamba ilikuwa na utamaduni wa hali ya juu sana katika mambo mengi tu mambo ya utamaduni wa vipodozi, vilikuweko vingi na takriban tulikuwa tukizungumza kwamba zaidi ya miaka pengine mia moja nyuma watu walikuwa hata *perfume* hawaijui kwa sababu watu walikuwa wanaweka kilua na asumini juu ya kitanda basi mambo yamemaliza kazi na mishambeni na kila kitu. Sasa mimi nikuombe na Waziri wa Kilimo umwambie ile mishambeni airudishe kwa sababu kuna mkadi, misanata vitu vyote havipo tena sasa hivi ukiukuta huo mshambeni unaweza kuukuta Pemba nzima upo mmoja ule kwa harufu iliyokuwa nayo mpaka majini walikuwa wanahamia pale, usiku utamkuta anachukua maua anakwenda kumpelekea mume wake wale mashetani wako wa kike na kiume. Mhe. Waziri wewe ni mfanyabiashara hivi vitu akusaidie Waziri wa kilimo katika upandaji wa hivi vitu najua kama vitakusaidia sana kwenye mambo mengi ya manukato na mambo mengine, sasa ningeona mambo hayo.

Lakini pia ningeomba nije kwenye eneo ambalo sasa hivi nimekushukuru sana wakati wa kipindi cha nyuma eneo la viwanda lilikuwa ni pale Maruhubi, sasa hivi najua umetafuta eneo katika maeneo ya Fumba, lakini kule Pemba sijaona umetenga sehemu gani ambayo ya viwanda umeiweka kwa hivyo kama umeshatenga kama ni Micheweni au wapi ukiisema itakuwa sio jambo baya ili ikaweza kujulikana.

Jengine mimi nizungumze kwamba nikushukuru tena kwa sababu hichi kitabu kimejiweka vizuri unajua biashara bila ya makubaliano bila ya mikutano, bila ya kukutana na wafanya biashara hakuna biashara biashara ni majadiliano ya kujua hapa pana matatizo gani, mimi nikuombe sana kwanza nimeona katika Waziri anayekwenda Pemba mara nyingi ni wewe mmoja unakwenda sana kwenda kuwashajihisha watu kwenye mikarafuu, kwenye mambo gani kwenye majadiliano mengi. Lakini mimi nataka nikuombe suala la makusudi unajua katika masoko yetu ya pale Chake Chake, kwanza mimi nikwambie pale Chake Chake kama patafanyiwa biashara ya utanuzi mzuri wa biashara pataongeza pato kubwa sana la Serikali ndio mji wenyewe uliokuwa tayari ushaanza kupanuka katika maeneo ya biashara. Ningeomba pale ukaja ukawasiliana nao au ukaja ukasaidiana na hawa watu wa Halmashauri, wao wanapanga biashara ndogo ndogo bila ya kukuza sasa wewe upeo wako ni mkubwa.

Kwa hivyo ningeomba kuna maeneo kama ya pale Kuwait lile eneo sasa hivi linafanyiwa masihara masihara sijui soko mara watu hawendi nina uhakika ukitoa maelekezo likitengenezwa eneo lile basi nafasi itakuwa haipatikani, kwa hivyo ningeomba ili kuangalia mustakabali wa masuala hayo katika muangalizo huo.

Lakini mimi nikuombe tena katika ukurasa wa 51 nataka nikupe pongezi sana katika wizara yako Wizara nyingi mimi naziona kwamba zinakuwa na mashaka na wafanyakazi wake wanalalamika wanahangaika, lakini mimi katika nafasi yako hii ya Wizara yako umewasaidia sana wafanyakazi wako ambao nao bila ya ushirikiano wako wewe na wao itakuwa hii Wizara haiendi lakini umejipanga vizuri kuwasaidia hawa afanyakazi wenzako katika hali ya uhakika, sioni kama kuna mambo ambayo yanavutana vutana zaidi ya mambo mazuri ambayo yameelekezana. Sasa niweze kusema kwamba uwe wigo baadhi ya Wizara nyengine inakuwa mashaka na wafanyakazi wao sasa watu wanakuwa na kama upinzani fulani ndani ya Wizara. Kwa hivyo na mimi nikushukuru kwamba umetoa changamoto nzuri zilizomo humu kwa hivyo hiyo ningekupendelea sana.

Lakini nione katika kitu ambacho kimependezewa ni katika ukurasa wa 57 nimependezewa na neno ulilolizungumza la kutunga sera au sheria ya kumlinda mtumiaji Mhe. Naibu Spika, mpaka hivi sasa hili ni jambo ambalo linatupigisha kelele sana biashara zinazoingia tunapiga kelele, biashara zinazofanywa zinakuwa na mashaka haya. Sasa watu wanaitegemea Serikali katika kuwalinda katika biashara za nje zinazoingia maana yake sasa kama itakuwa sera hii ipo ya kumlinda huyu mlaji inawezekana ikawa kuna ubora maalum naona umeelezea vizuri katika ukurasa wako wa 57, lakini nikupongeze tu kwanza hilo neno kutunga hiyo sera au kuandaa sera ya kumlinda mtu basi pia hii inaweza ikaja na sababu nyingi pengine zina *insurance* ya chakula zitakuwa na mambo gani kwa hivyo inawezekana zikaweza kusaidia.

Lakini chengine Mhe. Naibu Spika, nizungumzie kwamba Mhe. Waziri katika jumla ya mambo ambayo nataka uyatizame mambo mengi yanafanya ugumu yanafanywa na ughali wa kitu kutokana na utendaji wake au ufanyaji wake, sasa ningekuomba kwamba kuna vitu vidogo vidogo vimashine ambavyo vinafanya kazi kiurahisi bila ya kumpa mtu mmoja ku-*packed* kwa muda wa saa mbili masaa matatu pengine ukikitia kifuko pahala tu hivi kinaweza kikatoka katika masuala kama hayo au *packed* maalum hizi kwa hivyo ningeomba kwamba hizi mashine ndogo ndogo za vitendea kazi katika hawa hawa wana vikundi vikasaidiwa sana kwa sababu mara nyingi wanatumia

mikono ndio inakuwa tabu kubwa mtu anafanyakazi katika maingira magumu sana.

Kwa hiviyo ningeomba kwamba kitu hicho kinakuwa na ugumu mkubwa kwa sababu mfanyakazi anasema mimi nafanyakazi pale kutoka asubuhi mpaka jioni nalipwa shilingi elfu fulani na kitu kile ukikiuza kwa bei kubwa hakiuziki, lakini kama utapata vitendea kati watu wawili tu wanaweza wakafanya kazi na vitu vile vikauika kirahisi zaidi, kiwa hivyo hiyo pia ilikuwa nikukumbushie ili uone kitu kama hicho.

Lakini Mhe. Waziri mimi nakuamini katika kitabu chako niende katika makundi, nenda katika biashara, nenda katika maduka, nenda katika mahoteli, nenda katika maeneo mengi wewe kwa sababu ndio kiongozi wetu wa biashara hii biashara iko ya ndani iko ya nje na wewe unatusaidia kufanya mapato makubwa ya nchi hii ya Serikali, kuna watu wanakwama kidogo sana katika biashara zao amba wanakwama kipesa inaweza kuwa hawana mfumo wa kwenda mabenki, kuna watu mpaka leo mfumo wao hawana mfumo wa kuweka benki lakini wafanyabiashara wazuri.

Lakini kuna watu wengine pia wamekwama padogo kufanya ile biashara yenyewe ikawa na wengine walishaanza ikafa pengine ni mawazo tu na kila kitu, kwa hivyo ningekuomba ukawatambua watu wote wafanyabiashara ukamuuliza huyu alikuwa akifanya biashara amekwama nini, ukakaa kitako ukamuuliza ulichokwama, aa nimekwama hichi na hichi nitakusaidia hichi nenda huku ukatusaidia kwa hali kama hiyo nafikiri hayo naamini unayaweza sana. Kwa hivyo ningekushauri kwamba na hayo uweze kuyafikia ili uwawezeshe.

Lakini mimi niseme kwamba umeona katika jumla ya viwanda ambavyo vilikuwepo na vimeondoka ni Kiwanda cha Soda na Kiwanda cha Cotex ambavyo unaweza kuvirudisha pengine katika hali yake. Lakini mimi niseme hata ungeanza na hivyo kama umeona vinarudishika hebu tuanze na hivyo vitie *speed* nzuri sana ili vionekane ili tuweze kupapatua mambo mengine, lakini Mheshimiwa jambo ambalo nataka niseme na nimeona kwamba ni kitu kidogo sana lakini viwanda ambavyo hapa kwetu tunapenda sana soseji za kuku, *sausage* za ng'ombe. Watu wamezichukia *sausage* baada ya vituko vya *sausage* hasa huko nje wakirushiwa zile *clips* zao za mashine zinazofanya *sausage* na pamoja na mambo wengine wanazichukia wengine wanaona kinyaa. Lakini *sousage* ni myama tamu ni mzuri Mheshimiwa. Sasa ikiwa ya kuku hii mashine zake ndogo mimi ningekushauri sana uzitafutie mashine ng'ombe tunao hapa,

kuku tunao wakifanya hapa hapa halali tunakula Mheshimiwa vizuri sana na hizi za nje tunaweza tukapunguza kuleta. *(Makofi)*

Kwa hivyo, ningeshauri hivi pia ukawatafuta wajasiriamali ya *sausage* maana yake wa vitu hivi wakaweza kufanya kila kitu. Lakini Mheshimiwa mimi nikusifu sana nimepata taarifa sana kule Pemba kuhusu habari ya uimarishaji wa miche ya mikarafuu na upandaji wa mikarafuu na watu. Lakini sijakusikia kwenye minazi, ningekushauri tena wizara yako iingie tena kwenye minazi uongeze nguvu ya Wizara ya Kilimo msaidiane muifufue tena minazi ni vitu ambavyo kidogo vina nini.

Lakini Mheshimiwa nimeona vikundi lakini kama hawa watu wanaoshona kofia za viua zile asili. Mheshimiwa kofia hizi saa hizi ni bei mbaya sana na watu wanashonesha halafu wanakuwa na utaratibu wa kuwatumia watu, sasa kama vikundi vyako ukivisajihisha vitu hivi ambavyo ni kofia hizi za viua ambavyo vinauzika nje sana. Basi mimi ningeona kwamba waongeza mapato zaidi na ujasiriamali uongezeka. Lakini zaidi mimi Mheshimiwa nisema kwamba hizi bidhaa ambazo naweza kusema zinazokuwa na kodi, biashara Mheshimiwa inayouzika na unayonunulika na iliokuwa inasafirishika ni biashara kodi yake iliyokuwa ni ndogo kidogo na unapoona kwamba pahali kidogo kodi imeongezeka ghafla biashara inabadilika, sasa hali ambayo Mheshimiwa inatukabili ulitizame soko la ndani. Mheshimiwa soko la ndani mara nyingi sana hapa tunategemea Dar es Salam au tunategemea Mainland.

Lakini soko lake kila siku linakuwa na machafuko ya pale Dar es Saalam katika Bandari linakuwa halikai sawa, wakifanya biashara baada ya wiki wanabadalika hivi. Sasa na mimi ningekuomba sana kwamba uwe na mtu wa kutizama lile soko la Dar es Salaam ni ujanga wa watu wetu wafanyabiashara walioko ndani au pale Bara linakuwa linabadilika badilika kwa sababu ya kodi ambazo zinakuwa zinaongezeka. Kwa sababu sisi tumeshajiachia Mheshimiwa kwamba Zanzibar katika biashara zetu za chakula Mainland au Dar es Salaam huko ndio tumekamata kwamba inatusaidia kwa chakula kwa mambo mengine kama mbatata, hata ng'ombe hata kitu gani kitu gani. Lakini sasa wewe angalia kuanzia jana tu Ramadhani ilipoanza Mheshimiwa sokoni hakufikiki ndizi imeshafika laki sasa hivi mambo yamechafuka kweli kweli na nyama ya ng'ombe itapanda juu na mahangasha.

Sasa hili soko nalo ulitizame sana kwa sababu ndio tunalotegemea ndio maisha ya kila siku. Kwa hivyo nilipenda hili uliangalie ili masuala ya ndani najua uko ndani ya nje kimataifa uko safi vizuri, lakini na ndani inategemea kwa

mtazamo mzuri sana ututizame kwa sababu Mheshimiwa maisha ya kila siku ni maisha ambayo...

Mhe. Naibu Spika: Mhe. umebakiza dakika tatu.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Maisha ya kila ndio yanayoweza tuendesha. Lakini chengine Mheshimiwa ulichonifurahisha ni ukurasa wa 45 katika suala zima la utelekezaji wa bajeti. Mhe. Naibu Spika, suala la bajeti kwa programu ya mwaka huu mimi hii imefurahika nayo kama ulivyoeleza katika kitabu chako malengo yako ya Sekta kuu ya Uchumi katika mambo haya manne naona kama hapo uloimairisha basi mimi nina uhakika kwa hii programu uliokwisha kupagwa mimi nina uhakika mwakani tukijaaliwa hatutozungumza tena hapa, tutazungumzia mambo mengine mapya kutokana na utendaji mzuri wa bajeti hii tunayokwenda nayo hii, mimi nakuaminia mtu anapoaminiwa toka enzi hizo mpaka leo nakuamini sana na nikupe pongezi sana Mheshimiwa.

Lakini cha ziada zaidi Mheshimiwa nilitaka nikwambie kwamba kwa takribani nchi zote ulimwenguni biashara hiyo, kodi hao watu gani wanategemea biashara wanaokula ndani wanategemea biashara. Kwa hivyo, wewe ni muhimili mkuu usichoke kuwasaidia watu wa kila aina maana yake viwanda watakutegemea wewe walaji wa kawaida watakutegemea wewe maana yake kila pahali unaingia, masoko ya kila siku tayakutegemea wewe. Kwa hivyo, nikushauri sana Mheshimiwa nguvu yako uitumie hivyo hivyo na Pemba usichoke kwenda na watu wa Pemba umeona hali wanavyotaka biashara kwa sababu nimeona unapowapa vitu vya kusogeza wanasogezeka na hali ni ngumu lakini wanakukubali sana.

Mimi Mhe. Naibu Spika, namshukuru tena Mhe. Waziri kwa kazi nzuri anayoifanya na mimi naipongeza hotuba hii asilimia kwa mia. Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante mchangiaji wetu wa mwisho kwa leo atakuwa Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) karibu.

Mhe. Ali Suleiman Ali: (Shihata) Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa adhuhuri ya leo kupata nafasi hii kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko kwa bajeti yake ya mwaka 2017/18.

Mhe. Naibu Spika, nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii lakini pili nampongeza sana Mhe. Waziri kwa kazi nzuri anazozifanya yeye Katibu Mkuu

na watendaji wao wote kuhakikisha kwamba biashara inakuwa ili serikali ipate maendeleo katika faida hiyo ya biashara.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri Amina ni mtaalamu tena ni mtaalamu wa dhati kabisa kwa sababu kadri ya kitabu hichi ukikisoma kwa asilimia tisini na utafute cha kuchangia. Kwa hivyo, nampongeza yeye na watendaji wake wote kwa kazi nzuri waliokaa na kufikiria na kuleta bajeti hii ambayo kama ni maelezo baada yake wafanye matekelezo ya utekelezaji wapate maendeleo ambayo tunatarajia.

Lakini Mhe. Naibu Spika, mimi nitazungumza mambo machache sana lakini nitamuomba sana Mhe. Waziri ajitahidi kwa sababu kelele hizi napiga kila leo. Bahati nzuri Mhe. Naibu Spika, Zanzibar imezungukwa na bahari narudia tena kauli hii Zanzibar kwa asilimia mia moja tumezungukwa na bahari, lakini bado la kusikitisha narudia kilio changu, kwa kuwa yeye ni Waziri wa Biashara naamini kuna wawekezaji wengi duniani au katika nchi mbali mbali ulimwengu huu tuliokuwa nao kama wataitwa hasa katika Tanzania leo ya Viwanda waje kuekeza katika sehemu ya kuweka viwanda vya kushindika samaki au kuhifadhi samaki na kusafirisha nje. Naamini Mhe. Spika, kama tutasimama vizuri na kupata vyombo vizuri vya kuvulia nje na wizara ikasimamia vizuri tunahakikisha kwamba Zanzibar tutakuwa pato kubwa tunalitegemea kwenye samaki. Mwanza ni sehemu ya ziwa lakini wanasafirisha samaki wengi sana yaani Sato wale wanapelekwa nje kupata fedha za kigeni na kuendeleza nchi yao.

Kiwanda cha samaki Mheshimiwa kwa Unguja kikiwekwa Nungwi, Kiwengwa, Makunduchi na Pemba vile vile kikawekwa Mkoani, Wete, Vitongoji mfano nachukulia katika maeneo ya bahari kubwa hiyo, tunaweza kufanikiwa sana Mhe. Naibu Spika, kwa hifadhi ya kuweka samaki hao na kusafirisha nje na vijana wetu kadhaa nategemea watapata ajira kwa kuendeleza maisha yao. Hili naamini liko katika wizara zinazohusika moja Wizara ya Fedha nayo inahusika, Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi inahusika.

Lakini na yeye kama Waziri wa Biashara ni changamo moja kuhakikisha kwamba anawatafuta wawekezaji kuja kuekeza katika sekta hii ambayo inautajiri mkubwa wa samaki mameli ya nje yakuja kuvua hapa wanachukuwa samaki waenda zao. Tulishuhudia Mheshimiwa. Mhe. John Pombe Magufuli Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliwahi kuwa Waziri wa Uvuvi alilikamata meli kubwa sana mwisho akaitwa samaki wa Magufuli. Ile ni njia moja wapo kwamba bahari yetu ina rasimali kubwa ambayo kama tutajipanga

vizuri tukiendelea, serikali itapata faida kubwa ya mapato yake kupitia sekta hii.

Lakini jengine nimemuona Mhe. Waziri kaweka malengo mazuri katika ukurasa 57. Shirika la Biashara la ZSTC nampongeza, kuhakikisha kwamba karafuu hazipotei na karafuu tunazifanyia kazi ili pato letu liongezeke. Hasa baada ya changamoto ya Serikali kusema kwamba tunaongeza bei sasa hivi inayohistahiki, ili karafuu zisipotee kwenda kuuzwa magendo, kwa uhodari wake Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake ziara zake za mara mara anazokwenda kuhakikisha kwamba biashara hii inalenga kuhifadhi mali yetu isipotee hiyo nampongeza Mhe. Waziri. Kwa sababu usimamizi unataka wa kushtukiza hata Mhe. Magufuli, anaweza kushtukiza jana tulimuona Hospitali ya Muhimbili kwenda kuwakagua wagonjwa, siku nyengine utamkuta bandarini, siku jengine utamkuta wapi mimi napongeza sera hiyo na muelekeo huo kuwa ndio mzuri wa kuhakikisha rasilimali yetu inabakia katika mikono ya Serikali.

Lakini nasikitika kidogo Mhe. karafuu, narudia juzi nilizungumza hapa ni zao kubwa la Taifa hili ya nchi yetu ya Zanzibar, kwa upande wa Pemba upande wa kulia unakuta karafuu, upande wa kushoto minazi, bahati mbaya humu haikutiwa hata nukta moja kusema angalau uhifadhiwe kiasi gani, namuomba Mhe. Waziri akubuke tunakotoka, tulikuwa na viwanda vya mafuta ya nazi hapa, yanasafirishwa nje Tanzania Bara na kwengineko, lakini leo vimepotea havipo kwa sababu minazi rasilimali imekatwa, tena inakatwa makusudi hii inasikitisha. Nimuombe Mhe. Waziri kwa kuwa zao la minazi lina faida na nasema tu Mheshimiwa kutokana na mafuta yanayopatikana katika kuzalisha, viwanda vya mafuta ya nazi basi yanaubora kuliko mafuta mengine haya tunayotumia.

Kwa sababu wazee wetu tunakotoka walikuwa asilimia 99% unatumia mafuta haya, hawana mafuta kutoka nje, lakini leo bahati mbaya Mhe. viwanda havipo, minazi haipo sijui tunaelekea wapi, kwa hivyo nimuombe Mhe. Waziri wa Biashara haya ni maombi yangu naishauri wizara inayohusika kwa kujibu maswali mengi leo, lakini tujue kwamba minazi ni hazina na historia ya nchi yetu kwa upande wete wa Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Spika, lakini jengine katika ZSTC hao hao walikuwa wanasafirisha pilipili hoho, leo zao hilo limepotea kabisa halipo. Pilipili hoho tulikuwa tunazalisha kwa wingi, hasa katika maeneo ya ukanda wa pwani katika sehemu za mawe, pilipili hoho ilikuwa ni zao kubwa ambalo wananchi wetu walikuwa wanafaidika. Pamoja na ugumu wa uzalishaji maana ukenda kuzichuma pilipili

hizo uwe lazima utafute utie katika sufuria ili upoe mikono, lakini najua kwa utaalamu wa sasa hivi kama zingekuwa zipo au zitakuwepo basi utaratibu mpya upo basi watu wanaweza kuvaa *glove* wakachuma bila ya matatizo. Nimuombe Mhe. Waziri haya madogo madogo yanasaidia kukuza uchumi wetu katika nchi yetu hasa Sekta ya Biashara.

Lakini pia Mhe. Naibu Spika, niwapongeze kwa dhati wafanyabiashara ambao wanaingiza michele katika nchi yetu wanaingiza unga wa ngano, sukari, mafuta na nyenginezo kwa kuhakikisha kwamba Zanzibar inabaki salama kuwa chakula kipo cha kutosha, lakini pia Mungu atunusuru lisitoke wakati wa ukame yaani kipingi kirefu cha jua kali, tulishuhudia kwamba Zanzibar tulikuwa na mchele wa kutosha, sukari, unga wa ngano, sembe pamoja kuwa limepanda bei sana lakini watu waliokuwa na wenye uwezo ananunua anapata riziki yake. Kwa hivyo nimuombe Mhe. awape hamasa sana waingize bidhaa hiyo siku hadi siku kwa kuendeleza wananchi wetu wasipate shida.

Lakini pia wafanyabiashara wa vyombo vya ujenzi, hawa wanatusaidia sana na mpaka leo tunasema vifaa hivyo vingi vipo, vinaendeleza wananchi wetu na viwasaidia kwa hivyo nimuombe Mhe. Waziri, kwa kuwa kuna viwanda vikubwa Tanzania Bara vimejengwa sasa hivi, narudia hapa kidogo, Dangote Mtwara Mhe. sasa hivi tunasema ni mfano katika nchi zetu za Afrika, Dangote kufika sasa hivi mfuko mmoja ya saruji hapa Unguja au niseme Zanzibar inauzwa shilingi 13,200 tunatoka elfu 18,000 ilikuwa mpaka elfu 20,000 saruji, lakini Dangote kuingia saruji yote imekwenda bei poa 13,000 na kidogo 14,000 kwa hivyo niseme kwamba hii ni changamoto ya maendeleo katika nchi ya viwanda.

Lakini pia kuna kampuni ya Kichina imekeeza eneo kubwa la Bagamoyo huku, kiwanda vya *tiles* leo naamini Zanzibar au Tanzania hawatoagiza *tiles* kutoka nje, kwa sababu wenzetu wamekwenda vizuri na sisi kama kuna madogo madogo yanatufaa ni vyema tukawaomba wenzetu waje waekeze hivi vidogo vidogo ambavyo vinakaribia na wao. Kwa sababu Mhe. naamini bado uwezo wa maeneo tunayo, na sehemu tunazo maana wawekezaji wetu wa Zanzibar utashtukia sana wanakwenda mahoteli sio mbaya, lakini viwanda tunavisahau. Kama mwenzangu alivyosema Mhe. Suleiman hapa tukiwekeza katika tungule Mhe. matungule tele saivi mfano, au wakati wa tungule kilo shilingi 300/- huwa hatuna vya kuyafanya, ukenda kwenye ndimu, machungwa, maembe aliyezungumza Mheshimiwa mwenzangu aliyetangulia haya ni maeneo Mheshimiwa viwanda vidogo vidogo vinaweza kusaidia watu sana, tunaziona juice za Bakhresa za chungwa za ndimu za kerot sijui na kila kitu kwa hivyo

nimuombe Mhe. Waziri haya niliyoyazungumza ayazingatie ili wananchi wetu wapate kujiajiri zaidi.

Kama wakulima wetu watakuwa na uhakika wa mazao yao siku za humbo, tunaita siku za humbo maana ile biashara inakuwa nyingi huwa huna pa kuipeleka,wanajua wanaipeleka pahala fulani inanunuliwa kwa ajili ya kuendesha kiwanda fulani, tutafanikiwa zaidi, Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo machache niseme tu kwamba nampongeza tena Mhe. Waziri, Katibu Mkuu, Manaibu Watendaji wake wote lakini ningemuomba sana Mheshimiwa tuwashajiishe wafanya biashara wetu waongeze kuleta biashara zao ili wananchi wetu wapate nafuu, sisemi mwezi Ramadhani tu, lakini mwezi wa Ramadhani na miezi yote tunaelea nayo wananchi wanataka kupata bei nafuu juu ya kuishi salama katika nchi yao.

Baada ya hayo naunga mkono hotuba hii kwa asilimia 100% sina tatizo Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe niwashukuru sana kwa wale wote wamechangia lakini kabla ya kuakhirisha, nina tangazo linatoka Ofisini kwa Dau, Tangazo hili linasema kuwa kama kuna Mheshimiwa yeyote, aliyepotelewa na kitu chake afike Ofisi kwake. Hususan Waheshimiwa wanawake. *(Makofi)*

Baada ya Tangazo hilo Waheshimiwa naakhirisha kikao hadi kesho saa 3:00 asubuhi.

(Saa 9:00 mchana Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 30/05/2017 saa 3:00 asubuhi).